

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, ISILO CONSTITUENCY,  
HELD AT MODAGASHE TOWN**

**ON**

**May 14, 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARING, ISILO CONSTITUENCY, HELD AT MODAGASHE TOWN ISILO  
ON 14<sup>TH</sup> MAY 2002**

**Present:**

1. Com. Ibrahim Lethome
2. Com. Dr Githu Muigai

**Secretariat Staff in Attendance:**

1. Solomon Mukeinon – Programme officer
2. Vincent Wataku – Assistant Programme officer
3. Grace Gitu – Verbatim Reporter

Meeting started at 10:00 a.m. with Com. Ibrahim Lithome on the chair.

**Com. Lethome:** Twamshukuru Mwenyezi Mungu Sulhana waTaala kwa kutuwezesha kufika hapa, lakini kabla hatuja anza kikao chetu cha leo ambayo siyo siku yetu ya kuzungumza ni siku yenu kama nitakavyoelekeza. Kawaida yetu huwa tunaanza kwa kutaka baraka za mwenyezi Mungu Sulhana waTaala. Kwa hivyo namuomba Sheikh Husein kama yuko hapa karibu na mimi atufungulia kwa dua halafu tuweze kuanza. Sheikh Husein Kutoka Garbatula. Haya Sheikh wa Modogashe. Sheikh wa Garbatula amesema hapa ni mahali pa Sheikh wa Modogashe. Karibu Sheikh utuambie jina lako na (?)

**Sheikh Aleo:** Mimi ni Maalim Aleo wa Modogashe. (*Prayers in Islam*)

**Com: Lethome:** Munajua tunapokuja katika boma ya watu, lazima kwanza tutake kukaribishwa na Mwenyeji wetu ijapokuwa hii kikao yetu leo ni ya commission sisi ndiyo tulitangaza tukaita watu lakini kuna wale wenyeji wetu. Lakini kwanza kabla hatuja endelea ningependa kuwajulisha, tukubalini hebu tusikizaneni, tumeshaanza mkutano kwa hivyo naomba tusikizane. Kabla hatujaanza ningependa kuwajulisha wale ambao tumekuja nao kutoka Nairobi kisha nitawaeleza kazi ambayo imetuleta hapa na masharti yale ambayo tutafuata hapa, hii shughuli ambayo imetuleta hapa. Kwanza sisi tuko hapa mbele yenu tuna wakilisha Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya. Kwanza lugha ya kiswahili inafahamika na watu wote wanafahamu. Mnafahamu nyote lugha ya Kiwahili? Mnafahamu?

**Response:** Tunafahamu.

**Com: Lethome:** Baadaye kama kuna mtu hafahamu nitaomba Sheikh Kwa mkutasari kidogo ataeleza kwa kiBorana. Mimi kiBorana yangu inaishia pale yanavaa peke yake. Tumekuja hapa kuwakilisha Tume ya Marekebisho ya Katiba. Tume ambayo inazunguka kila mahali Kenya mzima kuweza kuchukuwa maoni ya wananchi. Na tumekuja hapa sehemu hii ya Eastern Province na Modogashe ni mahali ya kwanza ya Eastern ambayo sisi tunatembelea. Ma-Commissioners wengine wako sehemu yote ya Kenya lakini sehemu hii ya Modogashe ni ya Kwanza. Tumemaliza Central Province, tumemaliza Coast Province, sasa tuko hapa Eastern Province kuchukua maoni ya wananchi.

Wale ambaao tukonao hapa, nitaanza huko, kuna yule Kijana anaitwa Vincent. Kazi yake ni ku-record kila maneno ambayo ina zungumzwa anaandika. Hatutaki maneno ya mtu ye yeyote iweze kupotea. Karibu na yeye tuna huyo dada yetu Grace, Kazi yake ni ku-recordi kwa machine kila neno ambayo inazungumzwa lazima ichukuliwe na iweze kuingia katika Katiba. Yeye kazi yake ni ku-record. Karibu na mimi hapa ni ma-programme officer ambaye anaitwa Solomon, yeye ndiye anasimamia idhara ya ofisi yetu tukiwa inje, kwa hivyo yeye ndiye msimamizi wa kazi hizi zote na atashugulika pia na kuchukuwa record kwa sababu hii ni kazi ya (?) ya historia. Kila mtu atakayezungumza jina yake itakuwa hapa ndani na maoni yake na sign yake. Kwa sababu tunataka hata baada ya miaka mia moja, wale watoto ambaao hawajazaliwa wataangalia ni akina nani ambaao waliweza kushiriki katika kutengeneza Katiba mpya ya Kenya. Hivi sasa tunasema kwa kizungu, it is history in the making. We are making history now. Tunatengeneza historia ya nchi hii, hata baada ya miaka mia tano mingine records hizo zitakuwako kuonyesha wale walioshiriki katika kutengeneza Katiba mpya ya kenya. Kwa hivyo kuzungumza utakuwa hapa utaweka kidole yako na utaandika jina lako. Kisha tunaye mtu ambaye anasimamia shughuli zetu hapa katika district ya Isiolo naye ni Sheikh Dima Jillo, huyu. Yeye ndiye muakilishaji wetu Katika district ya Isiolo yote. Yeye atakuwa na nyinyi mpaka mwisho wa kazi hii. Hata sisi tukirudi Nairobi huyu ndiye macho yetu katika Isiolo district. Mimi naitwa commissioner Ibrahim Lethome, kuna mwenzangu ambaye ilikuwa afike hata saa hii tumepiga simu Isiolo kuangalia kama amefika, anaitwa Commissioner Dr. Githu Muigai, na mwininge wa tatu ambaye kwa bahati mbaya alipatwa na ugonjwa hakuweza kuja. Lakini aje ama asije shughuli itaendelea. Kwa vile Mwenyezi Mungu ametuwezesha kufika hapa shughuli haitakwama itaendelea.

Kisha ningependa tu kabla sijaongea masharti ya hii kazi yetu kwa sababu hata wale vijana munacheza mpira katika uwanja wa mpira si kuna masharti yake ambayo lazima ifuatwe? Hata wakati unaendesha gari kuna masharti yake kila mahali kuna sheria yake kwa hivyo tuna zungumzia sheria yetu leo katika kikao hiki, ni kitu gani nitawaeleza lakini kabla ya hapo ningemuomba kama Chief wa eneo hii yuko, azungumze maneno moja au mbili dakika mbili tu nampatia kwa sababu hii si baraza leo, ya kutukaribisha tu halafu tuanze kazi yetu. Kwa hivyo Chief kama yuko karibu tafadhali, tuko nyumbani kwake atukaribishe halafu tuendelee.

**Chief Hussein Ajiboru:** Bwana Commissioner, Bwana Ibrahim, na wageni ambaao wanaandamana naye kutoka huko Nairobi

headquarter, Mwakilishi wa district Bwana Dima Jillo, Maulama wako hapa, wazee, na vijana saalam aleikhum?

**Response:** Aleikhum Salaam

**Chief Hussein Ajiboru:** Yangu ni kukaribisha kweli hii ni historia katika karne hii ambayo Commission imefika hapa Modogashe kuchukuwa maoni ya wananchi. Nafikiri kila mtu ako na uhuru. Hii siku ni siku ya kipekee, kila mtu ajitokeze atoe maoni yake ile ana ona ni mzuri itatusaidia kujenga Katiba ya Kenya yetu. Nafikiri yangu kwa chache nasema karibuni, muwe nyumbani asanteni. Mini ni Chief Husein Ajiboru, mimi ni Chief wa Modogashe location.

**Com. Lethome:** Asante Bwana Chief, sasa tunajisikia tumefika kwa sababu mwenye nyumba ameshaa tukaribisha. Asante sana Bwana Chief. Sasa tuingie katika masharti yetu. Tunasema hivi, kwanza mnajua historia ya nchi hii ni kuwa, ikifika mambo ya kuzungumzia habari ya sheria watu wanakuwa na uoga, ati nitasema hivi halafu nitashikwa, nitasema hivi halafu baadaye nitaenda kuulizwa maswali, hiyo kitu ondoa katika akili yako kabisa. Munasikia. Mambo ya uoga imekwisha, tuko katika wakati ingine sasa. Ile wakati wa kuogopa kusema ile kitu unataka imekwisha, bora tu usivunje sheria lakini nakuhakikishia hi Commission imeundwa na sheria ya bunge ambayo imesema kila mwananchi atakuwa na uhuru wa kusema vile anataka. Kile unacho hii ndiyo fursa yako useme leo. Hakuna kuogopa, hakuna kila kitu, bora tu usivunje sheria useme vile unavyotaka na ikiwa kuna mtu ambaye atafuatwa na polisi baadaye ati ulisema kitu fulani ulisema kitu fulani, tujulisheni sisi tutachukua hatua. Kwa hivyo ukija hapa usiogope kutoa maoni yako yoyote bora tu usitukane mtu wala usitaje jina la mtu. Hii sio kikao ya campaign ama siasa, kikao ya siasa ndio watu wanatukanana huko. Hii ni kikao ya kusema unataka nchi hii itawaliwe namna gani kina mama karibuni hapa. Kina mama mkaribie msikae bali hata ninyi tunataka maoni yenu ninyi ni Wakenya pia kwa hivyo mkaribie,

Kwa hivyo ya kwanza utoe maoni yako bila kuogopa kabisa. Mumesikia hivyo hiyo tumekubaliana? Msiwe na wasiwasi, na mimi nawambia hivi katika dini ya kiislamu munaambiwa usidhulumu wala usikubali kudhulumiwa sababu ya kusema hivyo ni kwamba miaka thelathini na nane watu wameumia kwa sababu ya sheria baya tumeachiwa na mkoloni. Sasa serikali ya Kenya imesema wananchi Wakenya hii sheria ya zamani imekuumiza unataka nini? Halafu unyamanze useme siwezi kuzungumza itakuwa umekubali kudhulumiwa na hata dini imekataa dhulma ama sivyo? Halafu pia tunasema wakati unapotaka mabadiliko mabadiliko hayawezi kukaa unalala kitandani halafu mabadiliko ikuje. Lazima ufanye bidii ama sivyo.

**Response:** Ndivyo

**Com. Lethome:** Mnajua ndege anaitwa shindre? Shindre mnajua? Shindre anakula chakula ama hakuli?

**Response:** Anakula.

**Com. Lethome:** Na aka na shamba, Shindre?

**Response:** Mungu ndiye anamlisha.

**Com. Lethome:** Mungu anamlisha lakini analala kwa ile nyumba yake ama anatoka? Anatoka ama hatoki?

**Response:** Anatoka.

**Com. Lethome:** Basi sasa ndio unaambiwa mabadiliko hayawezi kutoka mpaka wewe mwenyewe ufanye bidii. Kama vile shindire unajua mtume (?) anasema (?). Kama ungemtegemea Mwenyezi Mungu hakika ya kumtegemea angekupatia riziki vile anampatia shindire. Lakini shindire anatoka na wewe lazima utoke ama sivyo? Sasa ndio fursa yako hii. Sema unataka kitu gani. Hata chakula Mwenyezi Mungu ndiye anakupatia lakiniunalala kitandani baridi inakuja kwa kitanda yako (?) haikuji? Lazima ufanye bidii. Sasa lazima useme mnataka kitu gani. Sharti ya kwanza hii hakuna uoga, kuogopa.

Ya pili, maoni ya watu ni tofauti. Mtu akitoa maoni na wewe hukufurahia maoni hiyo usimpigie kelele hiyo ni maoni yake. Mnasikia? Hiyo ni maoni yake, tuheshimu maoni yake, tusimpinge wacha azungumze amalize wewe utapewa nafasi yako utazungumza. Hiyo sharti ya pili.

Sharti ya tatu, ni kuwa unapewa kama una maandishi tutakupatia dakika tano ueleze kwa ufupi yale maneno ambayo yako kwa maandishi yako. Kama huna maandishi unataka kuzungumza tutakupatia dakika kumi. Sasa wacha ni kupatie siri ya kutumia hizo dakika kumi. Ukianza hapa kutuletea story nyingi, hiyo dakika kumi haikutoshi. Ukija hapa, anza kupendekeza, unajua maana ya kupendekeza? Mnasemaje kwa ki-Borana kupendekeza.

**Response/Translation:** (to Borana )

**Com. Lethome:** Eeh, unatupa mapendekezo. Kwa mfano kama unataka kuzungumzia mambo ya elimu, usianze kusema skuli zetu mbaya, sema unataka nini. Ikiwa pengine, hauridhiki na polisi vile walivyo, usianze kulete story ya polisi sijui wananiitisha kitu kidogo ama nini, sema unataka kitu gani. Chief anakuumiza, usilete story ya Chief kukuumiza, sema unataka siku za usoni chief awe namma gani. Unasikia hiyo ndiyo kupendekeza. Dakika kumi zikiisha nitakugongea kama kuna maswali ye yeyote tutakuuliza halafu tutaendelea. Kwa hivyo hayo ndio masharti ambayo tuko nayo hapa. Kwa hivyo tutaita mtu jina, ukija hapa useme jina lako uanze kuzungumza, usitaje jina la mtu usitukane mtu, zungumza kwa uhuru vile unavyotaka. Tumesikizana sasa? Tumesikizana? Aya bismilaa tunaanza.

Kina mama tutachukua maoni vipi kwa sababu wanaogopa wanakaa bali na tumalazimishwa na sheria kuwasikiza pia. Sasa wazee tutao nafasi kwa akina mama mkae upande mmoja, kina mama wakaa upande mmoja najua lazima tuheshimu

dini na mila kwa hivyo wazee kaeni upande mmoja kwa sababu sisi sheria inasema lazima tusikize kina mama pia. Kina mama karibieni hapa mukae pande moja tafadhalini. Kina mama karibuni. Wazee kaeni pande moja tafadhalini. Wazee patieni kina mama nafasi pande moja halafu mujue lazima mtu afanye registration kabla hajaitwa hapa, kwa hivyo hiyo desk tumeweka hapo ni ya registration unaenda unaandiksha jina yako halafu italetwa hapa nitaita jina kwa hivyo kama hujajiandikisha, kina mama tafadhalini, hata ninyi ni Wakenya pia, karibieni hapa, sisi tutafungwa tukikataa kuwasikiza ninyi tutakuwa tumeenda kinyume na sheria. mujiandikishe huko kina mama, jiandikisheni huko halafu mnganje tutaita majina yenu mimi najua munataka kwenda kupika tutawaita mbele mbele muende mukapikie wazee musitandikwe. Haya bismilaa tunaanza na mtu wa kwanza, Ali Haji Goret. Ali Haji Goret kama unawenza kuja hapa mbele. Karibu.

**Mr. Ali Haji Goret:** (In Borana dialect, through translator)

**Translator:** Ndugu yetu anasema yeze anatoa maoni yake ya kwamba anataka Kadhi, Wakenya katika ofisi ya Kadhi ipewe nguvu kabisa iweze kufanya kazi yoyote ambayo inayohusika na Waislamu na pia Wakadhi waongezwe wapewe mshahara mzuri, na katika kila Division tuwe na Kadhi ili waweze kuwatumikia wananchi kwa uzuri, na pia Makadhi wetu wawe na freedom, wasiwe chini ya judicial wawe wanaweza kuendesha mambo yao bila kuwa chini ya judicial commission.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Anasema tunataka, maoni yake anasema ya kwamba anataka Kadhi katika Kenya wapewe nguvu, sheria yoyote ambayo inayohusika na Waislamu, iwe ni Kadhi anashugulikia ikiwa Muislamu labda ametumia labda vitu vya kumlewesha akaleta uharibifu ama akakosa adabu basi Kadhi achukue hatua kwake ikiwa ni mauaji imetokeam makosa yoyote baina ya Wailamu hii kesi iwe ni Kadhi ambaye mwenye kushugulikia.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Anasema kwamba tunataka Kadhi mtu ambaye atachaguliwa katika ofisi yeze awe na Islamic education isifunganishwe na certificate kuhusiana na Magistrate kama elimu ya Magistrate ya kawaida isifunganishwe naye awe anatosheka awe na Islamic education ama kuhusiana na Islamic law basi hiyo itamtosha kuwa Kadhi.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Appointment ya Kadhi anasema itahusika na

(?) alamaa tunapendekeza kwamba tuwe na  
iwe inakuwa established na hii ofisi ya mfuti ndiyo pamoja na  
kuhusika na ma-appointment ya Kadhi na hii

(?) ambaye ina mfuti ofisi ya mfuti pia  
(?) ndiyo watakuwa katika kazi yao  
(?) na ofisi ya mfuti lazima iwe inakuwa pia funded na

government na serikali inasaidia kwa sababu sisi Waislamu ni tax payers na tunalipa kodi katika hii inchi kwa hivyo pesa yetu lazima iwe inatusadia tupate board kama ya

(?) ambayo inahusika na mambo ya Uislamu na tuwe na mfuti ya Islamu ambayo ofisi ya Kadhi yote itakuwa chini yao.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Anasema kwamba pendekezo yetu ni kwamba hii (?) ama ni Assembly of Muslim Scholars pamoja na mfuti yao wao ndio watakuwa mouthpiece ama wao ndio watakuwa wanazungumzia waislamu katika shida zao na mambo yao yote na waondio watakuwa baina ya Waislamu na serikali. Matatizo ya Waislamu yote wao ndio watakuwa wanashugulikia.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Anasema leo sisi Waislamu tuko 1/3 rd ya Kenya na tunapendekeza kwamba kulingana na idadi yetu sisi Waislamu ambayo ni idadi kubwa lazima tupewe mawaziri wa kutosha katika cabinet yetu isiwe chini ya sita ama tano mpaka sita lazima waziri wa Waislamu wawe kutoka tano mpaka sita kulingana na idadi yetu ambayo tuko 1/3<sup>rd</sup>.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Anasema ndugu yetu ya kwamba pendekezo yake pia elimu ya kiislamu ambayo inafundishwa katika mathali za Islamu ziwe zinatambulika, kama elimu yoyote inatambulika katika Kenya elimu ya Islamu pia inatambulika kabisaiwe inakuwa recognized walimu wetu wa mathalisaba ambao wanafundisha katika Islamic Institutions wawe wanatambulika certificate yao iwe inatambulika serikali iwatambue kabisa na Institutions za Islamic zote zitambuliwe na iwe inakuwa supported by the government kwa sababu sisi ni watu ambao tunalipa, we are taxpayers.

**Com. Lethome:** Malizia malizia tafadhali.

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Ndugu yetu anasema yaliyobaki mandugu wataongeza labda

**Com. Lethome:** Ngoja (?) kuna swalii.

**Com. Lethome:** Ningependa tu ufanuzi, amezungumzia habari ya Kadhi, ningependa tu azungumzie habari ya appeal kutoka

kwa Kadhi, mahakama ya Kadhi angependekeza kitu gani kwa sababu kwa sasa nikienda kwa Kadhi, na kama hukuridhika na hukumu ya Kadhi appeal unaenda High Court na High Court, wale Ma-judge wako High Court sio waislamu, sasa ningependa

(?) apendekeze angependa kuwe na appeal ya Kadhi ama tuendelee hivyo hivyo waislamu wapeleke appeal yao kwa High Court?

**Mr. Ali Haji Goret:**

**Translator:** Anasema Kadhi amependekeza kwamba Makadhi wawe kutoka Division, yule wa Division akishindwa mtu anaenda mpaka District, akienda akishindwa hiyo lazima ipatikane Court of Appeal ambaye ni higher kama ni Mombasa ama ni Nairobi hadi Makadhi wengine watasikiza hiyo Kesi.

**Com. Lethome:** Tumpate Arthun Eden, haya Arthur una dakika kumi ya kupendekeza.

**Mr. Arthun Eden:** ( In Borana dialect, through interpreter)

**Translator:** Jina yake anasema ndugu mimi naitwa Maalim Arthun Eden.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anasema anamurudishia Mwenyezi Mungu Sulhana Wa Taala shukrani sisi kukusanyika hapa na kutoa maoni yetu.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Mimi maoni yangu nitatoa namna gani inahusu dini.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Nasema katika Kenya leo sisi hani hatuna uhuru hatuna ngivu sana sisi Waislamu, haki yetu haina nguvu.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anasema ofisi yetu ya Kadhi pamoja na (?) wa Islam ni dhaifu sana hatuna nguvu hatuna support.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anasema mapendekezo yake ni kwamba tunataka serikali itambue dini yetu ya Islam na tupewe nguvu na freedom ya kutosha.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Waulamaa wa Islam wapewe support wawe wanatambulika kila pahali.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anasema hata sasa leo Ulamaa ikatika uislam ishirikishwe ni Islamic Institution hata mshahara hakuna.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Hakuna kitu ambayo tunayo sasa.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anasema yake ni fupi hii tu anataka dini yetu itambuliwe na tuweze kupewa uwezo kila pahali.

**Com. Lethome:** Hapa tu swalii moja. Je umezungumzia habari ya Makadhi unasema Makadhi watambuliwe lakini hukufafanua, ungependa watambuliwe kivipi? Hivi sasa si wanatambuliwa na serikali pia.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anasema lazima Kadhi wapewe nguvu ya kutosha, nguvu yao iwe inapanuliwa kabisa na pia wapewe mishahara ya kutosha walingane na watu wengine kama wale wa magistrate wengine.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Na anasema hata ulamaa wale wanafundisha katika Islamic Institution serikali iwasaidie kifedha.

**Translator:** Anasema tumpate dhaifu sana.

**Mr. Arthun Eden:**

**Translator:** Anatoa kiasi hiyo maoni yake.

**Com. Lethome:** Tumpate Abdi Abei. Abdi Abei, kuja hapa useme jina yako na uanze kupendekeza.

**Mr. Abdi Abei:** (In Borana dialect, through translator)

**Translator:** Anasema ye ye anaitwa Sheikh Abdi Abei.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anatoka katika msikitii Jamia hapa Modagashe.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anasema anzungumzia kutoka dini ya Islam.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anasema sisi tumezaliwa katika hii nchi na sisi kama Kenyan citizens tuna haki.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anasema haki ya ibada tunayo kiasi fulani lakini mambo ingine ambayo inatuhusu sisi hatuna haki ya kutosha katika welfare yetu.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anasema sisi leo ukiangalia Waislamu wako maalimu wako watu wasomi ambao wanafundisha katika Islamic Institutions lakini hawatambuliki ya kwamba kweli wanafanya kazi mzuri ama hata kupata usaidizi yote kutoka pande ya serikali.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anasema yeye pendekezo yake ni kwamba Islamic Institution iwe inatambuliwa ikiwa mtu ni Imam katika msikiti serikali imutambue iweze kum-support huyu Imam ikiwa ni mtu ari muslim scholar pia serikali iweze kum-support na atambulike kabisa na shahada yake itambulike na hata kifedha aweze kusaidiwa.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Anasema mimi maoni yangu yule ndugu yetu ambaye ametangulia hapa Sheikh Ali maoni yangu ni kama maoni hiyo tu.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Kumalizia anasema ya kwamba sisi ile yake ni hiyo tu, serikali lazima iweze kutusaidia katika kuonyesha kuinua dini yetu katika hii nchi.

**Mr. Abdi Abei:**

**Translator:** Amemalizia hapa.

**Com. Lethome:** Haya hakuna swali yoyote unawenza kukaa chini. Wazee munajua tumeweka akina mama pande hii ndio wawezza kupata nafasi ya kuzungumza naomba hawa wazee hebu rudini pande hii tafadhalini kwa sababu karibu nitawenza kuita

akina mama. Hii nafasi yote nataka iwe ya akina mama mpaka kwa Chief hapa pande hii yote tuache wazi kwa sababu ya akina mama. Halafu pia nawaomba make kimya tuna-record mkipiga kelele tutapeleka record ya Modagashe kelele ndani yake. Kwa hivyo naomba wakati mtu anazungumza tukae kimya ndiyo record iweze kwenda ikiwa safi huko. Hii cassette inapelekwa Nairobi utaenda Modagashe tunasikia kelele tu hakuna mazungumzo ya maana. Kwa hivyo mkae kimya musikilizeni tafadhali. Mazungumzo mtazungumza huko baadaye, kila siku mko pamoja lakini leo peke yake tupatiensi nafasi.

**Translator:** (to Borana)

**Com. Lethome:** Haya tunaendelea sasa, Abdilahi kuna list ya akina mama? Have they registered have the ladies registered? Abdilahi can I have the list with the ladies? Maalim Mahamoud Sheikh.

**Mr. Mahamoud Bora:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Sheikh anasema anaitwa Maalim Mahamoud Bora.

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema yeeye ni Sheikh ambaye anafundisha watoto wa Islam dini.

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema yale ambayo alikuwa angezungumza mandugu wametoa maoni mbele yake na maoni yake inalingana ama ina-ambatana na ile Masheikh wametoa mbele yake.

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema hana maoni ningine ya tofauti ya kando.

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema anataka hii dini yetu tuwe supported kabisa.

**Com. Lethome:** Umesema huna maoni ingine? Amesema waislamu wapewe haki sawa na watu wengine. Si ndiyo?

**Mr. Mahamoud Bora:** Ndiyo.

**Com. Lethome:** Uko na kitambulisho wewe mzee?

**Mr. Mahamoud Bora:** Ndio.

**Com. Lethome:** Ulipopata hiyo kitambulisho ulipata kwa urahisi ama ilikuwa ngumu kupata kitambulisho?

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Mzee anasema wakati alipopata kadi yake hakupata shida sana.

**Com. Lethome:** Watu wengine wanapata shida wakitafuta kadi ama namna gani?

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema watu wanaona wengine wanapata shida sana kuipata kitambulisho.

**Com. Lethome:** Na mshajua ni kwa nini wanapata hii shida?

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema hakufikiria sana namna hiyo.

**Com. Lethome:** Sasa angependa iendelee hivyo hivyo watu wapate taabu wakati wa kupata kitambulisho na passport ama angependelea mambo yabadilike katika sheria mpya?

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema angelipenda kila mmoja apate kipande yake na passport yake kwa njia ya urahisi.

**Com. Lethome:** Halafu tutamuliza, vile mfumo wa serikali vile ulivyo kila kitu kiko Nairobi, angependelea iendelee hivyo hivyo ama angekuwa na mapendekezo mengine?

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema angalipenda kuona serikali imekuja karibu pahali mkono wake unaweza fikia kila mtu kwa urahisi apate mahitaji yake.

**Com. Lethome:** Zamani mzee, mimi naona wewe ni mtu wa zamani, si ndiyo?

**Mr. Mahamoud Bora:** Ndiyo.

**Com. Lethome:** Zamani chief alikuwa akichaguliwa, siku hizi anateuliwa, ungependelea kitu gani?

**Translator:** (to Borana)

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema anataka chief awe anachaguliwa na wananchi si kuteuliwa.

**Com. Lethome:** Na angependa elimu ya chief iwe kiwango gani?

**Translator:** (to Borana)

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema kitu moja elimu ni elimu ambayo Mwenyezi Mungu si lazima awe msomi sana lakini kuna hata elimu ya kuzaliwa lakini mimi napendekeza pia awe na elimu ya kiwango fulani aweze kuongoza watu kwa uzuri.

**Com. Lethome:** Hiyo kiwango fulani ndio tunataka kujua.

**Translator:** (to Borana)

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema anataka chief wetu awe amefika kiwango cha form 4.

**Com. Lethome:** Kitu ingine nataka kumuuliza, unajua nimeona munashida ya kutoa maoni ndio nawasukuma kidogo sasa, kuhusu M.P wako, M.P wako sehemu hii ni nani? Unamjua?

**Translator :**(to Borana)

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anamjua. Anasema Dr. (?)

**Com. Lethome:** Sasa unajua tunapochagua Mbunge kwa sasa sheria ilivyo anakaa huko miaka mitano kwa bunge. Awe mzuri awe mbaya huwezi kutoa yeye mpaka miaka tano iiishe. Sasa katika hii sheria mpya ungependa mwananchi awe na uwezo wa kumuita tena akiwa ameenda hukoamekuwa chuche, amekuwa maziwa lala huko tuwe na uwezo wa kumuita tena ama vipi? Unajua chuche, maziwa lala, eeh, akienda akilala huko tuna haki ya kumuita tena ama vipi?

**Translator:** (to Borana)

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema anataka kama hawezি kufanya kazi vizuri tumurudishe tumuite kabla ya kumaliza miaka yake tano.

**Com. Lethome:** Na kuhusu viama vingi nya kisiasa sijui ako na maoni gani kuhusu hiyo?

**Translator:** (to Borana)

**Mr. Mahamoud Bora:**

**Translator:** Anasema vyama vingi multi-party si bayan anapendezwa.

**Com. Lethome:** Haya asante mzee wangu. Poleni nawaaulizia maswali kwa sababu ninaona maoni imekwama haitoki, sasa inanibidi nisukume sukume ndio itoke. Haya Abdillahi H. Ngonjobe, Senior Chief.

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Asante sana Bwana Commissioner na wazee ambao mumefika pamoja na secretariat akina mama Salam aleikum. Mimi kwa jina ninaitwa Abdillahi Ngonjobe, mimi ni senior chief kutoka Sirichwa location, nafikiri wengi wanajua, mimi ni mtoto waHaji Ngonjobe Diba ambaye alikuwa chief nyakati za ukoloni. Haji ngonjobe ni mtoto wa Diba Ngurubala ambaye ni senior chief wakati wa ukoloni kwa hivyo mimi leo ni chief si kuchaguliwa kama kingdom lakini hata hivyo bahati labda nimekuwa chief leo na nafikiri nawaongoza vile niwezavyo.

Kama tunavyojua sisi jamii ya Waborana ama Wasomali wale wanaishi huku, sisi tuna tradition tuna ile culture ambayo ina tunalinda system ambayo inakaa kama system ya serikali yenye kama inawachiwa kutawala hawa watu, haiendi pingamizi na dini yetu ya Kiislam. Nafikiri kama vile munavyo kumbuka wakati fulani kutoka karibu 1895 hadi mwaka wa 1963 sisi tulikuwa tunatawaliwa na wazungu ambaye ni koloni, alikuwa na sheria na sheria ambayo amejitengenezea ili aweze kuongozan hawa watu kwa vile anapenda yeye mwenyewe. Pia munajua vile mulikuwa mumetawaliwa, ingawa sheria yetu kidogo huwa inaangaliwa ilikuwa imepuuzwa, hakuna mtu alikuwa amekubaliwa kufanya sheria yake. Sisi tulikuwa na sheria, Borana walikuwa na sheria ya kutosha. Mborana alikuwa na sheria ya kumnyonga Mborana ambaye amea mwenzake, Mborana alikuwa na sheria ya kuweka faini ye yote ambaye alikosea mwenzake ndugu yake. Mborana alikuwa na sheria mingi, Constitution ya Boran ni kubwa hata kushinda hii ya serikali, lakini imepuuzwa na hakuna mtu anaangalia. Sio tu wakati wa mkoloni, hata leo sheria ya KiBorana imepuuzwa, ile ada yao ambayo wanataka kujihukumu naye haikubaliwi, haina nguvu, sio eti kwa sababu haibatani, inagongana na ile ya kidini, la! Kwa sababu wale wanatuongoza hawajui ya kwamba kuna sheria yetu ambayo ni mzuri kushinda ile sheria ameleta. Hata wakati Lancaster House ilikuwa imeundwa sisi tunasikia tu story. Hatukushugulishwa, sisi ni binadamu tukiwa hapa, hatukushugulishwa, kuna mzee wa miaka sabini hapa wakati wa Lancaster House alikuwa ni mtu mzima, hakushuguliswa. Hakuna Constitution alikuja kutushugulisha kama vile tumeshugulishwa leo.

Leo hii tunataka maoni yetu ichukuliwe kikamilifu kabisa kwa sababu, ninasema hiyo Lancaster House ilikuwa ni kama historia.

Wakati mimi nataja Lancaster House, labda hata mimi nimeiona tu kwa kitabu ndio nimejua lakini wengi wetu hatujui lancaster House ni nini na sheria gani iliundwa huko hakuna mtu anajua na ile sheria inatengenezwa kule haimbatani na sisi. Sisi ni wafugaji kama vile munajua, ng'ombe yetu leo haina dhamana na leo katika central province, kahawa iko na dhamana, majani iko na dhamana lakini ng'ombe yetu leo unaona hakuna dhamana na kitu ambacho tunaishi nacho, na unajua ile product ng'ombe iko naye kahawa haina hiyo product. Leo hii ulimwengu ile kitu ambayo iko na product, by-product nini, chakula na kila kitu iko nayo, hakuna kitu inashinda mifugo na leo hii mifugo haina dhamana hata kidogo. Hata Kenya leo inaleta nyama kutoka nje, I mean jeshi ya Kenya leo inakula nyama ya Zimbabwe, sijui Botswana na ngombe yetu hapa haina soko ngombe inakufa kila siku. Mbuzi zinakwisha afadhali za koloni ngombe huwa inanunuliwa ingawa wanaokota kundi yao ndio wanafanya hivo lakini hata hivo ni afadhali.

Kama vile ninasema sisi tuko na ile system ambayo inajulikana kama Gathers system. Tunataka turudishwe katika hali ya Gathers system, ile ambayo inaambatana kulingana na dini yetu. Ile ambayo haipingi dini yetu. Mimi ninge-recommend ama ningesema ya kwamba customary law yetu iwe recognised, itambuliwe kama sheria ya serikali. Sisi tujihukumu na sheria hiyo. Najua hata kama Kenya nzima kama ingechukua hiyo sheria ya KiBorana ya Gathers system, nina hakika tutaendeshwa kwa njia nzuri na kila mtu atatosheka nayo.

Tungependa system ya serikali iwe karibu na wananchi kwa hali ya kuleta majimbo. Majimbo ingetufaa sana vile mimi naona kwa sababu ni serikali ambayo iko karibu na watu, ni serikali yetu ambayo sisi tunajidai nayo. Tungependa local authority iwe empowered, ipewe nguvu sio local authority ambayo leo anachaguliwa na council la kumi na nane, la! Tunataka local authority ambayo inaongozwa na chairman ambaye anachaguliwa na kila mtu katika hiyo district mzima. Sisi kama jamii ya Borana ama Wasomali wale amba wanaishi huku ni kama watu amba wamesahaulika. Wengine wameenda bali sana na sisi. Watu wako angani na sisi tuko chini na ardhi, tunataka tuletwe karibu na wengine. Tunataka tupewe education ya bure, elimu kwa watoto wetu ya bure kwa miaka ishirini ili tupatane na wengine, sio hata miaka kumi, tunataka miaka ishirini. Kama vile unajua Bwana Commissioner unakubali na mimi jana wewe ulikuja umeona wewe vile barabara inakaa Sugutu leo watu wa Siricho location hawako hapa, Samburu location hawako hapa, wangepeana maoni yao, we have very poor infrastructure, tunataka tupatiwe barabara ya kutosha. Sisi tuko na product nzuri kushinda product ingine Kenya ambayo ni ngombe, mbuzi, ngamia, maziwa ya hiso mali zote. Tunataka tuletewe KMC karibu hapa hapa hatutaki KMC ambayo inakaa Nairobi ili kupatia wale Kikuyu ama Wakamba wako huko. Tunataka KMC ambayo inafaidi sisi, KMC ambayo iko karibu na sisi. Product hii iko hapa kwa nini KMC haiko hapa? Ndio ninasema ukoloni ama wale walitengeneza Constitution walikuwa wamejitengenezea kwa situation yao hawajatengeneza Constitution ambayo inafaidi watu, inafaidi wengine. Sisi tumesahauliwa kama binadamu tunadanganywa kwa nini? Leo hii unaona fish factory iko wapi? Fish factory iko Thika na fish inatoka wapi? Fish inatoka Kisumu. Fish inatoka Pwani, kwa nini fish factory hapana tengenezwa Pwani ama Kisumu? Mkikuyu amejitengezea hiyo sheria, hatutaki hiyo sheria. Tunataka hii ya sasa hii. Nafikiri kwa haya machache asante sana na ninaomba, tafadhali sana musiogope kutoa maoni hii ni wakati muhimu sana.

Maoni (in Borana)

Peana maoni yenu tafadhali sana bila kuficha kwa sababu utajuta baadaye kama wewe apana peana maoni yako. Asante sana Bwana Commissioner.

**Com. Lethome:** Imo tu swali, umezungumzia habari ya majimbo, tungenda upendekeze, hayo majimbo unataka yawe katika daraja gani? Yawe katika mkoa, district, katika location yani location yako iwe ni location yake peke yake ama vipi?

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Wakati nimesema majimbo kweli nimebakisha mambo mengi. Majimbo hatutaki majimbo ambayo tunashikana na Eastern Province, sisi tunataka majimbo yetu, sisi tunajitosha. Lithome Tunataka mpaka yake Isiolo, Marsabit na Moyale, inatutosha.

**Com. Lethome:** Umezungumzia habari ya councillors, chairman wa council ama mayor wawe wamechaguliwa na watu wenyewe sio kuchaguliwa na wale councillors peke yao. Na je hao ma-councillors ningependa kiwango yao ya elimu iwe kiasi gani?

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Ma-councillors ningependa wawe watu wako na elimu ya kiwango ya juu

**Com. Lethome:** Kiwango gani?

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Kuanzia form 4 na awe mtu makamu wa kutosha.

**Com. Lethome:** Na kuhusu majimbo tena, watu wengi wanaogopa kwamba majimbo italeta ukabila, sasa ukizungumzia jimbo lenu lianzie Isiolo, Marsabit na Moyale, na je ikiwa mimi ni Mmasai na niko na mali yangu sehemu hiyo nina nyumba, nina shamba yangu nitafanyiwa nini tukipata majimboa?

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Sisi wajamii ya Borana kama wewe bado jua ni watu amba wanapenda wale watu wanaishi kati yao hawasumbui, sisi tunapendanga watu ikiwa wewe Msomali, na wewe ni adui pande ingine, wewe Mkikuyu adui pande ingine, lakini ukiishi kati yetu unakuwa mtu ambaye ako na usalama wa kutosha kushinda wengine wote.

**Com. Lethome:** Asante Bwana Chief.

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Kidogo tu ningerudia Bwana Commissioner, vile nimesema ma-chief, ma-chief leo mimi si kuchaguliwa, mimi nimekuwa appointed na serikali lakini ukiona ma-chief wenzangu, wengine wengi wetu, hatujachaguliwa. Ni vizuri ma-chief pia wachaguliwe kama wako, wachaguliwe na watu, watu wachague wale ma-chief wanataka wenyewe hata

kama ni mimi niondolewe, niondolewe, lakini iwe ni yule chief anafaa watu. Kwa hivyo ninasema kwa sababu leo hii wale ma-chief ambao wameandikwa ninaona wengine ni vitaya ya ma-chief, ya askari wengine ni nani, leadership imepotea, asante sana.

**Mr. Abdillahi Ngonjobe:** Asante sana Bwana Senior Chief. Ibrahim Ngoricha, Kadugu Vila, Kadugu Vila karibu mzee. Unaanza kwa jina lako.

**Mr. Kadugu Vila:** Jina langu ni Kadugu Vila.

**Mr. Kadugu Vila:** (in Borana dialect through Translator)

**Translator:** Anasema jina lake anaitwa mzee Kadugu Vila.

**Mr. Kadugu Vila:**

**Translator:** Mzee anasema mimi pendekezo yangu ni kwamba sisi Waislamu katika Kenya lazima tupewe haki kamili.

**Mr. Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema katika Kenya leo tuna dini tofauti mingi,

**Mr. Kadugu Vila:**

**Translator:** lakini sisi dini yetu ya dini ya Islamu sisi tunanyanyaswa hatuna haki kamili.

**Mr. Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema sisi kama waislamu dini yetu sisi hatujauda, hajijatokana na mwanadamu, sheria yetu si sheria ambayo imetokana na mwanadamu, ni sheria ambayo imetokana na mwenyezi Mungu, tupewa sheria yetu ya kiislamu.

**Com. Lethome:** Tupe, pendekezo. Pendekezo ni?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema sisi tunataka tuhukumiwe na ile kitu ambayo kitabu yetu inasema ya Koran.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema katika Isiolo District pia sisi kama hapa haki yetu hakuna hata kidogo.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema hata haki ya ubinadamu na utu hakuna.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema tupewe haki yetu kikamilifu.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema leo sisi hata tukimalizwa hapa hakuna serikali inakuja kutuangalia.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Hata wanyama wa msituni wana haki.

**Com. Lethome:** Sasa angetaka wafanye nini? Kwa mfano angetaka serikali ifanye nini?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema tunataka serikali iangalie mifugo yetu, serikali iangalie maisha yetu, mtu akifa serikali iangalie bona huyu mtu amekufa, iweze kufuatia, sasa kwa hii hatuna

**Com. Lethome:** Iangalie kuwatafutia maji, au msikuliwe na wanyama wa msituni ama vipi, mnataka nini?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema kwa mfano leo mali yetu ikichukuliwa na watu adui, watu wamekuja wamechukua mali, wameiba majambazi, hakuna serikali inafuata ile mali.

**Com. Lethome:** Ungetaka nini?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema lazima mali yetu ipewe security ya kutosha na serikali, sisi raia tupewe security ya kutosha.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema anataka serikali iangalie nchi yetu kwa uzuri.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema hata siku za ukoloni mtu akiawa hapa, anafuuatiwa mpaka yule mtu muuaji apatikane, leo hakuna.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema wakati hata wa ukoloni mali ikiibiwa inafuatiwa mpaka hiyo mali inarudishwa, leo hiyo mali hairudi.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema anataka hiyo. Anasema sisi tuko na council hapa Isiolo distict, tunataka council yetu ipewe power nguvu.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema power ipewe. Anasema kwa sababu sisi tumeumia na tumekuwa wa mwisho, sisi hatujakaribiana na serikali, serikali imekuwa bali sana na sisi.

**Com. Lethome:** Anataka ifanye je?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema anataka regional, serikali ije karibu na sisi.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema serikali ikija karibu basi services kwa wananchi itakuwa karibu.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Sisi kwa sababu tumesahauliwa, kwa sababu serikali imeenda bali na sisi.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Sisi hatujui hata serikali ni kama mtu imekuwa kitu geni, ni bali sana imekuwa hata geni kwetu.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Sheria inaundwa Nairobi. Anasema sisi tunataka iletwe katika sehemu yetu ndio iweze kuundwa kama ni kitu yoyote inatengenezwe itengenezwe katika sehemu yetu, kama ni province ama.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** kama serikali inakuja karibu, kila kitu tutapata.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema ile kitu yoyote tutapitisha iwe serikali pamoja na sisi wenyeji ndio tunafanya pamoja.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema ile Constitution ya zamani ambayo imefanywa na wakati huyo wa wakikuyu, haikutusaidia chochote.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Vile saa hii alikuwa chief ametangulia mbele yangu, distict tatu.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema leo hii tukiangalia North Eastern Province ni district tatu tu zimekuwa Province mzima hata sisi leo lazima tupewe Isiolo, Marsabit na Moyale.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** (?) tumeshindwa hiyo, anasema kama ikishindwa hiyo tatu ikitaka iongezwe ingine labda tuongezewe Samburu district ama tuongewe Tana River district.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Kama tutakuwa kama zamani tu,

**Kadugu Vila:**

**Translator:** tukiwa chini ya Eastern province vile tuko sasa anasema taabu yetu maisha haitakwisha.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema ile vote ambayo serikali inapeana Eastern province haifiki Embu na Meru na Machakos inakwishia hapo hapo, sisi hakuna kitu tunapata pande hii.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Council yetu ikipewa nguvu, yule chairman wa council ama mayor,

**Kadugu Vila:**

**Translator:** councillors wasimuchague hasa,

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Raia wenywe wamuchague. Chairman wa sasa wa council,

**Kadugu Vila:**

**Translator:** yule mtu ambaye ma-councillors wanamtoa

**Kadugu Vila:**

**Translator:** ma-councillors tu ndio wanamchagua sasa.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Chairman wa council achaguliwe na wananchi asichaguliwe na councillors kabisa.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema mimi napendekeza kwamba mtu yelete ambaye anaongoza awe (?)

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Hata kama ni chief, hata kama ni D.O, hata kama ni D.C, mtu yelete kiongozi awe elected hatutaki mambo ya appointment.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Tusiletwe mwingine ambaye amekuwa appointed pale.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema wale watu wametumaliza ni hao watu wamekuwa appointed. Sisi tunataka watu elected.

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema hata sasa wako.

**Com. Lethome:** Unawenza kuwa unataka kama ni D.O awe ni mtu local, D.C awe mtu local, P.C awe mtu local pia?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema namna hiyo, anataka D.C awe local, D.O awe local, na mtu yote.

**Com. Lethome:** Asante mzee kwa maoni yako, swali moja tu, saa hii nikiwa mgojwa hapa nitapelekwa wapi? Sasa hivi nikiugua hapa nitapelekwa wapi?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema labda ile iko karibu sana ni Isiolo.

**Com. Lethome:** Sasa ninyi watu wa Modagashe mumeridhika na hiyo mambo hospitali ile iko karibu iko Isiolo?

**Kadugu Vila:**

**Translator:** Anasema hatutosheki. Anasema mzee, kama hospitali, kama ni mashule, vitu vyote hizi services ziwe zinakaribishwa kwetu.

**Com. Lethome:** Haya asante sana. Ibrahim Ngoricha. Yuko ama hayuko? Haya tunaendelea. Haya, tunaendelea, Abdilahi S.Oman. hayuko? Abdulzak zatani, Zatani, hakuna. Abubakar B. Nguyo, Yuko? Ibrahim S Osman Dida.

**Mr. Ibrahim Dida:** Kwa jina naitwa Ibrahim Dida. Kwanza nishukuru Mwenyezi Mungu Sulhana wa Taala ametuleta hapa pamoja. Yangu ni kugusia mambo ya dini. Hapa mbeleni kuna Sheikh wetu amezungumzia lakini mimi nitataja tu yale hajaongea juu yake. Ya kwanza ni kuhusu structure of government. Kuhusu structure of government, the post of Vice President na Deputy Prime Minister nataka ipatiwe ndugu Muislam kama kwa mfano ukienda nchi yetu ya jirani ya Tanzania the Vice President ni muislamu kwa hivyo sisi wale ambao katika Kenya 1/3 tunafika ya Kenya mzima. Kwa mfano yani sisi tuko 30 million people in Kenya, na waislamu ni around 10,000 kwa hivyo tunataka yani president akiwa ni mkristo lazima tupatiwe Vice President awe ni muislamu ama Deputy Prime Minister awe ni muislam kama yani serikali itakuwa na Prime Minister.

**Com. Lethome:** Wewe unapendekeza iwe na Prime Minister ama isiwe na Prime Minister?

Mimi napendekeza iwe ya Prime Minister. Jambo la pili ambalo nitagusia nikuhusu wanawake. Sheria yetu ya kislamu inaangalia haki ya wanawake na watoto, haki ya wanawake na watoto. Sheria yetu ya kiislamu inaangalia zaidi haki ya wanawake na watoto kuliko haki zingine zote. Inapeana nguvu sana kama kuangalia maslahi ya wanawake na watoto kuliko yani haki zingine binadamu ndugu waislamu. Kwa hivyo ninataka kuhusiana na hii mambo ya wanawake na watoto shuguli zote ama kesi yote ambayo inahusiana na watoto na wanawake ipatiwe kwa ofisi ya kadhi. Kadhi awe anaangalia maslahi ya watoto na wanawake pia, na kuhusu wanawake wanaofanya kazi ama civil servants, wanawake waislamu ambao wanafanya kazi wakati mabwana zao wamekufa katika sheria za kiislamu huyo mwanamke anatakikana akae nyumbani kwa muda wa miezi nne na siku kumi. Kwa hivyo nataka yani serikali ipeane leave ya miezi nne na siku kumi with full payment.

Na jambo lingine ni kuhusiana na financial institution. Tunataka Islamic bank iwe established in Kenya. Sisi waislamu watu wengine wanaumia kuchukua loan, na loan Mwenyezi Mungu ameharamisha katika Quran

(?) ameharamisha. Kwa hivyo tunataka Islamic Bank yani tukiwa tumechukua loan hatutaki loan ambayo inarudisha pamoja na interest hiyo Mwenyezi Mungu ametukataza, kwa hivyo tunataka nini? Islamic Bank na iwe tunapatiwa loan ambayo haina riba.

Jambo lingine ni kuhusu marginalization. In many cases sisi waislamu tunakuwa sidelined, tunaumizwa, tunadhulumiwa, kwa mfano katika kazi waislamu ni wachache, Kenya nzima ukienda kila ofisi utakuta wakristo ama wakafiri wengine. Upande wa kazi tumedhulumiwa, waislamu ni wachache. Katika kupata birth certificate tunapata shida lakini watu wengine wanapata haraka sana. Na pia katika mode of dress, yani sisi katika mashule kwa mfano, tunakatazwa watu wasivae full hijab kama ni

wanawake na mavazi mengine kama tukivaa kanzu tunachukuliwa sisi ni kama watu wazimu ama ni terrorists katika Kenya ndugu waislamu. Na pia katika kupata passport, ni shida sana waislamu kupata passport ni shida katika Kenya. Kwa hivyo inatakikana nini, sisi tuharakishiwe wakati tunatafuta passport na many others kama kutakuwako na zingine.

Na pia pointi yangu ya mwisho ambayo nitagusia ni kuhusu public. Kwa mfano bus, ma-bar ya pombe, vitu kama miraa, hizi zote katika sheria ya kiislamu hatutaki, kwa hivyo katika sehemu ambazo hii dini itakuja kutawala hatutaki kitu inahusiana na bar ya pombe na pia tujue kwamba miraa iwe categorised kamani drug, hiyo ni mambo baya. Na mwisho kabisayani watu wasichukue islamic education mtu akijifunza diniyani serikali ya Kenya isishtuke kwamba kama sisi tunaenda kujifunza mambo ya uharibifu ama mambo ya terrorism. Kwa hivyo yani serikali ya Kenya sisi tukijifunza dini yetu wasituchukue kama sisi ni terrorists in the country. Ni hayo tu Bwana Commissioner.

**Com lethome:** Umesema kuwa waislamu hawajapewa nafasi za kazi unajua kazi inapatiwa watu kulingana na kiwango chao cha masomo, na ukiangalia ni kweli kuwa kiwango cha masomo sehemu ya uislamu iko chini sana. Kwa mfano kuna university ngapi North Eastern Province, na Coast province na sehemu zingine za uislamu. Ungependekeza nini kuhusu elimu ama wakae hivo hivo.

**Mr. Ibrahim Dida:** Kuhusu elimu, ni nataka serikali ya Kenya ipeane nguvu, katika masomo ya dini ya ki-Islamu, kama mfano madrassa, watu wengi leo wamekosa elimu kwa ajili Islamic madrassa, hata wale walimu ambao wako hawangeweza kufunza kwa ajili ya kukosa mshahara. Kwa hivyo ningependa walimu wa madrassa wote waku chini ya Ministry of Education, na wawe paid by the government alafu ikifanywa namna hiyo nafikiri sisi wengine wote tutakuja kupata elimu hiyo. Na haita kosekana nafasi ya kazi.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo kazi kwa muislamu ni madrassa tu, kusomesha madrassa hakuna kazi ingine.

**Mr. Ibrahim Dida:** Sio madarasa peke yake mbali kata secular education, tukiwa secular education pia, kuna nafasi ya kazi kupatikana ni ngumu sana.

**Com. Lethome:** (?) Wafanye nini ndio wapate hiyo secular education wafanywe nini na serikali.

**Mr. Ibrahim Dida:** Iwe established university iwe hapa alafu hiyo university ita kuwa ina employ watu wa kiislamu na pia katika shuguli zingine kazi yote ambayo serikali inaandika watu, pia waislamu waandikwe.

**Com. Lethome:** (?) wengi wana lalamika hawawezi kupeleka watoto skuli kwasababu hawawezi kulipa school fees, unapendekeza kitu gani.

**Mr. Ibrahim Dida:** Ningependa serikali ipeane free education mpaka mwisho

**Com. Lethome:** Mpaka which level?

**Mr. Ibrahim Dida:** Up to university ikuwe free.

**Com. Lethome:** Mnajua imelazimika niwasukume sukume kwasababu maoni yenu yana kwama kwama. Tunamuita sasa Muhammed Madera alafu tutaanza kuita akina mama sasa. Muhammed Madera.

**Mr. Muhammed Madera:** Mimi naitwa Muhammed Madera kwa majina yangu, na ni mutu ambaye anatoka Modogashe.

**Com. Lethome:** Hapo kuna story nyingi hapo tafadhalii.

**Mr. Muhammed Madera:** Mimi kwa jina naitwa Muhammed Madera, na natoka Modogashe location pande ya Isiolo. Yangu ni kurudishia shukrani Mwenyezi Mungu kutupatia sisi nafasi ya leo kukuja kujiundia sheria ambayo inaweza kututawala kesho sababu tulikuwa na utawala ambayo sisi wenyewe hatujajiundia. Kwa hivyo ya leo ni bahati.

Nikianza maoni yangu, maoni yangu ya kwanza, lazima kwanza wewe uwe na serikali ndio upendelee vile inaendeshwa. Maoni yangu ya kwanza, ningependekeza tuwe na serikali ambayo iko karibu na wananchi. Kama majimbo, ambaye tuko na sisi, na wataona shida yetu usiku na mchana na tuta kaa pamoja usiku na mchana ndio wanaweza kutuendesha. Hizi majimbo, tumesema hivi ya kwamba, tutakuwa na jimbo ya mkoa lakini hatutaki kuwa na mkoa ambaye tunashikana kwa wakati huu, kwasababu sisi watu wa mifugo, ambaye tokona masomo yetu chini, ambaye tuko na experience ya kazi chini, hatungependa tulaliwe na hao watu. Tungependa kuundiwe (?) yetu, ambaye kama Isiolo, ama Moyale ama Marsabit, akiona ni kidogo anaweza kungezwa mahali kama Tana River ama samburu. Tuwe na jimbo zetu ambaye tunaweza kujiendesha. Na tumependekeza ya kwamba, county council ama serikali ya mitaa, ipatiwe nguvu ambayo inaweza kuendesha district mzima. Chairman wa council, achaguliwe na wananchi, ambaye atakuwa na masoma ya hali ya juu, ambaye anaweza kuwa na masomo ya degree, ambaye anaweza shikilia nafasi ya D.C. kama district nzima yeye anaweza kuwa D.C. wa hiyo district. Achaguliwe na wananchi, kwa vote ya wananchi aingie huko. Ndiye anaweza shikilia serikali ya hiyo district yote. Lazima tuwe na ministries wote saa hii wana kusanyika huko Nairobi. Lakini tukiwa na serikali yetu hapa kando, lazima tuwe na ministries yetu ministries, ambaye inaweza kuendesha sector yote, kama ni ya elimu, kama ni ya afya, kama ni nini. Kwa hivyo lazima ipatiwe kwa serikali ya

(?) nguvu ambaye inaweza kutuendesha katika district hii kwa masilahi ya wananchi wa hiyo district yote kwa jumla.

Yangu ya pili, ni kuhusu ardhi. Hii ardhi ambayo sisi tunaishi kwa wakati huu, ni kama ardhi hakuna mwenyewe, ambaye inaitwa

Trust Land, ni miji ambayo ni ardhi ambayo hakuna wenyewe. Tungependa hiyo jina iondolewe kabisa. Jina yakusema trust land iondolewe kabisa, na hiyo jina ikiiondolewa hiyo ardhi iwe ya community ya hiyo area. Afadhali iitwe kwa mapendekezo yangu, community land ya hiyo area. Kwa sababu kama sisi Isiolo south, tuko community anaishi juu ya ardhi, lakini kama tumeshalewa hapa, babu na babu na babu, na tunaita ardhi yetu, na serikali inasema sio yao, na sasa niya kila mtu, tunaona kama sisi hapa tunakaa kama kitemporary. Tungelipenda hiyo jina ya Trust Land iondolewe kabisa kwa sheria mpya ya leo, iwekwe community land ya Isiolo South. Na Kila division, iwe na document yake ya hio ardhi, kama ni (?) division, iwe na document yake ya hiyo community ya hiyo division, kama ni ya Garbatula, kama ni ya (?) ikatakatwe na division, na iwe na hiyo ardhi iwe na watu amba wanakaa kwa hiyo division, lakini kati yetu wale wa-Isiolo, wasiwe shida. Inaweza kuwa na kiwanja ya malisho, mnawenza tembeleana, asiwe shida katikati yetu. Kwa hivyo kwa ardhi ni hiyo.

Ya pili, (?) sisi ni watu wa malisho, ambayo tunafuga ngamia, mbuzi, ngombe na pundu, na ile ma-district ambayo tunapakana sana, ni yote ni madistrict ya mifugo kama hiyo. Ningependa kwa mapendekezo yangu, iweke kwa sheria ya leo, kila mtu wa hiyo district, alishe mifugo yake kwa district yake. Badala sasa mimi ni mtu wa Isiolo, na niende nihame Garissa, na mifugo yangu, ama Marsabit, ama Moyale, nataka iwekwe kwa sheria, isiwe kila mtu alishe kwa district ya mwingine. Kama mimi niko na mfugo, lazima kama mimi ni mtu wa Isiolo, nilishe katika district yangu. Mifugo asitambae kwa district ya mwingine kila mtu alishe kwa district yake.

Kuhusu haki, kama mimi ni m-Kenya, mwananchi wa Kenya, kuna haki lazima ni pate katika government yangu, kwa serikali yangu lazima nipate. Na ningependa nipatiwe haki yangu yote. Kama usalama, lazima serikali achunge usalama yangu na mifugo yangu. Usiku na mchana, kwa njia yote. Lazima serikali iangalie afya yangu na mifugo yangu. Lazima serikali aidimishe wananchi wote lazima wa (?) kwa elimu, kujenga shule, na (?) ya shule yote. Serikali aelimishe kwa kila kitu.

Afya. Saa hi sisi tuko kilometre karibu mia mbili kutoka Isiolo. Chochote ikitokea hapa, mgonjwa ghafla, hakuna mahali pa kukimbishwa. Katika mahali, location yote, location pahali wananchi wako, lazima ilet karibu matibabu karibu na wananchi. Kuwe na hospitali, kuwe na madaktari abao wako na ujuzi, hiyo lazima iwe katika sheria. Na tukikosa tunashtaki serikali wakati hiyo. Lakini kama bado haiko sheria ni hatari. Kwa hivyo ningependekeza kwa sheria, hospitali iwe mahali iko wananchi wote.

Na chakula, kama wananchi wana tawala, pengine ukame ukitokea, kuna haja gani wananchi wakufe na njaa. Lazima walishwe, mpaka wakati mambo yatakuwa mzuri, hiyo serikali lazima wachukuwe jukumu la kulisha wananchi.

Maji. Utakuta mahali kama modogashe, kuna wakati tumekosa maji mwaka moja, kama siyo NGO pengine ya ActionAid, kama donor si ActionAid, wananchi Modogashe hakuna kwa pande ya serikali. Hiyo ni jukumu ya serikali, ihakikishe wananchi wamepata maji safi kila pahali. Mfano kama sasa mifugo, kuna mahali iko na nyasi, hakuna maji. Kama sasa hakuna

maji, nyasi pekee, hakuna kazi. Kwa hivyo ningependa kuwekwe kwa sheria, lazima pahali ya malisho, yote iwe na maji ya mifugo na ardhi ya mifugo iangaliwe. Na tena yangu ingine.

**Com. Lethome:** Ya mwisho.

**Mr. Muhamed Madera:** Sisi tuko na mifugo, na kama tuko na mifugo yetu hakuna sheria. Naona serikali anangangana na kutafutia soko kahawa, majani kila kitu, kwanini mifugo yetu hakuna dhamana, na inaonekana sis mifugo hii, hakuna dhamana. Tungependa hii mifugo iwe na dhamana, serikali ichukuwe hii mifugo kama shamba ile inaichukuwa. Sasa naona KMC pahali inawekwa, factory ya maziwa kule inawekwa, na maziwa iko hapa na nyama iko hapa, sasa ikiwekwa huko, sisi ni kuonyesha hapa hakuna binadamu na mifugo. Sisi hatutambuliwi, hatuchukuliwa kama ni wananchi wa Kenya, sisi tunachukuliwa kama tuko tu ni wanyama hata wanyama iko dhamana kuliko sisi. Tunechukuliwa, hiyo mifugo soko ya mifugo, usalama ya mifugo, afya ya mifugo, malisho iangaliwe iko katika sheria.

Yangu ya mwisho. Sisi kama watu wa Northern Kenya. Tuko na shida kidogo. Kama mfano watu wa pande hii, kuna wakati, ametokea mambo ya emergency, mambo ya shifta. Na sema kweli, tulikuwa na serikali namna hiyo ambayo iko na uhuru, na hiyo serikali badala akiona mtu iko na makosa anashtakiwa, watu wamemalizwa, mifugo yao yamemalizwa. Sisi tunataka hiyo ridhaa ya watu yetu ilipwe. Tunataka mifugo yetu ambayo inamalizwa ilipwe. Na kama umetumaliza, watu wamekwisha, mifugo imekwisha, na katika sheria, ile mtu anahukumu mtu kunyongwa ni judge pekee, kama sasa askari amechukuwa jukumu ya kumaliza watu, na hiyo bunduki, wananchi wameisha, mali imeporwa, tunataka bidhaa ilipwe. Na tena, kama shifta hiyo tena imetokea namna hiyo, amemalizia sisi mifugo na mali na sisi tumbeki nyuma ya wakenya, tuko nyuma kabisa masomo hatuna, maendeleo hatuna, barabara ndiyo hiyo, hospitali ndiyo hiyo, kila kitu ndiyo hiyo. Nataka serikali ichukuwe jukumu ya kutufikisha na wananchi wa Kenya, kwa kila kitu, kwa masomo, kwa maji, kwa kila kitu watufikishe huko (?).

**Com. Lethome:** Umalize (?)

**Mr. Muhamed Madera:** Kidogo saa ni kidogo, saa ni kidogo na ningependa kuongea mambo mingi.

**Com. Lethome:** Kama una maandishi tutachukuwa maandishi.

**Mr. Muhamed Madera:** Lakini, sasa nitapeana nafasi kwa mwengine yangu ya mwisho. Mahali ya kitambulisho. Kusema kweli sisi tuko na ubaguzi, tunabaguliwa zaidi, zaidi, zaidi. Sisi hatupati kitambulisho kwa njia ya kirahisi. Tunapata kwa njia ya shida, kwa njia ya kununuliwa. Na kwa kupitia shida nyingi. Ndiyo tunapata kitambulisho, hasa kwanza...

**Com. Lethome:** Pendekesa (?)

**Mr. Muhamed Madera:** Tungependa vitambulisho tupatiwe kama Wakenya wengine bila kubaguliwa. Na ya pili, vitambulisho ya passport sisi hatupati. Tunetaka tupatiwe passport karibu na wananchi. Badala ya kuenda kutafuta Nairobi, ama sehemu ingine, tuate kama Wakenya wengine, asiangalie nywele nyepesi, atupatie haraka kama sisi Wakenya. Tukona vitambulisho, ili vitambulisho ambaye sisi iko naye haisaidii sisi kupata passport, mpaka tulete barua ya chief, na bara bara zingine nyingi hata hakuna maana. Kwa hivyo tungependa tupatiwe passport kwa njia rahisi kama Wakenya wengine. Kwa hayo machache, asanteni.

**Com. Lethome:** Swali moja tu kabla hujakaa Mohammed, na hizi mnyama wako akikuliwa na simba,unafanya kitu gani?

**Mr. Muhamed Madera:** Wanyama wakiliwa na simba hakuna chochote ninataka

**Com. Lethome:** Unataka nini?

**Mr. Muhamed Madera:** Nataka ridhaa ya hayo wanyama iwekwe kwa (?) ilipwe sababu wanasema wanyama ni wa serikali lakini wacha wanyama, hata inakula binadamu hapa, lakuna kulipwa ridhaa hatupati, sababu kwanza ofisi yenewe kupata kuna watu wengine hawajui mahali wanaenda...

**Com. Lethome:** Sawa hayo tumesikia sasa, mtu akiuliwa na simba alipwe na mnyama akiuliwa na simba alipwe.

**Mr. Muhamed Madera:** Alipwe.

**Com. Lethome:** Unajua ni nmimi nimekusukuma utoe hiyo ulikuwa umesahau. Haya asante sana Mohammed, sasa naona pole pole maoni inaanza kutoka pole pole, mashallah. Haya sasa tuate mama mmoja Asna Ishaac. Mama Asna Ishaac, karibu hapa mama. Ebu kaeni kimya mumusikize mama, watu wote kimya tumsikize mama tafadhalini. Haya.

**Asna Ishaac:** Ahsalaam Aleikhum.

**Com. Lethome:** Mama anza kwa jina yako tafadhali.

**Asna Ishaac:** Asna Ishaac. (in Borana dialect through Translator)

**Translator:** Mama anasema sisi katika Kenya, sisi waislamu tuko na shida.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema tangu baada ya uhuru watu wengi wetu waliuawa.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Mali yao nyingi ilimalizwa, watoto wengi walibaki yatima.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Watoto yatima ambao hawana wazazi waliobaki hawajapata elimu ingawa serikali imechukua hiyo jukumu.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Na wachache wale walipata elimu hawajapata kazi wanakaa ukutani.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Kuanzia wakati tumepata uhuru hadi sasa sisi tuko nyuma sana. Sisi hatuangaliwi na serikali.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Dini yetu ya kiislamu ni dhaifu ambayo haitambuliwi na ina sherehe yake na imetupiliwa mbali kabisa.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anapendekeza watu wao ambao waliuawa wakati wa emergency walipwe ridhaa yao.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anataka alipwe ridhaa.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema yake ni hayo tu machache. Asante.

**Com. Lethome:** Mama ngoja. Umesema kuwa kuna watoto ambao wazazi wao waliuawa wao ni mayatima, sasa unependeka wafanyiwe nini? Umesema kuna watoto wengine wamesoma hawajapata kazi, unataka wafanyiwe nini?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anataka wale watoto wapate elimu,

**Com. Lethome:** Nani atawasomesha?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anapendekeza serikali isomeshe hawa bure.

**Com. Lethome:** Na mambo ya kazi, umesema wanafunzi wanasoma na hakuna kazi ungependa serikali ifanye nini?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anataka serikali ipe hao vijana wote kazi.

**Com. Lethome:** Na hebu muulize mama sasa vile serikali ilivyo sasa, ameridhika ama angependa baadhinya mabadiliko?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anapenda kamwe kila kitu ibadilishwe kabisa.

**Com. Lethome:** Kwa mfano ni kitu gani ibadilishwe sababu serikali unazungumzia habari ya chief, maaskari wa chief, sub-chief, D.O, D.C, P.C, sasa tupatia unataka ibadilishwe wapi?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Yeye anapenda mabadiliko, hali iwe nzuri kuliko vile ilivyo sasa.

**Com. Lethome:** Haya kwa mfano,sasa machief, anataka waendelee kuchaguliwa na serikali ama wachaguliwe na watu wenywewe.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Wachaguliwe.

**Com. Lethome:** Haya, na D.O na D.C

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Kila mtu anataka wote wachaguliwe na raia

**Com. Lethome:** Sasa, kwa mfano angetaka mimi kama Mmasai niwe D.O, hapa kwa waborana?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Hataki wewe anataka mtu amezaliwa hapa.

**Com. Lethome:** Na D.C je angependa atolewe wapi?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema (?) kwa sababu yake mwenyewe hana kazi anakaa nyumbani.

**Com. Lethome:** Sasa hiyo yake amesoma ndio afikie kiwango ya D. C

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema tuko na watoto wa degree ambao wako hapa, hawana kazi.

**Com. Lethome:** Haya sawa mama saa hizi ukitaka kwenda hospitali ukiwa mgojwa utapelekwa wapisaa hizi?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema hana hospitali hapa labda garissa ama Isiolo.

**Com. Lethome:** Angetaka iendelee hivyo hivyo?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Angependa hospitali iletwe karibu na hawa na waletewe maji karibu na hawana kila kitu ambaye (?).

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Angependa serikali iltwe karibu, ofisi iwe karibu wakati ako na shida anaweza kwenda kwa hiyo ofisi. Anapenda soko ya mali iletwe karibu hapa mifugo yao ipate mali.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anapenda county council iweke market ambayo wanawenza kuza vifaa vyao ambayyo wanawenza kuleta kutoka kwao.

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anapenda council wapewe uwezo zaidi.

**Com. Lethome:** Hiyo ndio sawa, inatosha hivyo. Na kuna sheria yoyote anaona inaumiza kina mama?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema sisi upande wa islamu tuko na shida.

**Com. Lethome:** Shida gani?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Anasema watoto wao, wasichana wao hata wakiwa wamesoma hawapati kazi wote wanarudi nyumbani.

**Com. Lethome:** Kwa nini hawapati kazi?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Serikali haipeani kazi, na hata vijana wenyewe wanakosa kazi ya wanaume wasichana watatoa wapi kazi.

**Com. Lethome:** Sasa anapendekeza kitu gani?

**Asna Ishaac:**

**Translator:** Yeye anapenda vijana wanaume na wasichana wote wapatiwe elimu sawa na wapatiwe kazi sawa.

**Com. Lethome:** Basi asante mama asante kwa maoni yako. Shukrani mama Asna. Haya tunapata mama mwingine Gabale Talacha. Hebu kaeni kimya tusikize maoni munasikia kina mama wanajua maoni yale wanatoa wanajua kile kitu wanataka vizuri sana. Haya mama kuja. Vijana hapo nyuma kidogo hamsikizi kina mama ninyi.

**Gabale Talacha:** Salaam aleikhum.

**Response:** Aleikhum salaam.

**Gabale Talacha:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mama anasema anaitwa Gabale Talecha, na ye ye ni kiongozi wa group ya wanawake.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Naye pia ni mwenye kamati katika chama cha KANU.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Mama anasema ako na machache,

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Angependa kuzungumza juu ya Concentration camp.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Wakati wa concentration camp ambaye ni mwaka wa 1965, 1966/7 yeye alikuwa kijana.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema tangu tumewekwa concentration camp, hata wakati tumetolewa concentration camp, sisi bado tuko concentration nyingine.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema wakati wa concentration camp, sisi watu wengi waliuawa, mali yao walinyanganywa, wanawake wanafanywa rape, wasichana wanafanywa rape jambo ambalo waleli, katika sherehe yetu ya dini ya kiislamu, na mila ya Kiborana.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Jambo ambalo mila yetu haikubaliani sisi tunapokonywa kitambaa yetu kwa kichwa kichwa yako inaachwa uchi.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema mabwana zao huwa wanapigwa wakiwa karibu na wao, hawana nguvu kusaidia, mali inachukuliwa, ngombe ambaye ni mnene anachukuliwa yule mzuri anachukuliwa, mbuzi zinachukuliwa vile hawa hawana nguvu wanaangalia tu kwa macho vile mambo inaendelea kuwa baya zaidi.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Hivyo ndivyo mambo ilikuwa wakati wa concentration camp.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Tunawekwa kizuizini na hali tunakaa katika kizuizini ile tunkuja kuteswa, wanawake wanateswa, wanafanywa rape, wasichana wanaharibiwa mpaka hata mila yetu imeharibiwa kutoka wakati huo hadi sasa.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Watu wengi waliuawa katika concentration camp.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** wale waliuawa wengi wao ni wale wenye boma ambaa ni wazazi, wanaangalia mwanamke sura mzuri kuwa mkubwa anakuja kubadilisha kila siku, mwanamke yule mzuri anachukua anaenda kwake nyumbani na bwana yuko hapo anaachwa.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Hiyo ni hapo.

**Com. Lethome:** Anapendekeza kitu gani?

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Mama anasema tunataka tulipwe ridhaa na tulipwe ile mali yetu yote imechukuliwa, kiasi yake tulipwe ridhaa pia hata wale wanawake walifanywa rape walipwe ridhaa hata wale waliuawa walipwe ridhaa kwa sababu katika mila yetu rape iko na ridhaa na ilipwe hata hiyo yote na leo anasema ngombe zile ambazo ziko na Mkenya yote, yote anasema ni yetu imetolewa hapa, turudishiwe hiyo ng'ombe yote hapa hapa

**Com. Lethome:** Hata ile ya Wamasai ni yao pia?

**Translator:** Ile iko na pembe na nyumbo yote ni yao hapana                                  (?) mwingine.

**Com. Lethome:** Endelea endelea.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema aapenda watoto wao wapewe elimu ya bure, na wale wamepata elimu pia wapate kazi ingawa vile unajua vile nimesema mbeleni hapo awali, ya kwamba sisi hatuna mali na tunalisha watoto wetu kwa kuvunja kuni, kulete makaa kwa shinda ndio tunasomesha watoto wetu na baada ya kupata elimu tena hawana kazi ndio tunasema serikali iangalie sisi kuandika watoto wetu kazi.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema kama vile alivyokuwa amesema ya kwamba sisi hata baada ya concentration camp sisi bado tuko katika concentration camp, hiyo inamaanisha ya kwamba anasema baada ya uhuru inasemekana ardhi yote ya Kenya ni mali ya Kenya yote, kwa hivyo movement ya watu inakuwa bila kuzuiliwa watu wanaenda vile wanataka ndio hali anasema wafugaji ambaye ni jirani wалиingia katikati yetu baadaye walikuwa na bunduki waliumiza sisi, sisi tuliuawa bila hata ya msaada wowote kutoka kwa serikali. Kwa hivyo angependekeza kwamba hii ardhi yao iwe mikononi mwao isiwe mikononi wa mtu ye yote.

**Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema kweli sisi wote katika Kenya ni watu ndugu moja hata hivyo anasema ingawa Kenya ni Kenya, movement ya watu iwe restricted ambayo mtu asihame kutoka eneo moja kwa eneo ingine kwenda kulisha mali yake kwani anasema kila mmoja katika Kenya leo ako na nyumba wengine katika huko juu                                  (?) Kenya, kila mtu ako na ardhi

yake, ako na plot yake ambayo iko na cheti lakini ardhi yetu haina cheti. Tunataka yetu tuwe nayo cheti, tunataka ardhi yetu iwe katika miliki yetu sisi wananchi, sisi watu ambao waishi katika hiyo eneo, isiwe anasema sisi ndugu mbili katika Northern Kenya, Msomali na Borana huwa tunapigana kwa kutojua. Anasema hata hivyo wacha tuwe restricted kila mtu akae katika ardhi yake tepewe elimu ya kutosha ili tunaweza kupata msaada kutoka kwa ardhi yetu sisi wenyewe.

### **Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema ni uongo kusema hii miti ni yangu lakini matawi sio yangu anasema hiyo haiwezekani.

### **Gabale Talacha:**

**Translator:** Anasema sisi hatuna haki juu ya ardhi yetu, hatuna cheti ya kumiliki ardhi, hiyo ni moja. Anasema ardhi yetu ianaachwa kwa wanyama, wanyama wanaenda kutambaa na wao hawana ile resource ambayo inapatikana katika nchi yetu lakini resource ni ya serikali. Tunataka resource iwe ni yetu kama ardhin ni yetu tunasema ile kitu inatoka katika ardhi yote iwe ni yetu, kama ni miti, kama ni madini, kama ni wanyama ambao ni wa pori, yote iwe ni yetu isiwe mali ya serikali.

### **Gabale Talacha:**

**Translator:** Mama anasema sisi hatuna haki ya kumiliki ile resource iko katika nchi yetu, anasema sisi hatujui kuishi juu ya famine relief, sisi tulikuwa tunaishi na mali. Sisi tulikuwa tunaishi na zile matunda za misituni ambazo ni kama mandera, ndeka tulikuwa tunakula hata kama tuna njaa, naasema kuna kabilia ile inajulikana kwa kuishi juu wanyama wa porini. Wanyama wa porini wamekuwa ni wa serikali, hawa watu wameumizwa, wamekaa bila haki, wamenyang'anya mali yao, mali yao ilikuwa ni wanyama wa porini, kabilia ambayo inaitwa Wata katika Borana, iko kabilia inaitwa Wata ambayo walikuwa wakiishi wakipata njaa wanakimbia wanauwa siku moja mnyama wao wanakula. Hawa wamekatazwa kwa sababu wanyama wamekuwa ni wa serikali lakini serikali haija-substitute, haijapatia hawa chakula, hii famine relief tunapatiwa sio chakula yetu tunataka tuachiwe ardhi yetu na mali yetu tunajua vile tunaishi.

**Com. Lethome:** Asante sana mama nenda ukajiandikishe pale. Gubale Haji Jalpesa. Halafu kuna mama mzee alikuwa anapita pita hapa anataka kuzungumza jitayarlishe pia aje azungumze. Yule ana nguo ya blue mama. Haya.

**Kabale Haji:** Salaam aleikhum.

**Response:** Aleikhum salaam.

**Kabale Haji:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mama amesema ye ye anaitwa Kabale Gubala Hajalpesa ambaye ametoka katika kikundi ya wanawake, na angependa kupeana maoni yake kidogo.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anataka kuanzia na pande ya wanawake.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema katika Kenya leo inasemekana wanawake wako kisawa na wanaume na ni uongo kwamba hatuoni kitu imetufanya sisi sawa.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema hata wale wanawake wamesoma hawapati kazi ya D.O, hawapati kazi ya D.C, P.C, ama hata kwenda kwa Minister kuajiliwa kazi kama hiyo wanawake hawapati sawa na wanaume.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema tena pia katika local leaders hatupati kama kuajiliwa kama chief, na kuwa councillors anasema imekuwa vigumu.

**Com. Lethome:** Angependekeza kitu gani?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema wanawake wamefinywa sana hata hawapati nafasi ya kugombea kiti cha siasa kwa sababu ya kuogopa wanaume.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema wanawake katika eneo hii hawatambuliwi, hawajapewa nafasi mzuri, hawajapata elimu na kama hawa wamefanya juhudhi ya kujipatia kazi kama kuunda women groups hawapati msaada kwa serikali na kutoka kwa jamii yoyote, kwa hivyo angependekeza sisi tupate misaada kwa sababu sisi ndio misingi ya familia, kwa sababu sisi ndio tunalea watoto sisi ndio tunachukua jukumu ya nyumbani ingawa hivyo sisi misaada ile tunapata kwa serikali ni kidogo kushinda ile kazi tunafanya nyumbani.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Mama anasema hata katika wilaya ya Isiolo vikundi ya wanawake na vikundi ya wanaume hawapati haki sawa, msaada nyingi inaenda kwa kikundi ya wanaume na vikundi ya wanawake wanafinywa hata hawapati msaada sawa kutoka kwa serikali sawa na ile kikundi ya wanaume.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Leo wanaume wako sawa na wanawake, kwa hivyo wanawake wasipigwe, sisi tunapigwa bado, tunapigwa kama punda. Polisi anasema anapiga vijana wetu watu wetu. Mtu akishikwa kabla ya kupelekwa kotini anapigwa. Mtu anafaa kupelekwa kotini apigwe, sisi tunaonekana kama tuko bado ukoloni kabisa. Kwa hivyo anasema ardhi yetu tuwe tunamiliki sisi wenyewe ikisemekana kwamba ardhi ni yetu, ardhi yetu isiwe trust land. Ardhi yetu iwe community land, ardhi yetu iwe sisi ndio tunamiliki sisi wenyewe tujue vile tunaweza kufanya naye. Iko na resource ya kutosha juu ya ardhi yetu, tuna miti, tuna madini, tuna kila kitu ambayo tungependa kuhifadhi sisi wenyewe na tuwe tunamiliki sisi sio serikali.

**Com. Lethome:** Ngoja nimulize maswali halafu tuendele. Swali la kwanza ni kuhusu uongozi, amesema kina mama hawapewi nafasin ya uongozi, ile nimefahamu ni kwamba ni kwamba hakuna mmama councillor ama MPs, mjumbe, ama chief, sasa unependeka ya kuhifadhi sisi wenyewe na tuwe tunamiliki sisi sio serikali?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Angependa hata wanawake wapate nafasi sawa na wanaume.

**Com. Lethome:** Kwa hivi sasa kuna mtu anawazuia kusimama kupigania kitii?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Hawapati kazi wanawake (?) Anapendekeza ya kwamba mifugo yao ambayo imemalizwa wakati wa concentration camp walipwe ridhaa pamoja na watu na yale yote imetokea tangu wakati ule walipwe ridhaa.

**Com. Lethome:** Kabla hujaendelea sana maswali hujajibu. Unependaka kuwe na kama vile viti vyaa nominated councillors vipewe kina mama ama namna gani na MPs ile nominated seats tipe kina mama ama namna gani?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema hawapati nominated kwa hivyo angependa wapatiwe nominated kwa sababu hawapati nafasi kwa sababu wamefinywa na wanaume zaidi.

**Com. Lethome:** Haya sasa turudi habari ya kufinywa na wanaume, umesema hapa wanaume wanawapiga, angependeka tukiunda sheria mpya mwanimume akikupiga afanyiwe nini?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Mama anasema tumependekeza katika washaa nyingi kwamba wanawake wasipigwe, na kama watapigwa, wanataka wanaume pia waadhibiwe katika kotini.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo mzee akipiga mama apelekwe kotini ashitakiwe, ndio hivyo mama?

**Kabale Haji:** Eeh.

**Com. Lethome:** Na wewe ukipiga mzee kwa sababu kuna wa mama wengine wanapiga wazee?

**Kabale Haji:** Hata mimi nipelekwe kotini, kila mtu.

**Com. Lethome:** Sawa eeh, sheria inataka iangalie pande yote sio pande moja peke yake. Umesema habari ya polisi wanasumbua vijana, wanapiga piga vijana. Sasa unataka polisi akimsumbu kijana bila makosa yoyote, akiwa na makosa achukuliwe hatua, lakini hana makosa, huyu polisi unatakiwa umuchukulie hatua gani ama angeshitakiwa kwa nani, sema?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Mama anasema, vile imesemekana kwamba sheria haikubalii watu kupigwa wapelekwe kotini vijana na kama polisi wanapiga watoto ama vijana waadhibiwe pia wao pia wapelekwe kotini.

**Com. Lethome:** Haya sawa, sasa polisi leo wakikusumbua ama akikukosea unaenda kumshtaki kwa nani (??).

**Kabale Haji:**

**Translator:** Yeye hana mtu wa kushtaki.

**Com. Lethome:** Sasa angependa tuwe na mahali ambapo unaweza kwenda kushtaki.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Ndio angependa pahali pa kushtaki polisi iwe karibu na wao.

**Com. Lethome:** Okey sio ofisi ya polisi mkubwa zaidi?

**Kabale Haji:**

**Translator:** Angependa yule mtu amechaguliwa na raia wa kusimamia polisi na wao, polisi akikosea hao, waende wamshitaki kwa huyo mtu na huyo awaadhibishe hao awapeleke kotini.

**Com. Lethome:** Sasa endelea umalize malize.

**Kabale Haji:**

**Translator:** Anasema angependa kusema juu ya poverty, na umaskini anasema zaidi tumeletewa na ukosefu wa ardhi, ukosefu

wa kumiliki ardhi yetu, ukosefu wa kukosa kuwa mwenye ardhi yetu kuwa na mwenyewe. Sisi hatuna uwezo wa kuzuia mtu yeyote kukaa kwenye ardhi yetu na serikali yetu tukufu iko, sisi hatulindwi. Sisi sikuliki yetu iko katika hali baya, yule ako na nguvu anakuja kumaliza wewe na serikali iko na jeshi, serikali iko na polisi, serikali iko na kifaru ya kwamba angezua watu usalama wao na mali yao yote wapate salama yani hiyo angependa serikali izingatie usalama wa watu wetu ili hii umasikini iondokee sisi.

**Com. Lethome:** Haya maliza mama.

**Kabale Hajji:**

**Translator:** Mama anasema angependa Kadhi ambaye anachaguliwa na wananchi, sisi wenyewe tuchague kadhi yetu. Ya pili angependa Islamic Bank pahali ambapo tutapewa mkopo bila ridhaa inatakiwa na dini yetu ya Kiislamu.

**Kabale Hajji:**

**Translator:** Ya mwisho kabisa mama anasema sisi tungependa customary law yetu ipewe nguvu ili sisi tunaweza kujilinda, na jambo ambalo linaweza kutokea huko ndani tunaweza kujangalia na kujiletea mali halafu serikali ipatie sisi, yani central government ikuje karibu na sisi, yani anapenda jimbo.

**Kabale Hajji:**

**Translator:** Anasema angependa kuuliza pande ya wale wasiojiweza waangaliwe sawa na wale wanaojiweza, yani wapatiwe msaada kushinda wengine kwa sababu wao hawajiwezi. Pia hata wanawake waangaliwe kwa upande wa serikali wapewe msaada zaidi ya wanaume kwa sababu hawa pia ni wale amba ni weaker sex.

**Com. Lethome:** Asante sana, sasa tatarudi tena kwa list yetu halafu baadaye tutaita kina mama wengine. Ibrahim Kanata. Sasa kidogo tufanye haraka haraka zaidi, muda unaenda watu ni wengi.

**Mr. Ibrahim Kanata:** Mimi kwa jina ninaitwa Ibrahim Kanata kutoka Modagashe location, Sirichwa Division. Basi mimi mapendekezo yangu ni haya; kwanza, structure of the government. Ningelipenda kwa maoni yangu Raisi, kwanza tuwe na serikali ya majimbo na tukiwa na serikali ya majimbo, ile Ceremonial President, asiwe na chama akuwe bila chama, halafu kuwe na Prime Minister na kadhalika na kuendelee namna hiyo. Na president pia asikuwe na constituency, asikuwe mwakilishi sehemu ya Mbunge kwa sababu akiwa namna hiyo atakuwa na mapendeleo na mambo nyingi hata saa hizi zimetokea kwa sababu ya shinda kama hiyo. Nikiwa ninasema mambo ya majimbo tunasema hivyo kwa sababu ya shinda zilizotupata hapo mbeleni kwa sababu tumewekwa kwa kijiji na kama tumewekwa kwa kijiji tumepata shinda nyingi na saa hii tukiwa tunesema majimbo hatutaki kuwa katika sehemu ya mkoa wa mashariki. Mapendekezo yangu ni kuwa tuwe katika District tatu, Marsabit, Isiolo na Moyale. Pengine kama haitoshi Tana River na Samburu District, sisi ni pastoralist community tunaweza kuishi pamoja hatuna kahawa, hatuna majani kwa hivyo tunaweza kuishi pamoja na tunaweza kusikizana na hali yetu ya

kimaisha infanana kwa sababu tuko na mifugo na lazima wakati huo tumeshikana namna hiyo tuwe katika jimbo moja sisi tunawenza kujitafutia soko ya mifugo yetu kwa sababu saa hizi soko zinatafutwa sana unasikia ni ya majani na kahawa kwa sababu ile serikali iko hapo inategemea ile resource wako nayo ile product, wako na product land, fertile land sasa hakuna mtu anajali mambo ya mifugo, lakini sisi tukiwa katika jimbo moja tunawenza kutetea wanyama wetu tupate soko, tupate factory, hata unaona zamani Kenya Meat Commission zamani imejengwa Thika hiyo ilikuwa ni kutafutia watu wa huko kazi. Lakini kama ingeangaliwa ukweli kabisa hiyo KMC ingekuwa Isiolo ama wajir ama Marsabit kwa sababu ng'ombe zinatoka huko. Nasema hivyo tuwe na majimbo kwa sababu hiyo.

Pia nataka kuongea juu ya freedom of movement. Freedom of movement ya human beings iwepo lakini katika sheria iwekwe ya kwamba isikuwe na freedom of movement ya pastoralist community. Watu wasihame na mifugo kwenda huku na huku kwa sababu ndio inatatiza mambo ya usalama katikasehemu zetu ambazo sisi wafugaji tunaishi. Pia sisi kama wa jamii ya kuhama hama, ile serikali itakuwapo, ile serikali itakuja, ama ile iko saa hii tunatoa maoni yetu tunasema kitu ya kwanza tunataka usalama wetu uangaliwe kwa sababu sisi ni watu wa kuhama hama iwekwe kwa sheria ya kwamba hata ile bunduki watu wako nayo ya kujichunga, iwekwe kwa sheria kwamba ihalalishwe ikuwe kama ya homeguard kwa sababu sisi huwa tunahama, leo tuko hapa kesho unasikia Kokom, kutoka Kom, tunaenda Yamicha, unaenda wapi, kwa hivyo sasa polisi hawezi hama na wewe, MP hawezi hama na wewe, serikali haiwezi angalia vile mali iko, wakati wote machinery ya serikali, security haiwezi kuwa na wewe, lakini kama uko na bunduki na imekuwa registered, na imeonekana kwamba watu wako nayo lakini ihalalishwe ya kwamba iwe kama bunduki ya home guard na ichunge watu katika sehemu wako.

Tena mambo ya Trust Land. Tungependa sheria iondoe hiyo jina. Mambo ya Trust Land vile maoni imetolewa iwe community land, na tuwe tuna own sisi wenyewe na ile resource iko juu ama chini ya ardhi iwe ya community. Ikiwa sasa unakata miti unaambiwa ooh umekata miti, Forestry Department inakushtaki na miti iko hapa kwa plot yako. Kama ni madini imetokea hapo unaambiwa ni ya serikali. Kwa hivyo hiyo tunaona ni dhulma iwekwe kwa sheria ya kwamba ile ardhi na resource ile iko juu na chini ya ardhi yote ni ya community iwe ya jamii ambao wanaishi (?) iwekwe kwa sheria tunataka namna hiyo pia.

**Com. Lethome:** Haya maliza.

**Mr. Ibrahim Kanata:** Tena mambo ya Idemnity Act. Hiyo kwanza iondolewe kabisa kwa sababu sisi vile tumeteswa na vile tumeangamizwa kwenye concentration camp tunataka tulipwe vile wazee wametoa maoni yao hapo mbeleni tunataka tulipwe kwa sababu ya mambo mengi yametendeka hapo mbeleni tunataka tulipwe kwa sababu ya mambo mingi sana yametendeka, mifugo zikasafirishwa kwa magari ya jeshi, nini na nini zimefanyika ndion sababu tunataka tulipwe pia. Mambo kuhusu kuwekwa kwa hiyon kijiji tukisema tulipwe kama hatuwezi kulipwa direct, kama itakuwepo na serikali ya majimbo tunataka hiyo ridhaa tujengewe university, tujengewe hospitali everywhere, at least every division headquarters kama hiyo kulipwa (?) na ikuwepo na free education from primary level to university level tukiwa tunesema na majimbo katika

jijini mwetu tunataka namna hiyo. Pia tunataka afya na elimu namna hiyo na tupate bara bara nzuri kama Wakenya wengine katika jimbo yetu saa hiyo, tupate sitima everywhere ndio tuweze kujifanyia biashara nyingi ambazo zinataka sitima. Tunataka tuwe na university pia katika jimbo yetu, hata every location ikuwe na university, ikuwe na colleges nyingi ili watu wapate masomo, watu wapate kazi kupata kazi lazima uende mpaka university level au uende college u-qualify halafu unapata kazin ya daktari ama nini na nini na kadhalika.

**Com. Lethome:** Maliza ndugu yangu.

**Mr. Ibrahim Kanata:** Nikimalizia namalizia mambo ya uchaguzi wa bunge. Mimi kwa pendekezo yangu, kuchaguliwa kwa Member of Parliament, MP achaguliwe akuwe 2 seasons ya miaka tano tano na baada ya hiyo huyo mtu asigombee hiyo kiti. Yangu ya mwisho Mbunge awe akichaguliwa na kama hajafika constituency for three months, for continous three months hajatembelea sehemu yake ya uwakilishi bungeni, ikuwepo na sheria ya kuweza ku.. I think two third ya constituency population inaweza kumwondoa iwe na re-election tena. Kwa upande wa bunge pia ninasema namna hiyo.

Upande wa local authority pia, local authority iwe independent isikuwe chini ya ministry yoyote, ikuwako na ipatiwe nguvu na ipatiwe fund na iwe na system yake mwenyewe ya kujitawala ikuwako na mayor, deputy wake namna hiyo na itakuwa ikisimamia wilaya kama ni main chairman ama clerk asimamie wilaya kama D.C vile ilikuwako zamani kwa sababu tunaona hiyo ndiyo inatusaidia. Wakati wa ukoloni wazee wetu7 wanatwambia kwamba kila kitu katika wilaya ya Isiolo ilikuwa chini ya council na council ndio ilikuwa ikiendesha na katika hiyo council, councillor lazima awe mtu wa O' level awe mtu ako na masomo ya o' levels na chairman na clerk awe ni graduate, clerk akuwe graduate, mtu ambaye amesoma na ako na masomo ya hali ya juu huyo ndiye anaweza kuendesha na kujua mahali vile iko na anaweza kuwasiliana na watu vizuri. Maoni yangu eeh....

**Com. Lethome:** Ibrahim inatosha

**Mr. Ibrahim Kanata:** Okey asante.

**Com. Lethome:** mengine unaweza kutuandikia upeane. Asante tunaendelea. Abdillahi Diba. Tafadhalini sasa nikikuambia umalize, umalize, pendekeza haraka haraka, watu ni wengi sana naona watu wengine wameanza kufika. Abdillahi Diba.

**Mr. Abdillahi Diba:** Asante sana Bwana Commissioner, kwa jina mimi naitwa Abdillahi Diba, nikitoa maoni, haswa nataka kuanzia mambo ya mipaka. Sisi kama wafugaji wa mifugo tuko na shinda sana, kama wafugaji wa mifugo tuko nq shida ya mipaka. Na hii mipaka tangu ukoloni,

**Com. Lethome:** Pendekeza, pendekeza.

**Mr. Abdillahi Diba:** Nitapendekeza, tangu wakati wa ukoloni mipaka imewekwa lakini kwa ajili ya mambo ya utawala kila wakati mpaka huwa unababilishwa, na huwa unaleta shinda. Nikipendekeza, nataka mpaka wa kila mmoja yani kutoka wilaya mpaka iheshimike. Hiyo ni kusema kila mmoja ajue sehemu yake ya utawala, kama ni kutawala yani sehemu za Isiolo, iwe na mpaka yake ya rasmi. Nikisema hivyo wakati mwingi imetokea vita ya kikabila, hii vita yote imeletwa na mambo ya mipaka. Mtu akikunyang'anya ardhi yako lazima utetee hiyo ardhi, ukiona sasa sehemu zote za ufugaji kulikuwa na tofauti za kikabila na watu ambao wanapigana na wanapigana kikabila vita hiyo yote imeletwa na serikali, vile imeletwa, serikali imechukua haki ama amani ya kulinda mali ya mwananchi na maisha yake. Wakati hii maneno ya mipaka ilikuwa imetokezea, serikali imeacha watu hivi mpaka watu wamemalizana mifugo ikaisha na mpaka saa hii hata watu wamezimiliki silaha ya haramu na hata serikali haishugulikii na watu huwa wanauana. Mpaka saa hii sehemu zetu za jirani hapa Garissa sisi kila wakati huwa tunazozana juu ya mpaka, mpaka huu wote mtu tu akiingia serikali anajibadilishia mpaka wake..

**Com. Lethome:** Unajua kwamba unarudia sasa pointi ambayo umefanya already? Enda kwenye pointi ingine ndugu yangu.

**Mr. Abdillahi Diba:** Kwa hivyo nikitoa resolution nataka hiyo mpaka ya kila wilaya iheshimike. Kidogo nikirudi mambo ya majimbo kweli tunataka majimbo. Tukitaka majimbo sisi hatuna nguvu, resource yetu haina value yoyote, kwa hivyo majimbo tukitaka tunataka serikali iangalie yani resources yetu iwe na value, na ikiwa sisi hatuna nguvu, mpaka saa hii tunaendelea kulishwa na mahindi ambayo imetolea kwa msaada. Kwa muda wa miaka ishirini iiao, tunataka hiyo majimbo tusaidiwe na kila msaada wote, ikiwa ni kujengewa shule, shule iwe ni ya kutoka primary mpaka university iwe free education. Na pia hatuna usaidizi ingine ya ki-resource kwa hivyo tukiwa tunataka majimbo, tunataka zaidi yani Marsabit, Moyale, wajir na Isiolo iwe moja lakini kwa wakati huu resource ile ambayo tuko nayo haina value yoyote, tunataka serikali nitukubalie sisi majimbo tuwe na usaidizi wa serikali kwa muda wa miaka ishirini.

Wakati wa emergency, wengi wamegusia hiyo mambo ya emergency, kweli sisi wakati wa emergency tumewekwa kwa kijiji, hiyo kijiji imeumiza sisi, mpaka saa hii kila mmoja yuko hapa hiyo mambo ya kijiji ime-affect hawa. Tukilipwa ridhaa, sisemi ridhaa ilipwe kwa kila mmoja, lakini ridhaa iwe ikilipwa kwa kupatiwa elimu ya bure kutoka primary mpaka university level. Na barabara pia tujengewe. Mpaka saa hii barabara yetu kutoka Isiolo sehemu hii ya wafugaji yote haina barabara na maendeleo yoyote inaanza kutoka barabara, maji na manbo ya hospitali hiyo yote hatuna sababu hiyo yote serikali haituangalii sisi. Kwa hivyo ikisemekana ni ridhaa, hiyo ridhaa ikilipwa sio ilipwe mtu binafsi ilipwe kwa kujenga mabarabara katika sehemu za Northern Kenya yote (?) mzima. Elimu iwe bure.

Mambo ya I.D card. Kweli sisi tunapata I.D kwa mambo ya taabu. Ingala tunaenda safari ndefu mpaka Isiolo kuipata tunataka hiyo I.D kwanza iwe scrapped ibadilishwe tuwe na passport, passport waislamu hawapati. Leo nikisema naenda kutafuta passport mimi kama muislamu ambaye mwenye nywele nyepesi, nachukua hata miaka tatu kutafuta passport. Kwa hivyo hii mambo ya kipande ibadilishwe kila Mkenya awe na passport na hata akiwa anataka kwenda nje awe na hiyo passport badala ya I.D. hapasi kuwa na I.D, I.D kwanza imeleta shinda sana katika Kenya. Kwa hivyo tunataka kuwa na passport

Kenya nzima. Kwa hayo machache nasema asante.

**Com. Lethome:** Haya asante sana Bwana Abdillahi Diba. Wakati huu ningependa kumkaribisha Commissioner ambaye niliwambia ako kwa njia anakuja naye ni Commissioner mwenzangu Dr. Githu Muigai, amekuja ningependa tu awaamkue kisha tuendelee.

**Com. Githu Muigai:** Habari zenu wananchi? Mimi nafurahia kuwa hapa kwenu. Asanteni.

**Com. Lethome:** Haya kwa hivyo tunaendelea, ningependa kurudi kwa akina mama tena lakini kabla ya hapo kuna mtu mmoja ambaye ni katika wale tunaita watu with disability, ambao kidogo ni walemvu, tungependa kumpa nafasi hii pia azungumze Sheikh Abdi Ali. Na kama kuna mtu mwingine huko ambaye mnajua tungependa pia tumpe nafasi, Katiba ni ya Wakenya wote. Unapenda...

**Sheikh Abdi Ali:** Mimi hapana (?)

**Com. Lethome:** Haya Senior Chief yuko hapa? Haya Ibrahim anaweza kufanya hiyo kazi pia. Mandera.

**Sheikh Abdi:** Salaam aleikhum, Wabarakati. (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Sheikh anasema baada ya salamu, maneno yangu ni mafupi. Anasema majina yangu ninaitwa Maalim Abdi Ali.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema maana ya kuitwa Maalim ni mtu anatimiza usalama lakini jina yangu yenyewe ninaitwa Ale Abdi aAli.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema ile kitu nitaongea juu yake,

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** anasema wale wako hapa wengi ni Waborana.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema Borana katika Kenya wako na district tatu kutoka Moyale, Marsabit, Isiolo.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema kuna district inaitwa Marsabit, Moyale, Isiolo.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema waborana wenyewe ni kabilia nne

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema kabilia nne wanaitwa Borana.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema ile ya kwanza inaitwa Bora ngutu. Anasema ya pili nayo inaitwa Sakuye.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema ile ya tatu nayo inaitwa Gabra. Anasema ya nne nayo inaitwa Wata.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema hawa watu wote nne wanaitwa Borana.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Kutoka Kenya ilipata uhuru, anasema kutoka Mungu alileta watu duniani anasema walizaliwa pamoja.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema hakuna tofauti yote kati yetu, anasema sisi hatuna tofauti ndani ya Kenya.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema kati ya wale watu wanne ametaja hapa, kuna mtu mmoja amekosa haki ndani ya Kenya hii kabisa amebaki nje.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema hao watu jina yao wanaitwa Wata.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema iko kati ya wale watu Waborana wanne iko kati yao ndani anasema.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema Kenya iko na kabilia arobaini na mbili, anasema hawa watu wanaitwa Wata, jina yao haiko kwa hayo makabila, wamebaki nje.

**Com. Lethome:** Sasa anapendekeza nini? Wajua tulipoanza, asubuhi tulisikizana tukianza historia hatutaweza kumaliza, Kenya yao hakuna wafanye nini?

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema hao watu walikuwa wamekosa haki lakini sasa anataka hao watu wapate haki yao na wawe na jina yao kama wale Wakenya wengine.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema asilia wa Kenya iwe kabilia arobaini na tatu.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema ile ya pili nitaongeza,

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** anasema hawa watu wale walikuwa wawindaji hawana mali ile kitu walikuwa wanategemea ni wanyama wa pori.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** halafu serikali inasema wale wanawinda hao wanyama ni waharamu.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema ukipatikana umegusa hao wanyama unashtakiwa.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema sasa wamekosa ile mali yao walikuwa wanategea.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** wamekosa ile namba ambao makabila arobaini na mbili wengine wamepata.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema angependa hao watu wapate haki yao ile walikuwa wamekosa.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Sasa anasema hawa watu walikuwa wanategemea wanyama na wanyama inasemekana wamekuwa wa serikali na anasema kwa sababu wamekuwa wa serikali hao wanyama wanaleta pesa, wanaleta income, anasema anataka hiyo income,

asilimia ipatiwe hao watu wafunze watoto wao, wapate income ndani ya hiyo income inaletwa na wanyama.

**Sheikh Abdi:**

**Translator:** Anasema hiyo mimi namalizia hapa.

**Com. Lethome:** Haya asante sana mzee karibu. Haya yule mama wa nguo ya blue. Mama, mama Kabale kuja. Aseme jina lake kwa sababu sijapata jina lake mpaka sasa. Sema jina mama.

**Mama Kabale wako:** (in Borana dialect, through translator)

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Mama anasema anaitwa Kabale Wako Kaki.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Anasema vile unaniona mimi karibu mwaka umekwisha.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Lakini leo ye ye anazungumza juu ya watoto, wajukuu wake. Sisi tumezaliwa huku, hata wakati wa ukoloni tulikuwa huku.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Wakati wa ukoloni sisi tulikuwa na ada yetu.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Mkoloni amehama,

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** mjumbe wetu wa nkwanza hapa ni Bonaya

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** ye ye ndiye alikuwa mwanzilishi katika chama ya KANU.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Tangu bonaya amepoteza hiyo kitu yake sisi tunachagua kila baada ya miaka tano tunachagua mjumbe.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Anasema mtu akiwa bunge kuna marshati ako nayo.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Anasema wakati tulikuwa na concentration camp ambapo watu wengi waliuawa mifugo yao nyingi ilichukuliwa na tungependa tupewe ridhaa kwa hiyo mali yote imekwishamaliza pamoja na hao watu ambaa wamemalizwa.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Mtu akikosa mali anabaki na ardhi.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Ardhi inakuwa na mimea na inaletea wewe chakula.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Lakini anasema sisi tumekosa ardhi hiyo.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Mtu akikosa ardhi ataenda wapi?

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Sisi tumekosa ardhi yetu.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Wakati wa mkoloni, tulikuwa na mipaka ambayo inaheshimika sana.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Jirani hawavuki kwa jirani mwagine, bila idhini ya wazee na serikali. Watu walikuwa wanawekwa bali bali kilaa mmoja anakaa wilaya yake. Leo tunasemekana Kenya imepata uhuru watu wote ni ndugu na tumeletwa pamoja sisi wote. Na jirani wetu ambaa tunaishi na wao sasa wamevamia ardhi yetu na tunaumia. Tunataka kila mmoja akae kwake. Tunataka kumiliki ardhi yetu. Sisi tunachagua wanasiasa lakini hatupati yale ambayo tunahitaji kwa serikali yetu ingawa tunasemekana sisi ni Wanakenya, sisi hatuna hospitali, hatuna shule nzuri, hatuna barabara, sasa anapendekeza, barabara nzuri iwekewe sisi, shule watoto wetu wapate elimu ya bure, tuletewe hospitali karibu na sisi.

**Mama Kabale wako:**

**Translator:** Watoto ambaa mama zao ama wazazi wao waliwaelimisha kutokana na ile kuni wanavunja, makaa, wamekosa kazi baada hata ya kumaliza shule na wanaishi huko. Misaada ambayo tunapata kutoka kwa serikali ni yellow maize na hiyo

siyo chakula yetu sisi. Asili yetu tunakula nyama, tunakunywa maziwa, wakati tunpewa msaada, hii msaada tunapewa yellow maize. Tunataka tupewe chakula nzuri wakati tunapewa msaada na serikali.

**Kabale Wako:**

**Translator:** Sisi zamani ni watu ambao wakati wa kale hata wamama wakijifungua ama vijana huwa walikuwa wanakula damu ya ng'ombe, wanakulanga nyama ya ng'ombe, wanakulanga samli, maziwa ya ititu na leo wanasema hiyo mali yote hapana iko kwa sababu ya ukosefu wa ardhi.

**Com. Lethome:** Ungependekeza nini?

**Kabale Wako:**

**Translator:** Tunataka tumiliki ardhi yetu na sisi tuwe na mamlaka ya kupeana ardhi kwa yule mttu tunataka na sisi tunataka kuishi peke yetu.

**Kabale Wako:**

**Translator:** Amemalizia hapa.

**Com. Lethome:** Haya asante sana mama. Haya tupate huyu mama mwengine ambaye anaitwa Fatuma Ali. Fatuma Ali?

**Fatuma Abdi:** Salaam aleikhum.

**Response:** Aleikhum salaam.

**Fatuma Abdi:** Mimi naitwa Fatuma Abdi.

**Com. Lethome:** Sio Ali?

**Fatuma Abdi:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mama anaitwa Fatuma Ali Abdi.

**Translator:** Anasema angependa kuzungumza juu ya elimu.

**Translator:** Tumesikia baada ya ukoloni wakati serikali yetu ilipata mamlaka serikali ilituahidi elimu ya bure.

**Translator:** Lakini baadaye tunaona hakuna hiyo elimu ya bure watoto wetu hawapati elimu na sisi tunakaa maskini nyuma.

**Translator:** Elimu ile ambayo tunawekewa hapa ni ya primary, na hiyo hata haina quality nzuri.

**Translator:** Napendekeza watoto wetu wapate elimu ya bure kutoka nursery mpaka ahitim University amalizie, serikali ipatie sisi elimu ya bure kabisa.

**Translator:** Haya inaweza tufanya sisi tusahau nyakati za ukoloni ambayo tulifinywa na concentration camp ambayo watu wengi wetu walieuawa.

**Translator:** Pia anataka kuzungumza mambo ya hospitali.

**Translator:** Baada ya uhuru serikali imesema tutapata dawa ya bure.

**Translator:** Wacha dawa ya bure hata aspirin huwezi pata bilakulipa shilingi kwa hospitali. Sasa yule maskini kabisa, watu wanaumia nyumbani hata akiwa mgojwa hawaendi hospitali kwa sababu wanajua hawana pesa ya matibabu.

**Translator:** Sisi nchi yetu sisi ni maskini, maskini ya elimu, maskini ya mali ndio unaona sisi tumekuwa wachache sana katika hii eneo.

**Translator:** Sisi tunataka tuletewe hospitali karibu na hospitali mzuri ambayo tunaweza kutibiwa badala ya kwenda Isiolo ama Garissa kutoka hapa.

**Translator:** Anapenda kugusa pande ya usalama tena.

**Translator:** Anasema baada ya uhuru usalama wetu umekuwa katika hali ya hatari ya kwamba sisi tunakaa sawasawa hatuna serikali, watu wanaumizana yule ako na nguvu ananyang'anywa mwininge bila kuangaliwa wanaumizana.

**Translator:** Sisi tumekosa mali, hatuna elimu, tume wanhwa kama wanyama wa porini, na tunaumia.

**Translator:** Tungependa serikali yetu ilinde usalama wetu na mali yetu kikamilifu vile imesekana katika sheria.

**Translator:** Pia anapendekeza watoto baada ya kupata elimu wasirudi kwa ukuta na kula miraa peke yake bali serikali ipe hawa kazi ya kulipa wazazi hawa ambao walikuwa wamesomesha hawa.

**Translator:** Tukishinda kujitambua kama sisi ni wanyama ama sisi ni binadamu.

**Translator:** Anasema katika pahali binadamu anaishi, kuna barabara mzuri ambayo mtu hata akitaka kutoka hapo kwenda London anaenda katika siku moja.

**Translator:** Wacha wakati wa mvua sisi hata hatupashani habari habari kwa mwingine, lakini hata wakati wa kiangazi very poor road network anasema.

**Com. Lethome:** Apendekeze sasa.

**Translator:** (to Borana)

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Tungependa tupewe barabara yetu inaitwa rami, kutoka Nairobi hadi kwenda Mandera, iende Merti, iende Sericho, iende Samburu, rami, rami.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Wengine hata kwenda choo wanawekewa rami, kwenda hata choo.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** hata ukosefu wa barabara umetuumiza sana.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Angependa kugusa pande ya dini ya Kiislamu.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Anasema benki ya serikali yetu ya Kenya leo hailingani na vile dini yetu inataka kwa sababu inapeana mkopo ya ribaa,

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** na dini ya Islamu haikubali ribaa.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Angependekeza aletewe banki ya Kiislamu ambaye inapea hawa mikopo bila ribaa.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Yeye hapendi Kadhi ambaye anachaguliwa na serikali, hatutaki. Tunataka yule Kadhi ambaye sisi wenyewe tunachagua na anatuwakilisha katika korti ya serikali.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Katika shule tungependa wasichana wetu wapewe nafasi ya kuva mavazi ambayo ina aambatana na dini yetu ya Kiislamu ambayo ni nguo ndefu ambayo mwili yao haioneckana ila nyuso.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Ingawa tumelazimishwa na hali ya maisha vile watoto wetu wanasoma sisi tuko na dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu vile wanasoma katika hali ile wanasoma, wasichana wapewe nafasi mzuri ya Kiislamu.

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** Anapenda watoto wao waandikwe kazi na serikali na wapewe barabara ya kutosha,

**Fatuma Abdi:**

**Translator:** na usalama urekebishwe haraka, hali ni mbaya sana mama anasema.

**Fatuma Abdi:** Basi natoka hapa.

**Com. Lethome:** Asante sana mama. Haya tumpate sasa Kaltuma Mursale.

**Kaltuma Mursale:** Salaam aleikhum. Jina yangu naitwa Kaltuma Mursale Ibrahim.

(in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mama anasema atazungumza machache.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Angependa serikali ya jimbo, anapendekeza serikali ya jimbo.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Anasema baba yake alikuwa na ngamia karibu elfu moja, mbeleni yeye mwenyewe alipokuwa mtoto alikuwa mfugaji wa ngamia, leo hii hawana hata ngamia moja na yeye ni maskini hana hata kitu chochote, zilimalizwa wakati wa concentration camp.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Nataka serikali ilitulipe ridhaa ya mali yetu.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Anapendekeza either hiyo ngamia ilipwe kila moja dhamana yake au kama serikali inafikiria inaweza kubadilisha na hali ingine ya kujengea shule mzuri, hospitali, labda barabara mzuri iwe inaweza kulipwa yote amekubaliana na vile walikuwa wamezungumza.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Anasema sisemi kwamba serikali ya Kenya sio serikali yake, bali anasema hatoshekin kamwe na yale ambaye serikali inawapea msaada ama vile anawaongoza ya kwamba hatosheki kabisa ya kwamba vile watu wa down Kenya wanapewa wao hawapewi sawa wale watu kutoka Northern Kenya.

**Com. Lethome:** Sasa angependeza angependa serikali ifanye nini sasa ama ilazimishwe... (*interjection*).

**Kaltuma Musale:**

**Translator:** Angependa serikali ippee sisi barabara nzuri, ape sisi elimu, ape sisi hospitali, na pia tuwe sawa na wengine katika Kenya ya kwamba mawasiliano iwe karibu na sisi ya kwamba mtu akiuawa leo, hata watu mia moja hawasikiki lakini mtu mmoja katika Kenya akikufa huwa anatangazwa kwa redio na sisi tuko bali sana na mawasiliano tunakuwa ni afadhali wanyama wa msituni ambao serikali inalinda, sisi hatulindwi. Wanyama wanamaliza sisi, na sisi hatulipwi, tunataka tulipwe ridhaa wakati wanyama wanakula sisi, wakati wanyama wanakula mifugo yetu isiwe ni wanyama iko bora kushinda sisi binadamu.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Mama anasema sisi watu wa Northern hasa Waborana, sisi tumekuwa marginalised. Mfano alichukua ni kwamba Commission hii ambayo iko hapa leo huwezi kuona Mborana yejote ambaye yuko represented hata katika secretariat huwezi kuona Mborana. Kwa nini? Sisi apapa iko sawa na wengine? Sisi hatuna haki sawa sawa na wengine? Kwani kama mmoja wetu angekuwako vile tunazungumza sasa tunatafsiriwa, yeye angesikia kushinda ninyi ambao mumetoka nje. Anasema hatutoshesi vile representation inafanya hata wakati wa Constitution Commission imeundwa inaonekana sisi inaonekana ni bahati leo tu, tumekuja kuulizwa maoni yetu. Inaonekana kwa wengine ni kama ile story tu ya Lancaster house Commission.

**Kaltuma Mursale:**

**Translator:** Mama anapendekeza ya kwamba wana ardhi ambao wanamiliki angependa wapewe nafasi ya kumiliki ardhi yao hiyo ndiyo pendekezo moja ardhi iwe ni yao wao wenyewe wanatumia vile wanavyotaka sio ati ardhi inakuwa ati movement haina restriction. Watu kutoka kwa wilaya jirani wanakuja wanaingilia kwa nguvu baadaye wanaleta ukosefu wa usalama, na tungependa, anapendekeza pia serikali ape sisi security ya mali yetu na sisi.

**Com. Lethome:** Sasa time yake inakaribia kuisha amalize sasa.

**Kaltuma Musale:**

**Translator:** Mama anasema amependekeza ya kwamba tunataka kumiliki ardhi yetu, sio eti kusema ardhi, miti ni yetu, na mchanga na yale iko chini ya ardhi, sio yetu kama vile ametoa mfano ya kusema (?) ambayo ni hii serikali imepea mtu binafsi na ni ardhi yetu na huyo mtu sio Mborana sio mtu katika hii wilaya, iwe ni sisi tunamiliki hata madini iko katika nchi yetu. Sio ati ni nchi tu ya kulisha mifugo halafu kesho tunaondoka. Ya pili anapendekeza ya kwamba sisi ni watu ambao tumbaki nyuma kwa elimu, kwa hivyo mashule yetu hapa haina standard mzuri kwa hivyo angependekeza ya kwamba mini grade ile ya kupeleka watoto university isiwe sawa na wale ambao wametoka Kenya kwa sababu nhao watu wako advanced kushinda sisi kwa hivyo mini grade yetu iwekwe chini na watoto wetu wapewe kama bridge course hivi saa ingine wapate elimu sawa na wengine katika Kenya. Pia anasema usalama wetu uangaliwe kwa wingi.

**Com. Lethome:** Hiyo asharudia.

**Kaltuma Musale:**

**Translator:** Amerudia rudia. Anasema sisi tuko na dini na ndini yetu ya kiislamu iko na a full system ambayo watu wanaweza kufuata kwa hivyo angependa tutawaliwe kutoka na dini yetu ya Kiislamu na mila yetu ya Kiborana ambayo haikosani na yale inasemekana katika dini.

**Kaltuma Musale:**

**Translator:** Pia anasema sheria ambayo imeundwa wakati wa ukoloni haifai sisi karibu 80% iangaliwe hizo zote ambazo haifai sisi na tuwachiwe ile ambayo inatufaa, na yale ambayo tumependekeza yachukuliwe na iwekwe maanani na iwekwe katika sheria ilikesho tunaweza kufaidika naye.

**Com. Lethome:** Haya asante sana mama nakuhakikishia maoni yako yamechukuliwa, asante sana. Tafadhalini sasa nikiambia mtu amalize, amalize. Watu ni wengi na tukiendelea hivi itabidi hata usiku. Kwa hivyo Shahad, haraka, haraka, dakika tano.

**Mr. Guracha Boro:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mzee anasema anaitwa Guracha boro.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Yeye ni jamii ya Modagashe location.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Anafurahia vile mumekuja kwa mabadiliko ya sheria.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Mzee anasema tangu Kenya ipate uhuru iko karibu miaka thelathini na nane.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Kati ya hiyo miaka thelathini na tisa ambayo iko,

**Guracha Boro:**

**Translator:** vile anaona sisi katika Kenya hatuhesabiwi kama watu wa Kenya.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Serikali ambayo iko na utawala miaka thelathini na tisa.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Mimi mwenyewe wakati Kenya ilipata uhuru nilikuwa miaka kumi na tano.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Leo hii anasema ako miaka hamsini na tatu.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Hakuna kitu anajua hii serikali inafanya,

**Guracha Boro:**

**Translator:** wala hajui kitu gani inaendelea mambo kwa sababu hana elimu, hafahamu vile mambo inaendelea.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Mtu anaweza kujifunza kutokana na masomo, 1

**Guracha Boro:**

**Translator:** unaweza kuwa na maarifa ya dunia na unaweza kuzaliwa na akili.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Anajua ye ye aki na akili ya kuzaliwa, sababu ambayo inamfanya ye ye hajui vile mambo inavyoendelea.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Hakuna sheria ambayo inatulinda.

**Com. Lethome:** Sasa nataka aanze kupendekeza.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Anapendekeza yale yote yamesekana hapa yote yapitishwe.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Anapenda customary law yetu ichukuliwe, amependekeza hivyo.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Wanadini ya kiislamu bali na hiyo ya customary, pia anapendekeza hiyo dini ya Kiislamu ifuatiliwe.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Anapenda wapewe security ya kutosha kwa mali yao na maisha yao.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Wakati wa ukoloni, sisi tulikuwa salama.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Tangu Kenya imepata uhuru, serikali yetu hatukulala salama hata usiku moja.

**Com. Lethome:** Pendeleza. Hiyo anarudia tena ya security, endelea kwa jambo lingine.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Sisi tumbaki nyuma kwa sababu ya ukosefu wa elimu,

**Com. Lethome:** Pendeleza.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Tungependa watoto wetu wapate elimu ya bure.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Angependa hospitali iletwe karibu na wao.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Anapenda barabara ya rami ipitie kila Sub-location.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Angependa kila nyumba iwe na tap water.

**Guracha Boro:**

**Translator:** Amemalizia haya.

**Com. Lethome:** Haya asante sana Guracha. Haya tupate sasa Abdillahi Rashid. Abdulahi Rashid yuko? Haya, haraka umeona huyo amependekeza haraka haraka hivyo, na wewe ni

(?) dot com fanya haraka haraka.

**Mr. Abdilahi Rashid:** Kwa majina naitwa Abdilahi Rashid. Ningeanza na Katiba, ningependekeza Katiba irekebishwe na 85% ya majority vote ni Parliament. Parliament to amend the Constitution should be limited. Yani marekebisho ya Parliament yasirekebishe Katiba yote. Ya tatu part of the Constitution should be beyond the amending powers of the Parliament eg. The basic rights to be amended by the public votes eg. 70% yani kuna part kama basic rights wabunge wasipatiwe uwezo sisi ndio tut-a-m mend (?) inatumiwa vibaya. Civic na MP election iwe tofauti. Siku ya civic election iwe kado, ya bunge iwe kado, ya President iwe kado.

Ya pili ni pande ya basic rights. Sisi jamii ya cushites tumekuwa marginalised, hatuna shule, hatupati passport, tunataka passport tusitafute kitu ambacho kinaitwa ulete kitambulisho ya mama yako, sijui birth certificate ya babu yako, tunataka tupewe passport, tutengenezewa barabara. Human rights violation, mambo ya wagala, mambo ya emergency yote tulipwe hiyo kunyanyaswa. Kwa sababu sisi ni second class hatuna haki katika Kenya.

Freedom of media. Media to be registered. We are fed up with KBC. Tunataka media iwe registered, mambo ya propagada KBC moja tumechoka naye. Tuwe na kitu kama Citizen, (*clapping*) tuwe pia na kitu kama FM, media iwe registered na wa-criticize positively.

Judiciary, iwe independent kutokea executive wasitumiwe vibaya. Appointment of Chief Justice ifanywe na Parliament.

(?) kwa Kadhi. Kadhi awe graduate na awe na shahada ya degree ya Kisamu. Kuwe na korti 1, korti 2,korti 3 na pia kuwe na pia kuwe na court of appeal ya waislamu independent hatutaki iwe ya Kenya hiyo ya kawaida hiyo ya serikali.

Executive, yani executive ni Rais na ministers. Power yao iwe reduced to avoid (?) sio mtu wote awe above the law, kama ni hivyo tunaweza tengeneza kitu kinaitwa impeachment na kuwe na procedure ambayo tunaweza fanya mtu akitumia kifua yake zaidi tunapiga a vote of no confidence. Nobody should be above the law. We don't need nominated MPs and Councillors. (*clapping*) that is a big thing of the government of the day to do those things to please their own things. Halafu Parliament quorum to be increased from 30 to 60 MPs and Councillors yani kuwe na quorum sio thelathini.

(?) ambaye ni maziwa lala kazi yake ni kutoa kitambi ovyo ovyo na madiwani ambao hawakuji kwa jamii tuna wa-sermon tunawaambia kwamba wao wamepotea sana kuja kwetu wakikataa tumuita mhadhara wa wazee, tunatengeneza, baadaye akizidi tunampatia vote of no confidence hiyo kitambi yake ipungue asanteni.

**Com. Lethome:** Haya asante sana, Commissioner sijui kama uko na swali lolote wataka kumuuliza. Asante sana kijana asante sana. Haya Bidu Adhi. Bidu Adhi njoo. Hivyo hivyo kijana ametupeleka tupeleke hivyo.

**Mr. Bidu Adhi:** Mimi naitwa Bidu Adhi Sora hapa kutoka Modagashe. Mabwana, wageni, watoto, vijana Asalaam Aleikhum.

**Response:** Aleikhum salaam.

**Mr. Bidu Adhi:** Jambo?

**Response:** Nzuri.

**Mr. Bidu Adhi:** Mimi maneno yangu ni mafupi kwa sababu mimi mwenyewe ni mfupi. Mimi nazungumza kwanza juu ya ardhi. Ikiwa sisi ni watu wa Modagashe na Isiolo district, sisi hatuna ardhi yetu, ardhi tumenyang'anywa. Hata mahali pa kuishi hakuna Mwenyezi Mungu anasaidia sisi kwa sababu ardhi yetu kila mtu anakuja kukanyanga bila ruhusa yoyote, bila kujua na mvua ikinyesha, nyasi ikitoka maji ikitoka bila sisi kuoja watu kutoka nje wanakuja kumaliza mpaka maji wanamaliza na nyasi inamalizwa sisi ng'ombe yetu inakufa kwa kiu na unakufa na njaa.

**Com. Lethome:** Sasa sheria mpya ifanye nini?

**Mr. Bidu Adhi:** Sheria mpya tunataka ardhi yetu isikanyangwe na mwengine vile wengine wako na ardhi tukae ardhi yetu kwa sababu sisi Waborana wa Isiolo hatuna ardhi lakini mahali penginewote wako na ardhi yao, hakuna ruhusa ya mwengine kukanyanga hata wakati sisi nakwenda njiani kutembea nje, ukikojoa kwa shamba uache barabara anasema makanyago mguu moja nashika nakupeleka kotini ilikuwa imakanyanga nyasi tu peke yake na hakuna ng'ombe hapa lakini mtu, hakuna mtu anastakiwa. Pia kama kitu kidogo inatokea na serikali ikitoka, askari anakuja bila sheria nakuja kupiga nyumba yetu napiga teke navunja nyumba yetu yote na bwana na bibi, bwana natoanga huko nje na rungu na bibi huko anachezewa na watoto

wasichana wanachezewa na hakuna sheria kama hiyo.

**Com. Lethome:** Sasa unapendekeza sheria mpya namna gani?

Kwa sababu pahali ingine sisi natembea nyumba ya mtu mtu anakuja bila warranty hakuna mtu anasimama mlango ya mtu na sisi wajinga hapa bila warranty nakuja kuua mtu ndani ya nyumba. Tunataka iwe kama sheria ingine mtu akikuja kwa nyumba ya mtu uje na warrant, huwezi kuja ati nakunja kuvunja (?) halafu unapiga teke. Tunataka nyumba wakikuja uje na sheria na warrant na district yetu akae na nchi yetu kila mtu anakaa kwa district yake.

No. 2 sisi si kama watu wengine kwa sababu watu wengine wanaweza kupata title deed kwa plot na sisi hatuna title deed plot yetu ni (?) ya kuhesabiwa. Tupate kama watu wengine title deed, kwa sababu yote tumeandikwa na unalipa rent plot, na unalipa license, na hakuna title deed na unajaziwa, sisi hata kwa nini sisi tunalipa. Hatupati vile watu Kenya mzima wanapata. Na watoto wetu hapa ukisoma primary kidogo tu na mkifika secondary hakuna pahali pa kusoma, na ukienda university unaenda kuhangaika hata bila kupata. University yetu na secondary yetu yote ikuje karibu na sisi ili watoto wetu wapate faida vile watu wengine wanapata, Kenyan nzima vile wanapata kwa nini sisi tunarudi nyuma? Sisi tumeachwa nyuma kabisa wainuliwe, tuwe karibu na Kenya yote. Na soko sisi hatulimin shamba, shamba yetu ni ng'ombe na mbuzi na hakuna soko ya kuuza. Tunataka soko yetu ifanywe kwa ng'ombe yetu, kwa mbuzi yetu pahali mali yetu iko wafanye soko hapa. Kwa nini sisi tunakosa soko na watu wengine hata hata wali iko mboga anaiva viazi na cabbage iko na siku yao. Kwa nini sisi nakosa watu iko na ng'ombe na mbuzi tunakosa soko? Hii ni kudharau kabisa. Afanye sisi kama Kenya ingine mimi napenda namna hiyo. Na hospitali, kama tunapata mgojwa hakuna hospitali hapa. Mtu akufe kwa sababu wengine

(?) wanakimbia na wale hawana nguvu wanakufa hapa hapa tu kwa hivyo hospitali inje hapa, ikule karibu yetu kwa nini tunawachwa nyuma tunafanywa wanyama na sisi ni binadamu. Ninyi bado andika maneno yangu siju kwa nini mnazungumza tu mimi naona tu.miminaona tu. Kwa nini wewe unaita kwa sababu ameweka mimi hapa. Mnanidharau sio?

**Com. Lethome:** Apana.

**Mr. Bidu Adhi:** Wacha basi.

**Com. Lethome:** Endelea mzee Pole mzee pole sana

**Mr. Bidu Adhi:** Town yetu hapa, town hiyo yetu hapa tunaita Modagashe, mimi bado ona, mimi nawaona leo naona town hiyo ni chafu sana, tena town tambarare, lakini ukiangalia ndani yake kama mtu anajua habari ya town hii town inashinda Kenya mzima kwa sababu barabara wacha barabara ya Kenya barabara ya (?) kutoka nje yote unakutana hapa. Hii town ingekuwa town ya maana ya kushinda Kenya mzima town hii sababu sasa nakuwa maskini tambarare hata ninyi wenyewe jana mulilala hapa mimi najua ninyi hamkupata maji ya kuoga wala hamkupata maji ya kunywa kwa sababu ninyi nakataa hii

umejua ile na hata ninyi nasikia wametoa borehole ya maji walitoa mara tatu hapa na munakula njiani hakuna kitu nafika hapa na huko juu wanaandika watu wa Modagashe wanapata maji ya kupanda mboga hawa hawawezi kununua mboga huko nje kwa sababu plot yao yote maji inajaa. Ninyi munaandika uongo hata ninyi wenyewe muliona hata jana hamukuoga kwa sababau hakuna maji hapa. Tunapenda mijin yetu iwe kama mijji ingineipate maji ya kukunywa na binadamu sasa sisi hakuna kunywa maji yote (?) huko. Ile kisima kidogo sisi nachimba asubuhi sisi nachota usiku nyandau nakunywa na fisi nakula asubuhi inakuja kukula ile mgojwa hapa napata

**Com. Lethome:** Unaweza toa maoni ingine mzee tafadhali.

**Mr. Bidu Adhi:** Tafadhali sisi tupate maji vile watu wengine wanapata.

**Com. Lethome:** Haya asante.

**Mr. Bidu Adhi:** Mimi ningesema mengi lakini nyamesemwa na watu wengine mbele yangu siwezi kurudia. Asante sana.

**Com. Lethome:** Asante sana mzee asante nashukuru sana. Haya Jamila Hilole halafu msichana huyo atakuja. Jamila nafikiri utazungumza kiswahili wewe.

**Jamila Hilole:** Kwa jina naitwa Jamila Hilole, yangu ni mapendekezo tu. Mapendekezo ya kwanza ni kuhusu citizen. Citizens sisi tunataka watu wa Modagashe, birth of parents, naturalization na registration. Hiyo inamaanisha ni mtu kuzaliwa hapa ndio mtu atakubaliwa akuwe citizen. Na yule anatoka nje,five years and above akiishi hapa ndio atakuwa citizen. Spouse of Kenya citizen regardless of gender, mtu ambaye ametoka Somalia ama London akija hapa halafu akiolewa atakuwa Kenyan citizen.

Kuhusu basic rights, death penalty should be abolished. Kile kitu tunakubali watu wa Modagashe, mtu akiua mwenzake ndio atauawa, lakini sio kwa makosa ingine ni kuadhibiwa au kufungwa sio kuuawa ovyo ovyo.

Health, hapa Modagashe tuko na hospitali moja ambayo hata hiyo ni pande ya Garissa, na huko kuna wakati (?) inakuja. (?) ikikuja hatuwezi vuka huko.tunataka hospitali zijengewe upande wa eastern angalautuko nayehuko tunasaidiwa bado lakini tunataka tupate upande wa eastern hospitali.na hospitali yenyewe tukienda tunalipa tu pesa hata asprin yenyewe hatuwezi chukua bila pesa. Tunataka hiyo hospitali tupatiwe bure.

Shule pia. Tunaambiwa shule ni bure, lakini hata primary level si bure. Kila wakati watoto wanafukuzwa nyumbani, watoto wanatumaniwa nyumbani watafute fee. Hata hiyo shule si twenty shillings ni zaidi. Hata kama ni cost sharing tunataka iwe kiasi kidogo ambayo sio zaidi.

Employment, hapo kwanza ni serious. Kwetu, wanafunzi wengi wamemaliza shule na wamekaa. Tunaenda kutafuta polisi tukipiga laini, wakituona sisi tuko na nywele nyepesi ni nyuma tu. Nyumbani hakuna kuangaliwa kama umepita, hakuna grade yako inaangaliwa, tunafanywa marginalised community sasa tunatolewa hata kwa file. I recommend ya kuwa tusifanyiwe ubaguzi, tukuwe sawa Kenya yote.

Kuhusu local government, councillor. Mtu akitaka kusimama hiyo cheon ya councillor, awe na masomo ya O' levels. Na kitu moja nominated councillor iwe cancelled, hatutaki kwa sababu, hao watu ni kisiasa imeletwa, tunataka wawe elected tu. Hao nominated hatujui ni nani alimkubalia pale ni mtu tu amechaguliwa, pengine ni bunge alijipendea mwenyewe mtu yake, kisiasa, kifamilia kwa hivyo tunataka hiyo nominated councillor iwe banned, scrapped off.

Marginalised communities, sasa hii nina notes briefly. Every person belonging to racial cultural a linguistic and ethnicity or religious minority, including the pastoral communities shall enjoy the same treatment and protection of the law as other people. Sisi tuwe haki sawa na watu wengine, watu wa down country hatuna haki sawa, njia hatuna, maji hatuna, matibabu hatuna, masomo ya bure hatuna kama wengine unasikia wengine wanaenda university ni kwa sababu wanapata masomo from beginning hata kama ni shule wanaapata shule ya bure kutoka primary, secondary level kwa sababu secondary hawatatumia fare ya kwenda mahali ingine kusomea secondary mahali ingine, watasomea kwao hawatakuwa wanapata shinda lakini mzazi hawezi akaafford kupeleka mtoto shule pamoja na fare. Tunataka tukuwe sawa na Wakenya wengine. Shukrani.

**Com. Lethome:** Ngoja kidogo hapo, umesema adhabu ya kuuliwa itolewe, na adhabu ya mzee kumpiga mke wake unataka iwe nini nkwa sababu kuna mmoja alipendekeza, tunataka hata wewe upendekeze.

**Jamila Hilole:** Sasa, according to me according to islam mmwanamume akikosea bibi yake hawezi a. kuna kupigwa kupigwa mara mbili. Kuna slight beating, na kuna kupigwa kama mnyama. Hiyo islam yenyewe haikubali. Inakubali slight beating.

**Com. Lethome:** Unataka sheria iweze kumuadhibu huyo (?)

**Jamila Hilole:** Kinyama sheria ya Islamu..

**Com. Lethome:** Pendekeza adhabu yake, afanywe nini? Ama mzee ako hapa unaogopa?

**Jamila Hilole:** Hapana, ni kadhi tu iangalie lakini sio kufungwa, mzee wako akifungwa unapata shida na watoto.

**Com. Lethome:** Yule msichana sasa aseme jina yake halafu atoe maoni yake.

**Nasra Osman:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Anaitwa Nasra Osman.

**Nasra Osman:**

**Translator:** Anasema hataki wasichana watahirishwe. (*clapping*)

**Nasra Osman:**

**Translator:** Hana maoni ingine.

**Com. Lethome:** Haya asante sana, asante. (*clapping*) haya asante tunaendelea. Tumpate sasa huyu bibi kutoka Siricho. Shoba Bagaja kutoka Siricho.

**Shoba Bagaja:** Salaam aleikhum.

**Response:** Aleikhum salaam.

**Shoba Bagaja:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mama anaitwa Shoba Bagajaro, ametoka Siricho.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Mama anasema amefurahia vile sasa constitution change imeanza kuletwa, amefurahia sana kwa sababu anasema wakati wa ukoloni, baada ya serikali ya ukoloni kuondoka, serikali ya Kenya kupata bendera ansema waliletwa kwa concentration camp kwa sababu walipinga chama ya KANU, watu wa hapa. Baada ya kupinga chama ya KANU watu walilazimishwa katika concentration camp, watu wanapigwa, watu wanaumizwa, watu wanaauawa, mali nauawa, mali napokonywa kwa nguvu, wanawake wanafanywa rape, (?) ambaao waliuawa pamoja na wanawake ambaao walifanywa rape.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Serikali ni yetu lakini hata hivyo bado wametuumiza, hatujapata pole na tuna watu wa hivyo hivyo maskini na ardhi yetu inafanywa wazi kwa kila mtu, ardhi, inasemekana ni Trustland, hatutaki mambo ya Trustland, hatutaki jambo ya Trustland, tunataka community land, ardhi yetu sisi wenyewe tusimamie.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Anasema leo katika sheria ya serikali ya Kenya, madini ambayo iko chininya ardhi, kitu yote ambayo iko chini ya ardhi, futi tano inakuwa ni ya serikali, kwa nini inakuwa ni ya serikali na ardhi ni yetu? Anapendekeza kwamba madini yote iwe inamiliwi na wananchi.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Mama anasema serikali imesema wanyama wa msituni ni wake, lakini leo hii anasema kutoka mwezi wa nne mpaka leo, Siricho vile ametoka asubuhi, hata jana usiku, wanyama wamekula mifugo, karibu zaidi ya mia tano imeuawa na mnyama simba. Anapendekeza serikali ije ichukue hiyo wanyama wake ipeleke pale inastahili kukaa, na walipwe ridhaa kwa wale wanyama wamekwisha kuliwa na mnyama huyo simba ama fisi hata kama ni kuku.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Mama anasema ye ye vile yuko hapa ametoka Sirichwa leo asubuhi na walitoka Sirichwa saa mbili na wamefika hapa saa tano na Sirichwa iko 40 kms kwa sababu ya ukosefu wa barabara ndio wamepata hiyo shinda. Anapendekeza wapewe barabara mzuri sawa na vile wale wengine katika Kenya wanaishi. Barabara ya rami iwekwe kutoka sirichwa hadi hii mijji na iendelee mpaka kwa district headquarters mpaka Nairobi.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Anasema sisi hatuna mali na mali yetu serikali ndio imemaliza, lazima serikali ipatie sisi masomo ya bure kwa watoto wetu, kutoka nursery hadi kwenda university kumaliza.

**Shoba Bagaja:**

**Translator:** Anasema tumelaani hiyo juu ya serikali kwa kufinywa na kuwa marginalised kwa sababu serikali ndio waliacha sisi bila msaada yoyote. Mama amemaliza haya machache.

**Com. Lethome:** Asante sana mama, asante sana tunashukuru. Tumpate sasa, Ahmed Shariff Hassan.

**Mr.Ahmed Shariff:** Shukrani Bwana Commissioner. Katika kupendekeza, mimi jina yangu naitwa Ahmed Shariff hassan, nafanya na idara ya huduma kwa jamii katika tarafa ya Siricho ambye headquarter yake ni hapa Siricho. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa hakika tuko hapa katika hali ya kupendekeza kwa sheria mpya. Kupendekeza kwa sheria mpya napendekeza hivi, katika serikali yetu ya Kenya iko kitu inaitwa social welfare programme, kusaidia maslahi ya jamii ambayo vile mnajua katika bunge ya Kenya ile mlango wabunge wanaingia katika nyumba hiyo wanaandika kule tunaenda nkwan social welfare, kuangalia maslahi ya jamii kuangalia haki ya jamii na katika hii wizara ya huduma za jamii katika serikali yetu tukufu ya Kenya niko nkitu inaitwa social welfare programme ambaye wale wasiojiweza wale hawajabahatika hawana mali wanasaidiwa na (?) na fedha na asila fulani wanunue restocking na kusaidia wazazi watoto wao kwa njia fulani kununulia rations wale watoto amba wako kwao. Jambo kama hii inapewa nguvu ambayo jambo ya social economic project ambayo inatakikana upewe

katika Katiba ya Kenya kwa wananchi Wakenya ambayo inaweza kusaidia wasiojiweza, wasaidiwe na fedha ambazo wanasaidia kazi yao kwa maana leo mtu ako na nguvu amepata ajali ya gari mtu amekosa mkono ana mkono mmoja anaweza

(?) jirani yake lakini anahitaji fedha asaidiwe na serikali ambayo itakuja baadaye. Kitu kama hii ambayo inaweza pewa wananchi kwa wakati wa maisha kuendelea mbele kusaidia watoto wao, hiyo inaitwa social economic project katika serikali hii ambayo tayari iko katika serikali yetu tukufu, mpaka hivi sasa iko pesa kidogo kidogo kule ndani lakini ni ile sehemu ambaye wakubwa tu ndio kule wako ndani katika serikali, P. S na Director, na Commissioner hiyo tu (?) tu. Sehemu kama Isiolo haonekani hata mjumbe akienda pale anafukuzwa. Vile munajua ile hazina ya ambaye chairman (?) hiyo ambaye mwenye kiti wake sioni kama Isiolo hata imenyimwa, hata forms yetu katika wilaya hii imeweka kwenye kule Nairobi ni ajabu kubwa sana. Kwa hivo haki sawa ipewe kwa wasiojiweza katika hiyo (?) organization kama hii ambaye baadaye itakuja katika nchi yetu. Katika Katiba yetu twapendeza jambo kama hiyo.

Zingine kwa hakika ni wajibu na ni haki ya serikali yejote iwape wananchi wake elimu ya bure, matibabu ya bure kwa maana kama serikali iko imara iko na rasilmali kubwa ambayo inapata misaada kutoka nchi juu nya lengo hii na mifuko yake pia ni kubwa, kwa hivyo ana uwezo wa kulisha watu wake, anaweza kuwawekea elimu bure, matibabu ya bure ambayo tunapendekeza katika Katiba ya Kenya ambayo inakuja. Jambo hili napendekeza ya kwamba Kadhi au Chief Kadhi awe yule ako kwa kiangazi No. 3, ipe sawa kama korti ya Kadhi na korti ya Chief Kadhi ipewe sawakama korti ile ingine katika nchi yetu tukufu ya Kenya ipewe

sawa kabisa ipewe security sawa sawa ambayo hivi sasa leo Chief Kadhi au Kdhi yule wa Isiolo Garissa haonekani kama korti ya serikali na ambaye hawa wameajiriwa na serikali. Hayo tunapendekeza ipewe haki sawa kama korti ile ingine iko katika taifa yetu ya Kenya. Na

Kadhi kuu ambaye (?) Chief Kadhi tunapendekeza tupate Kadhi mwingine ambaye

(?) kule aidha Mombasa au Nairobi, sio lazima Nairobi peke yake tunaweza pendekeza hata akae Garissa ama Moyale kama sehemu hizi Somali hata wakati wa ukoloni sehemu ya North Eastern Province (?) hata na Moyale ikule mboga ambaye unawezekana sio Nairobi peke yake watu waweza

(?) kitu yoyote kule halafu Nairobi inapora kila kitu nanyanyaswa tumevumilia Kenya hii.

Jambo ile ingine ambayo napendekeza katika sheria yetu mpya, kina mama katika Kenya hii hawajapewa haki sawa kama sehemu yetu ya Uganda ama Tanzania kwa mfano East Africa ambayo hivi sasa hata (?) iko pamoja kule ambako nimeshaona Minister wa elimu, Prime Minister, Vice President ni mwanamke, kwa hivyon hata Kenya lazima ipewe haki sawa katika cheo chochote kile cha juu kwa akina mama wakenya amba wako na uwezo hata katika Ilamu iko wamama amba wako na shahada karibu ma-degree tano sita, wako na katika hali hii hata waislamu wapewe haki sawa katika nchi hii ya Kenya katika Katiba mbaye inaonekana mila ya Kenya inaonekana kama nchi hii ni ya christianity lakini serikali ya christianity kwa hivyo waislamu wananyimwa sana, hiyo jambo ifutwe kabisa, na tunapendekeza katika Katiba mpya ya Kenya watu wote wapewe haki sawa hakuna kufuata maneno ya dini ifanywe kama kulentanzania hata waislamu ni majority kama millioni kumi vile ambavyo msemajji mwingine hapa amkariri kwa hivyo tunataka hata akina mama wapewe haki sawa na nafasi ya jamii ya

Islamu pia iangaliwe katika hali ya juu.

**Mr.Ahmed Shariff:** Jambo lingine.

**Com. Lethome:** (?) maliza.

**Mr.Ahmed Shariff:** Okey, jambo lingine katika hali ya wale watoto ambao hawana wazazi, mimi napendekeza wale wazazi wao walikosa nguvu za tiba wengi katika Kenya hii leo wale watoto wanatembea tembea barabara tunapeleka kule mission, parish na missionaries na kule Institution ya Islamu kitu kama hiyo inastahili serikali ya Kenya iweke katika nchi yake ijengwe institution kwamba katika taifa hii popote katika wilaya yote wale watoto hawajabahatika hawana wazazi, wazazi wao hawana nguvu, niseme leo mimi sina mali, mtoto wangu hakuna haja ya kutembea barabarani ni wajibu wa serikali ichukue mtoto huyo ilishe, isomeshe, iweke katika kituo hiyo mpaka elimu ya juu. Naona katika Kenya yetu leo watoto wanapelekwa kwa missionary lazima aingie dini ya kikristo. Okey asante sana, kwa hivyo jambo hiyo mimi napendekeza hivyo serikali iwekw katika Katiba yake ijenge (?) institution, orpan institution, institution ya ambayo wale watoto hawajabahatika kitu kama hicho napendekeza katika Katiba kama nchi zingine katika dunia yetu Africa hata katika kule nchi ya ng'ambo iko kitu kama hiyo hata Tanzania, Uganda iko kitu kama hii sana lakini Kenya yetu tunashangaa hao viongozi wetu hawajajali maslahi ya wakenya kwa hivyo tunapendekeza hakuna haja ya watoto kukaa barabarani..

**Com. Lethome:** Unarudia sasa.

**Mr.Ahmed Shariff:** Haya asante sana, wacha nitasimamisha hapa, Commissioner shukrani.

**Com. Lethome:** Haya asante sana. Tafadhalini mtu ukija usikariri jambo moja mara mbili, mara tatu, dakika ni chache, pendeleza ukiendelea bila kukariri, usirudie rudie, hebu waambie kwa kiBorana wasirudie rudie. Chief, waambie mtu asirudie rudie kitu ambayo amesema anarudia tena.

**Chief:** (to Borana)

**Com. Lethome:** Wamefahamu sasa. Haya Dika Abduba Molu. Yuko? Ameshaondoka. Asante ametusaidia. Guyo hasano.guyo Hasano, haya. Chief kuna kazi.

**Mr. Guyo Hasano:** (in Borana dialect, through translator)

**Translator:** Mzee anasema anaitwa Guyo Hasano na ametoka Sirichwa Location.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Jambo ambayo angependa kuzungumza wengi walizungumza.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Yale maoni ambayo yamepewa hapa anasema sisi tuko pamoja. Anataka kuongeza machache.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Yale anapenda kuongeza ni jambo la ardhi.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Wakati za koloni kila mtu alikuwa na nchi yake.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Wazee wa karne hiyo wengi wamekufa sasa ni watu wachache wamebaki.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Wale ambao tunapakana kama tuseme watu wa Garisa kuna namna tunaishi katikati yetu.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Kama ni wizi wa ng'ombe umetokea ama mtu anahaja ya kwenda kuvuka kwa wilaya ingine kuna cheti ambayo unapewa ambayo inakubali wewekwenda kwa wilaya ingine.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Na wakati huo anasema mtu akiibiwa ama mifugo ikiibiwa si serikali inatafuta bali ni wazee wanajukumu ya kwenda kutafuta.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Wakati huo nyasi na maji ilikuwa na mwenyewe.lakini tangu kenya ilipata uhuru,

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** ardhi ya Kenya yote inakuwa free.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema sisi tunakosa maneno yani maneno yetu inakosa dhamana.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Wazee wanakosa jukumu watu wabaya ama wale hawana mali ambao wanakaa town ama wanachukua jukumu yote ya kueneza mambo baya katika nchi.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anapendekeza ya kwamba mipaka ya zamani irudi na kila mtu aheshimu mpaka ya mwagine.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Hiyo ndiyo jambo inaweza kuleta usalama kwa wengi.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Yake ni hayo.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema sisi katika mila tuna sheria yetu wenye.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Kwa mfano watu wakipigana, assault ama kuvujana kichwa ama kuvujana mwili ama kuumizana kuna sheria ambayo inaambatana na hiyo.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Leo wazee hawana maneno na mambo ikienda kwa kortini haiishi inachukua muda murefu ambao wale watu wanaumizana, pengine kesi yao inapotea.

**Com. Lethome:** Anapendekeza nini kuhusu wazee?

**Guyo Hasano:**

**Translator:** Anapenda wazee wapewe mamlaka na sheraia ya kienyeji hiyo iwalinde.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anapendekeza hiyo sheria ya customary yote ichukuliwe maanani na iwekwe katika laws of Kenya.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Hiyo ni hayo.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema sisi ingawa tangu Kenya ipate tuko mika thelathni na tisa hatuoni serikali karibu na sisi tungependa serikali iletwe karibu na sisi yani anataka majimbo na angependa barabara ire kebishwe tuwe na barabara nzuri, tuwe na mawasiliano kama simu, tuwe na sitima, tuwe na hospitali, tuwe na shule za kutosha.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema mali yetu, mifugo yetu imekosa soko kwa sababu ya ukosefu wa barabara ukosefu wa mawasiliano.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anapendekeza serikali iletwe karibu.

**Com. Lethome:** Hiyo ameshasema asirudie tena.

**Guyo Hasano:**

**Translator:** Sasa anaendelea kwa maneno ya wanyama wa msituni.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Wanyama wa msituni ni wa serikali.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema wanyama hata zamani wako na inakula mifugo lakini hii ya sasa anasema ni karibu miaka saba sasa, wanyama wamezidi na imemaliza mifugo ya watu.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Miaka saba imemaliza binadamu na mifugo.

**Com. Lethome:** Anapendekeza nini katika sheria mpya?

**Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema kama wanyama ni wa serikali ichukue jukumu ya kuzuia wanyama wake wasivamie mali yetu na isivamie watu, imalize watu pia anapendekeza ya kwamba kila mtu alindwe kutokana na wanyama moja, pili tulipwe ridhaa ya mali yetu na watu wanaokuliwa na simba ama wanyama wa msituni.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema hapa nchi yetu hatuna maji, tungependa maji mazuri kwa binadamu, na kwa mifugo.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Ameunga wale watu wametangulia mbele yake mkono.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Kwa haya machache amemalizia hapa.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anasema wale hawajiwezi wako na shida.

**Mr. Guyo Hasano:**

**Translator:** Anapendekeza wale hawajiwezi wapate haki sawa na wale wanajiweza. Wale wazee, akina mama ama wazee wale makamu ambao hawajiwezi waangaliwe sawa na wale wengine. Wapatiwe msaada wa kutosha, waangaliwe special, wapewe special attendance na serikali.hasa kama watoto ambao wameachwa na wazazi, watoto ambao akina baba wana-neglect ama nini iangaliwe iwekwe katika sheria.

**Com. Lethome:** Haya asante, mzee asante sana, Sheikh Ishaak Alio.

**Sheikh Alim:** Salaam aleikhum (?) mimi jina langu ni Sheikh Ishaak Alim na sina mengi ya kusema ni kidogo tu nitazungumza. Na hiyo kidogo ni kuhusu juu ya sheria. Tuko na bahati leo tuko na sheria leo ambayo tunaunda, zamani hatukuwa na nafasi ya kuita sisi ama kuchukua nafasi ya kulete maoni ya kulete sheria. Lakini kwa bahati leo sisi tuko na bahati. Kwa hivyo tukiwa sisi tuko na bahati, nafasi hii na sisi ni waislamu lazima tutaje ile kitu tunahitaji kulingana na sheria ya kiislamu. Sisi hatuna sheria ingine. Kama sisi ni waislamu sheria yetu ni ya Islamu, ni ya mtume Mohammed (?) na ni kitabu ya Koran tukufu Sulhana Wataala, hatuna kitu ingine. Mimi nimependekeza katika sheria hii ambayo inaundwa leo sheria ya Islamu, ipewe nguvu ya kutosha. Sheria ya Islamu haina hakimu ingine, hakimu yake ni Kadhi, tumesema Kadhi apewe jukumu ya kutosha, mimi napendekeza Kadhi apewe nguvu ya kutosha ijulikane Kadhi ni mtu ambaye anasimama mahali muhimu, na tumesema Kadhi akuwe mahala tatu, three classes; class1, class 2, class 3. kama mmoja anashindwa, ajue ile ingine afanye appeal kwa ile ingine ili amalize hiyo kesi. Kesi ikiwa kidogo, ikiwa kubwa, kesi yoyote ambayo anahuksika uma ya Islamu inaenda kwa Kadhi aweze kwenda kwa magistrate ingine ama (?) ama mambo ingine inaenda kwa Kadhi. Mimi naomba ama nimependekeza, katika sheria hii, Kadhi awe kwa ofisi yake awe na adhabu yake na ajulikane rasmi.

Ya pili ni upande wa sheria ingine mahali ambapo waislamu wanaishi. Watu wanaleta kitu ambayo inaitwa club, night club. Unasikia mahala kama Garissa ni mji wa Islamu, ukienda leo usiku kitu inaimba, kuna drum inapigwa, ukiuliza ni kitu gani ni night club watu wanajisanya, wanakusanyika huko wanakunywa pombe, wanafanya dansi na aina ingine ambayo yanadhuru,

ambayo yanapinga dini ya Islamu na sheria ya Islamu. Mimi napendekeza katika sheria hii ambayo inaundwa leo, kitu kama hiyo ikatazwe na isimamishwe mahala ambapo waislamu wote wanaishi.

Yangu ingine ni upande wa elimu. Elimu, shule, serikali ameimba usiku na mchana, anasema shule, shule, shule

(?) ya education ni mzuri ni maisha ya dunia lakini ile kitu ambayo Mwenyezi Mungu atauliza sisi siku ya kiama ni dini. Mimi napendekeza serikali pia iweke nidhamu ya kusoma hii dini ya Islamu. Kama ni kujenga madrasa ajenge wa sababu hata kujenga shule usiku na mchana tunasikia mahali fulani wanafanya mchangano wa kujenga shule kwa hivyo tunataka kama ni kujenga madrasa pia serikali pia achukue nafasi yake ya kuchangisha pesa yake na kuweka ujenzi huo na nidhamu, administration (*clapping*) waajiri walimu, watoe ishahara ya walimu na kila kitu. certificate ya madrasa itoke under ministry of education awe recognised. (*clapping*) ndivyo watu wa Islamu vijana wakisoma secular na Arab pia pamoja na dini pia pamoja ndiowanaweza endelea na wanawenza kuwa na elimu zaidi.

Pendekezo yangu ingine ni hivi, kwa NGO's kuna NGO's ambao wanatoa msaada, msaada wa aina nyngi. Kuna chakula nyngi inaletwa, pesa nyngi inaletwa. Upande wa NGO's, Islamic NGO's wako na shida. Wakileta msaada ya chakula hasa wakati wa Ramadhan sisi tunasikia ya kwamba kuna meli kadhaa ambayo imefungwa huko bandari Mombasa kwa sababu ya tax ndio inasumbuliwa. Kama ni European NGO's, NGO ingine ya kikirtisto, inakubaliwa hata kama inalipishwa tax, chache sana inalipishwa hata saa ingine hakuna lakini waislamu wamehuzunika ya kwamba wanakosa msaada kwa sababu ya kuweka tax, bila kulipa tax hakuna kukubaliwa hata kuleta ngunia moja ya mchele ama hata tembe moja ya kuvuturu waislamu kulete nini katika nchi kwa sababu ya tax wanasema mpaka ilipwe tax, ndio inarudi ama ile chakula inaozea huko ndiosasa waislamu ama waarabu wameshindwa kuleta msaada wao katika Kenya hii. Wako na aina nyngi, wako na mambo mengi ya kusaidia watu lakini wanaogopa, wanafungwa na tax, wanaweka tax kubwa, high tax. Tax ni nzuri lakini ni vizuri kuleta tax kidogo, kuweka tax kidogo ili wananchi wafaidike ama waislamu wafaidike na hayo mimi napendekeza ili mambo kuruhusu waislamu yote awekwe freedom na tuendele na sheria yetu

(?) dini ya Islam kwa sababu mfano dini ya Islam leo anasema

mtu akiuawa yule mtu aliua huyo mtu lazima ataua, ingine sheria ya Islam inatueleza mtu ambaye alifanya ndoa akifanya zinaa atauawa. Mtu akitoka dini, tunaita

(?) akitoka dinin atauawa lazima kama tunakuwa na Kadhi, na sheria yake itakuwako hiyo yote itakuja chini yake. Kwa hivyo tukisema tunatimiza sheria ya Islam na tusipotimiza ambapo tunatimiza ile iko na Mwenyezi Mungu Sulhana wa Taala atatuuliza mbele yake siku ya riama Ishara. Kwa nhayo machache, yangu mimi nimependekeza mbele yako ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Sasa Sheikh umesema night clubs zipigwe marufuku side za waislamu, na miraa na mabaraza katika sehemu za waislamu unapendekeza kitu gani?

**Sheikh Alim:** Napendekeza hata miraa ni moja ya drugs. Hatuna faida naye kwa sababu nikichukua Modagashe hii gunia kadhaa ya miraa inatoka Meru inaingia ndani nya hii town watu wanakula, mtu ambaye yuko na shilingi mia moja mtoto wake ako na njaa badala ya kupelekea ile shilingi mia moja anunulie mtoto maziwa, anakula miraa. sasa ile gunia tatu ya miraa inajazwa pesa inarudishwa Meru. Kwa hivyo miraa ni faida ya wengine si faida ya waislamu. mimi nimependekeza hata hiyo

miraai isimamishwe.

**Com. Lethome:** Asante, asante. Sasa tunajua kuwa time ya swala yake adhuhuri inakaribia ama sivyo?

**Response:** Ndiyo.

**Com. Lethome:** Mimi ni msafiri kwa hivyo sitaenda kuswali na hata kama nitaenda kuswali nitaacha mwenzangu ataendelea nanyi. Kwa hivyo tungependa hivi kama watu wanaweza kwenda kama kuna watu amba ni msafiri wanaweza kuendelea kutoa maoni yao watu wa swali na warudi tuendelee na maoni. Sawa. Ama mtaandike hapa hapa tuswali hapa kama tunaendelea na shuguli. Kwa hivyo sisi hatutaki kuondoka hapa tunataka kuendelea, sawa. Haya Abdi Diba, Abdi Diba amezungumza? Abdi Diba.

**Abdi Diba:** First and fore most may I thank the almighty Allah who has given me this nice opportunity to sustain this crucial moment.

**Com. Lethome:** Hebu msikizeni, msikizeni Abdi Duba. Hamtaki kumsikiza?

**Abdi Diba:** First I don't know the (?) because it is also the national language, English I will also elaborate in kiBorana. So my (?) was that all the (?) be equally involved in the management of resources, that is the elder women and youth. (*interjections inaudible*) (In kiBorana).

The second point was that in the local government, was that, the local government, the community, accessibility to be the councillor. I'm talking about the qualification of the councillor. If we say that the councillor should be a form 4 leaver, that one the other people are illiterate. Also we said, the councillor should be somebody who can understand Kiswahili and English we cannot say form 4 but std 8 to form 4, we cannot say that it is only O' level. That has a right to vote for or to contest for the std. 7 to form 4 not only the form 4 I'm saying std 8, primary level to the O' level.

The councillor like the nominated councillor even the (?) person should be scrapped off because the nominated councillor is appointed by the parliament (?) MP (?) and this nominated councillor bring corruption among the councillors themselves. Like the previous Isiolo district, I can talk, you see they bring the corruption and they started among the internal local government so the nominated councillor should be scrapped off.

The other point, the chairman of the Kadhi council should be appointed by the people withinthat field of the council in those elections. Yani kwa mfano debe ya councillor tukipiga tulipomaliza tena tutachagua chairman of the Kadhi Council hapo hapo and the different offices and (?) be at its own location. For example Modagashe, the councillor should be

here and also the chairman of the Kadhi council should be in Isiolo district and be controlled by the regional assembly and mayor of the council of municipal council should be the province or for example the councillor if he is not capable to do things for us in one year, this person to be recalled. How are we going to recall? We are going to write a letter to the mayor, if he refuses what action are we going to take or the remedy? We are going to take a big action which is so paramount and that action is going to call through the ECK, Electoral Commission and he is going to be re-elected another councillor

(?). for that may I say thank you.

**Com. Lethome:** Okey thank you Mr. Diba. Can I have Siad Noor. Yuko ama amekwenda? Haya njoo.

**Mr. Siad Nur:** Natoa shukrani kupata hii nafasi nije napatiane yale kidogo iko kwa kichwa yangu lkiwa itanisaidia maisha yangu yajayo pia ya watoto wangu. Nafikiri nikiwa napatiana kidogo kwa miaka nafikiri nimemaliza miaka arobainne, Kenya nayo iko thelathini na tisa nafikiri nashinda mwaka moja tu. Kwa hivyo ningependekeza kutoa maoni yangu hasa mimi naona tukiwa watu wa Northern Kenya ama ile develeplment tungefikia yale tunayolia saa hii yote inamezwa na administrators. Nikiwa unaanza chief mpaka P.C. kwa hivyo natoa maoni hizo ofisi zifungwe kwa sababu haisaidii sisi yale ingetuletea development yote inakwishia hiyo ofisi. (*clapping*) Tunalia masomo, utapata masomo namna gani D.C anakalia ofisi. Unalia maji masafi, utapata nanma gani mpaka ipitie DDC members hakuna kitu itafikia kwa hii location kwa hivyo tutasikia development namna gani kwa hivyo Bwana Commissioner, tunaka hii maoni tunatoa leo wacha radio kwa T.V tuonekane kama tunatoa maoni hivi, hizi ofisi hakuna faida inatuletea katika nchi yetu ya Kenya hasa Northern side ifungwe hakuna kitu inatusaidia, hiyo ni maoni ya kwanza.

Inginge, hospitali. Akina mama wanapata shida hasa wakati wanajifungua. Hatuna hospitali bora mama anakimbizwa Isiolo, anakimbizwa Garissa, kufika huko unasikia mtoto amefariki njiani ama mama amefariki njiani. Mbona hatuwezi kuwa na haki sawa na Kenya wengine? Kwa hivyo tunaomba hospitali zetu kuanzia tarafa mpaka tuseme Sub-locations tunataka huduma ya haraka kulingana na Wakenya wengine hibuniwe hasa mkoaa huu wetu wa Northern side. Mimi siongei mambo ya Isiolo peke yake ama Garissa peke yake nasema Northern nikisema Northern tuko jumla sisi ni wafugaji. Lingine hatuna soko ya uhuru kwa sababu unasikia saa hii mtu akijaribu kusafirisha mbuzi mia moja saa hii saa hii analazwa hapa hapa kwa sababu hana permit. Permit naye hakuna mahali inaweza kutoka kwa sababu maskini mwenyewe ameamua kulipiza watoto wake karo pengine amepeleka form one watoto wawili ana mifugo tuseme kama mbuzi arobainne na anataka kuuza ishirini Mogadashe haina soko sawa, kupeleka Isiolo anambiwa lete permit. Maskini ametoka reserve atatoa wapi permit hata hajui njia kwa hivyo tunataka yule mtu, ile jambo ama biashara anafanya iwe ya uhuru si ya lazima, iwe ya uhuru.

Pengine ingine upande ya shule. Tukisema shule nafikiri sisi yetu ni primary level tu. Yani tuseme watoto wetu hakuna mahali ingine wanaweza enda sijui hii tulifinywa. Hatuwezi kujua tunafinywa wapi. Tunataka upande wa masomo, Bwana commissioner, upande wa masomo hasa tunataka at least Kenya itu-lift tufanane na Kenya ingine kwa sababu hata we do not have workshops. Hatuna mahali watoto wanaweza kujifunza sanaa ya mikono iwe mechanics, woodworks, we do not have

them so tunataka Kenya ile Workshop ya Thika ama tuseme ya Nyeri iwe hapa Mogadashe ama Mogadashe Northernside kwa sababu shule ni sawa. Ministry ya education ile rules inaweka kwa katiba yake ni sawa kwa hii shule yote mbona ingine inafanyiwa inayo facilities ingine inanyimwa? So tunataka at least ministry of education itilie maanani hasa iangalie kwa kimacho upande wa Northern side asante yangu ni hayo tu (*clapping*)

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Siad. Asante kwa maoni yako. Sasa tumpate Mohammed Nur Rashid.

Kesi yote ambaye inahusu akina mama na watoto waislamu ipelekwe kwa kadhi, na kadhi wetu awe na nguvu ya kuhukumu vizuri kulingana na mafundisho na maamurisho ya kitabu ya Koran na (?). Kina mama wa kislamu ambao wanafanya kazi katika civil services wakiwa mwanamume akifa, bwana yake akifa, sheria ya kislamu inamuweka huyu mama katika nyumba kwa miezi nne na siku kumi. Si mapenzi yake ameamurishwa na dini yake akae hivyo nyumbani asitoketoke nje. Akikaa, tunapendekeza sheria iweze kumpatia huyu mama haki yake kama kweli tunatetea haki ya kina mama aweze kukaa na leave ya miezi nne siku kumi hiyo apewe leave na apewe mshahara yake kamili kamili.

Sisi tukiwa Waislamu, tumesema tumekuwa marginalised katika sehemu nyingi tanachukuliwa saa ingine kama second class citizens. Haya mafikira yaachwe, tuwe equal yani na Wakenya citizens wengine kama ni kupata passport tusije tukasumbuliwa na kutafuta vile inasemekana ma-certificate ya mababu na manyanya ambaye hata sijui hawakuwa na hiyo birth certificate utazitoa wapi mambo mengine mengi. Kama ni kipande, tupewe haki ya kipande vile Mkenya yeoyote. Leo sisi Uilete form ya birth certificate mpaka ujaze sijui security bond, sijui ujaze nini, sijui ujaze mambo mangapi. Tupewe haki haya ndugu za.. ili tunapendekeza, tuwe bila kusumbuliwa. Na kama upande ya kazi pia tupewe kazi kulingana, tusionekane kama sisi Waislamu tuwe tunakuwa marginalised tupate haki na tujione ya kwamba kweli sisi ni Wanakenya pekee. Itulinde vizuri tuwe na Constitution mpya itakayo tengenezwa mimi natoa pendelekozo yangu ya kwamba ionyeshe usawa. Usawa kabisa equality hakuna khabla kubwa imnyanyase khabla mdogo, wala hakuna dini ingine itanyanyasa dini ingine equality ioneerane yani usawa, idhihirishe usawa na pia idhihirishe haki ya dini katika hii Katiba mpya ambayo itakayoundwa.nikirudi kwa serikali, yaani structure ya serikali, napendekeza tuwe na ceremonial President, halafu tuwe na prime minister, na sisi kama waislamu tunapendekeza pia cheo kama ya Deputy Prime Minister hii si hata sisi tunafaa kupewa tu jamani na ma-ministers tupewe kulingana na idadi yetu ambayo tuko wangapi ya population ya kenya. leo utakuta nchi kama South Africa ambayo wako na karibu 1 million tu wako na karibu sijui ministers wangapi sisi naye tuangaliwe kulingana na population yetu tupewe haki katika civil services, katika post mzuri yani muhimu muhimu key posts.

**Com. Lethome:** Sasa sema dakika moja umalize tafadhalii.

Nafikiri yangu pia nataka kuongeza ya kwamba upande wa power ya President, executive power yake leo, rais anaweza kutoa yuko above the law. Hii power iwe reduced, asiwe above the law, na pia, asiweze kuwa na amri ya kutoa vita kutangaza war yeye peke yake. Vile itatangazwa isitangazwe na executive Rais peke yake hiyo ipelekwe katika assembly bunge ikalie kama ni vita itangaze na emmergency law ni namna hiyo. Na pia upande wa wakati wa kumchagua Rais awe over 45 years of age awe ni degree holder ama kama ni Prime Minister awe na good conduct iangaliwe moral na ethical vote qualification awe naye na the same iwe applied to the MPs na hiyo hiyo ethical na moral qualification iwe applied to the councillors. Parliament ikiwa kiongozi kama Rais akiweza kama imepatikana kama misuse of office kwake, ama kama amekuwa na corruption aina fulani, ama immorality aina fulani, parliament iwe na uwezo wa ku-vote vote of no confidence, ama ipatiwe haki ya impeachment, basi aweze kuondolewa. na asiwe, Rais asiwe na vitu ya kuzuia kitu parliament ambayo imepitisha, yeye azuie kwa vitu yake aikatae. Parliament wawe na uwezo. na mambo ya amendment ya laws, parliament isipewe uwezo, pendelekozo langu ni isipewe

uwezo kabisa ya kufanya ammendment yoyote ya sheria. Kama ni amendment ambayo inahusu hii Katiba, lazima irudishwe kwa wananchi ifanywe referendum ndio sisi tuweze kuamua tena kwa sababu Katiba wakati sisi tunatengeneza sisi ndio tunaitengeneza. na kama kutatokea mabadiliko lazima tuulizwe sisi mbele kwanza ndio iweze ipatikane hiyo mabadiliko. hiyo anayotaja sehemu ambayo inagusia mambo ya dini isiguswe kabisa, hiyo ni haki ya dini ya mtu na vile mola wake anapenda iachwe hivyo. Kwa haya machache nafikiri pia nasikia muda wangu umekwisha, sehemu yetu hii iangaliwe sana hali tupewe affirmative action sisi ni watu ambaye tunataka affirmative action, ni watu tumepata shida ni watu mifugo yao imemalizwa, ni watu tumepata taabu kubwa kubwa, hatuna maendeleo yoyote, hapa mabarabara ni mbovu, mashule hakuna, tunataka free education, tunataka tuangaliwe, tunataka mifugo yetu ipate soko, na haya mambo yote. Na pia wale walemavu wasiojiweza haki yao iangaliwe, Constitution ichunge haki yao, wawe wanatambulika na serikali iwasaide ili waweze kama mtu ana skills aina fulani, apewe support by the government, state ya support ili aweze kuendeleza maisha yake asionekane ye ye ni kipofu ama ni kiwete ama kiguu aachwe namna hii akihangai. Ni haki ni binadamu ana haki ya kulindwa. kwa haya machache nafikiri sijui nitamalizia hapa.

**Com. Lethome:** Asante sana shukrani. Hebu tumpate sasa Joseph Samath, catholic justice and peace commission Isiolo, yuko hapa? Joseph Samal karibu. Nilikuwa nimekuita mwanzo lakini ulikuwa hauko.

**Joseph Samal:** Okay. ni asante. Karibuni sana Commisioner na jamii ya modagashe yote, hamjambo? Nafikiri yangu ni kusisitiza tu maoni ya wale wengine sijaandika chochote ambacho lakini kuna watu ambao wamefanya kazi ya kuandika karatasi ya ku-present hapa. yangu ningependa kusisitiza kama kwa upande ya affirmative action to the pastoral communities. There is need for affirmative action ili tuwe na kind of redress to the social economic and political marginalisation of something that will address the social economic and political marginalisation of pastoral communities. Na hii ni kama kuanzisha things like the comprehensive national projects. There is need to address the issue of comprehensive national projects ili the pastoral communities wawe involved na iwe kupunguza ipunguze pia hali ya shida mbali mbali ambazo ziko kwa pastoralist communities.

Kuna jambo lingine tena ambalo ningependa kuongea that promote the justice and equality among the pastoral communities. imetajwa lakini ningependa kusisitiza ya kuwa ili tuweze kuondoa sheria ambazo zinanyanyasa kwa pastoral communities ni vizuri kuwe na kitu kama truth and reconciliation committees, commission. tukiwa na Truth and Reconciliation commission, tunaweza tukafutilia maneno mengine kama yale yamesemekana compensations za watu wakati ambapo wamekuwa wakitendewa maneno mengine mabaya mabaya enzi hizo kama ya ma-shifter. Kukawa na Commission kama hiyo tunaweza tukafutilia tunaweza tukafutilia na yawe yaweze kupatikana shida ilikuwa upande gani. kuliko kuwa na kitu kama anti-corruption unit na anti-corruption unit yenyewe tukafutilia inaweza ikawa na shida nyingi kuliko vile inaweza ikatatua. kwa sababu tukiangalia kati ya pastoral communities, kama sisi hapa kulingana na vile tumekuwa tukifundishwa watu unasikia watu waki-complain wakisema, sisi watu wetu walilipukiwa na bomb fulani, watu wetu sijui waliangukiwa na kisima wakati wakiwa wanachota maji nafikiri haya yote ni mambo ambayo yangeweza kuangaliwa na serikali hatunge poteza watu wetu kwa njia

hizo. Kwa sababu ukiangalia jeshi nyingi kutoka nje zinakuja kufanya mazoezi yao hapa na watu wetu ndio wanaumia.

Ukiangalia hali ya hizi tunasema resources,tukijua ni katika hali ya community sovereignty over natural resources. Ili vitu tukiangalia kama hapa tu karibu Bw. commissioner kuna mahali panaitwa Duse. Duse watu wanaumia kwa sababu kuna watu wanakuja kutoa hii inaitwa blue sulphur. Kuna blue sulphur watu wanakuja kutoa hapa na ukiangalia wale watu wanaishi hapa Duse wanaumia hakuna faida yoyote wanapata kulingana na wale wanakuja kufaidika hapo, mtu wa nje anakuja kufaidika. ingekuwa afadhali community ambayo inaishi hapo iweze kufaidika. Tukiangalia pia lodges zetu kuna watu wengi wana-invest katika hizi lodges ambazo ziko Isiolo. Hakuna community yoyote ambayo inafaidika katika resources kama hizo. tukiweza serikali ikiweza kuangalia iwe na sheria ambazo zina sisitiza vizuri ya kuwa ukienda ku-invest katika jamii fulani kuna percentage ili tunaita kuna percentage fulani ambayo inaenda kusaidia katika elimu, katika afya, hizo njia mbali mbali katika community ambayo inaishi hapo, nafikiri tutaweza kufaidika. Ningependa pia kutaja mambo ya registration. tuna vitu kama passport, tuna vitu kama registration of voters tuko na vitu kama registration of persons. Hizi zote ni vitu ambazo zinahusu jamii. Tukiwa na passports, ambazo zinapeanwa mahali kama Isiolo ama mahali ambapo watu wanaweza wakafikia, kila mtu anaweza akafikia, mtu kutoka hapa Modagashe hawezo akaenda Isiolo atafute pesa zingine tena za kwenda Nairobi. Akae miezi karibu tano, sita kabla kupewa passport, unakuta wengine hapa wamepoteza nafasi zao za elimu ya kwenda kusoma kule nje kwa sababu ya kucheleweshwa kupata passport. Ikipatikana hapa Isiolo, itakuwa rahisi. hizo sheria zote ambazo zinatumika mahali pengine huko ikiwekwa hata hapa Isiolo katika kupeana passport itakuwa rahisi sana hata sisi kuendelea na kuweza kuona huko nje, watoto wetu wanaweza kuona huko nje inakaa namna gani. itakuwa kazi rahisi.

Jambo lingine ni kama hiyo registration of voters it has to be continuous ni kitu ambayo ni continuous. Nafikiri iko records ambazo ziko ikiwa ni kufuatalia nani anaweza kujandikisha mara mbili ama tatu inaweza ikajionyesha kwa hiyo voters register. Kwa hivyo ni vizuri iwe continuous process tusiwe tunapewa muda wa siku mbili, miezi miwili, mwezi mmoja,tunaongezewa siku kumi na nne, itakuwa ni shida sana. Kwa sababu kuna watu amba wako huko ndani ndani nafikiri Bw. Commissioner atakubali kuna mahali hapa hata kulingana na hii njia ukifuata hata hapo umepita kuna mahali pengi huko ndani ndani watu wanaishi lakini hawajui hata serikali imekosa namna ya kufikisha magari pande hizo na hakuna hata njia ya kuweza kufikia watu ili tufanye registration ya hawa watu. Hapa hivi tunapoteza percentage kubwa ya watu amba wakati hata kura. Kwa hivyo ni muhimu iwe ni kitu continuous ili vijana amba wanahusika katika jamii hii iweze kuingia ingia. This I mean all pastoral communities. waweze kuingia huko wawafkie wale amba hawangeweza kukuja pahali ambapo imetengwa kuwa registration centre. Registration of persons pia, kama issuing of identity card. Issuing of identity cards unakuta tunakuja tunapigwa picha, tunajaza hizo forms zote, unaambiwa identity cards zimechelewa Nairobi. kama juzi tumekuwa tukifuata tunakuta, vitambulisho za wale watu amba wamekosa kukata kura hapa haziko Isiolo ziko Nairobi. Na hata kama ziko Isiolo, hakuna njia inaweza ikaenda Merti, hakuna vile inaweza kuja Modagashe, Siricho division, Garbatula ama Kina, inakuwa shida sana. Kwa hivyo ikiweza kuwa kitambulisho unatafuta na unapewa baada ya siku mbili, tatu ingekuwa rahisi ku-beat hizo deadline ambazo zilikuwa zimewekwa na electoral commission kwa kupata vitambulisho. Kuanzisha sustainable social welfare services, nafikiri tumechoka na relief food. Wakati tunapata relief food, tunakaa ni kama tumetosheka. Na tukishatosheka hivyo hakuna kufikiria maneno

mengine kama ya kujiendelesha sisi wenyewe.

Itakuwa vizuri kama serikali inaweza ikatuanzishia miradi zingine ambazo ziko hapa ndani na sisi na tunaweza tukajipatia nguvu. Kwa sababu hata Bibilia na nafikiri hata Koran inasema Mungu anasaidia mtu ambaye amejisaidia zaidi. Unajisaidia na Mungu anakuongezea nguvu unaenda zaidi. Tukianzishiwa vitu kama Kenya Meat Commission hapa, nafikiri watu hata wale pastoralists wangependa wale ambao wamekataa kuuza mifugo yao wataanza kuuza na wajue unaweza ukaweka mia moja ikifika mia moja hamsini unauzu hamsini unabaki na mia moja ingine. Hiyo itakuwa ni njia mzuri sana ya kuweza kusaidia hii jamii ya pastoralist communities.

Tumesema kitu ingine kama, mwisho kabisa ningesema appointments zote, appointment to kama ya parliamentary, una-appoint Mbunge. Wakati una-appoint mbunge nafikiri tunaangalia vitu nyingi. Hata Constituion yetu nafikiri imetaja ya kuwa wakati mtu anakuwa anawakilisha labda minority group fulani ama people of special categories, but this is not the case. there has to be, lazima tuisitize ya kuwa itafanyika hivyo iangaliwe vizuri kwa Constitution ni kitu ambaye itakuwa na ifuatiliwe vizuri vilivyo vilivyo. Kwa hivyo ni asante, sikuweza kuji-introduce, naitwa Samal co-ordinator wa justice and peace commision na tunajaribu kusaidia jamii kufanya kuwakilisha maoni. Asante sana.

**Com. Lethome:** Asante sana Samal. Tumpate sasa Abdi Haji Gonjove. Nilikuwa sijakusahau. kwa sababu tunakupenda tunataka kukaa na wewe zaidi

**Mr Abdi Haji:** Wananchi wapenzi wandugu yangu, yangu itakuwa....

**Com. Lethome:** Aanza na jina lako.

**Mr Abdi Haji:** Jina langu naitwa Abdi Hali Gonjove kutoka Siricho. Kwanza naomba hii Review Commission tunasikia mwaka yote hapa review commission bahati tumewakuta leo. Kenya hapa tukisikia iko mambo mengi sana. Tunasikia commission, commission, commission, hata education tunesikia, tunesikia nini, lakini kesho baada ya kutumia pesa mingi yetu ya serikali hakuna matokeo, inapotea. Naomba hii Commission hii ya constitution isipotee hii mambo (?) mimi naogopa Kenya, Africa hii inaweza tokea mambo mtu mmoja tu atokee na bunduki aseme mimi ni mkubwa nitakuwa President nasema kila ile kitu yote hakuna na hii ni sheria ni kitu muhimu na kitu inalinda sisi. Mimi naomba sana tafadhalii hii commission iwe si kitu kidogo tu namna hii namna hii halafu mtu mmoja tu aseme hakuna tutaendelea na ile ingine, au tufanye ile ya kimbavu, iwe ni kitu inaheshimika. Mimi, naunga mkono hii serikali ya majimbo, kwani hii majimbo watu wengi sana wamezungumza juu yake zaidi na nilifurahi zaidi sana kwa wenzangu, ambayo wametoa maoni tofauti tofauti na mzuri mzuri. kwangu sasa nikiendelea kwa ufupi, hii majimbo ukiangalia sana ni mambo ile inarudisha sisi mambo inarudi hapa shambani. I mean bottom inakuwa top na top inakuwa bottom. sisi tunataka mambo irudi namna hiyo, inanza na sisi hapa halafu wale watu wa Nairobi, iwe ni watu ya mwisho. Mahitaji yetu ni sisi tunajua ni nini na nini na nini inatufaa hapa. kwa hivyo majimbo ni

serikali ya hapa hapa hapa ambayo inaanzisha hapa, kama ile wengine wamesema juu ya local government, wamesema ipatiwe nguvu, na tena kidogo ndani nikisikia, wengine wanasema tunataka mtu awe na sijui masomo mengi, katika councilors na local government maana yake ni serikali ya hapa hapa ya wazee. Wacha hii mambo ya masomo na nini, bora mtu awe anajua Kiswahili na ni mtu yenyе hekima. na ni mtu anaheshimika, anaweza kuwa councilor, kwani ni nini councilor ni kitu gani? Iko kitu unafanya na ma-degree na mashamba na nini na nini, si kufunza tu mambo ya maendeleo hapa? Mimi na-support, hapa hii maneno ya local government, yejote anafahamika, anafahamu Kiswahili, anaweza kutuongoza. mtu yejote anajua kusoma Kiswahili na kuandika, atakuwa councilor, wacha hata masomo ya standard seven na eight, bora tu mtu awe ni mtu mzima, ana hekima, ni mtu miaka yake amehitimu, ...

**Com. Lethome:** Ana umri wa miaka ngapi?

**Mr Abdi Haji:** Arobaini.

**Com. Lethome:** Kuelekea juu.

**Mr Abdi Haji:** Na ingine hapa kidogo nitaongeza, ni hii mambo ya central hii tulikuwa tuki (?) hii mambo ya majimbo. Majimbo sisi tunataka, iwe tushikamane na watu wale tunafananana. Kama sisi Waborana sasa hapa, kuna Marsabit, Moyale, Isiolo, na hata Tana River ambaye tunafananana hata kwa lugha, na kwa kidini na mambo yote. Na kama inataka izidizwe zaidi, hata afadhali badala ya kushikanisha sisi hapa na wengine, Samburu afadhali hata tuongezwe moja. Au hata bado ikitaka zidi zaidi, Wasomali hapa wenzetu ambaye tuko dini moja, tukishikana nafikiri haina mbaya Kama labda governors, sehemu ile nataka ni nyingi labda ni district kama nane, au saba hivi na sisi tuko wachache, kama ni kuongeza tuongezewe watu kama Garissa, Wajir, na Mandera hivi badala ya kuweka sisi na watu kama Embu, na nini na Wameru hapa wale watu wameendelea zaidi kwa kisomo na kwa.. hata ni wale walitufinya, mimi nasema.

Mambo ya kipande, kipande mimi nasema, ningezungumza mengi lakini mambo yanu sio mengi points sasa mimi naweka ingine tu kidogo kidogo hapa, hatuna haja sisi tuwekwe na kipande, ya nini sisi nakuwa na kipande? Mimi najulikana ni mwanakenya, mtu wa Kenya. Kenya hapa, tuko na uhuru na tukae huru ya nini nawekwa hata nafungiwa karatasi nitembee naye kichwa yangu iwe nini najulikana. Mtu kama mgeni mgeni anajulikana na sisi yote. Ni sisi hata sasa hakuna mtu nachunga sisi. Sisi mwenyewe najichunga. Mtu mimi napendekeza hakuna haja ya kipande. Kipande ifutiliwe mbali kabisa kwetu. Sisi yule mtu anataka kuwa na passport akatembee inje awe na passport. Kama sio hivyo, hakuna haja ya kipande.

Maoni yangu, ingine naongeza, mambo ya dini ya Islamu. Mimi ningependa sana sisi, dini ya Islamu atuangalie dini ya Islamu ndio dini ile tunakaa nayo, na dini ile inatuongoza, na kiasi ile tunafahamu ni dini inatokana na hadithi ya mtume, na Quran tukufu. Vile mimi naonelea, hii mambo ya Kadhis, iwe ma-judge wetu wawe ni watu Waislamu kwa sababu, ukiangalia hapa Kenya, Sheikh amezungumza sana hapa, juu ya Kadhis na vile watachaguliwa, wawe chini ya Ulamaa, (?) Ulamaa amesema

ni mzuri, lakini hawa Kadhi, kama kweli sheria yote anapatiwa, mambo mengi sana hapa inakuwa, kama mchezo na ni mambo hatari hatari. Kama kunajisi msichana hapa, msichana mtu anafanya napatia mimba, hana haki, leo sheria hii ya Kenya, hakuna kitu nafanya lakini ukiangalia mfano moja dini ya Islamu nasema hiyo mtu apigwe kiboko mia moja. Kama ni kijana hakuolewa, hajaolewa. Au msichana ule hajaolewa, akifanya zinifu, akifanya kuzini, apigwe kiboko mia moja. Nafikiri mtu akipigwa public viboko mia moja, ingine hatakuwa mfano hapa ataogopa. Kwa mfano kama haya, sisi sheria yetu tunataka sheria ya Kislamu iwe ya Kadhi. Mambo mengi sana ukiangalia sana mwizi leo sheria ya Islamu anasema kama anaiba akatwe mkono. Na mwizi ingine ya ng'ombe hapa kama anakatwa moja mkono, hauna mtu ingine utaona mfano tena atarudia. Nafikiri dini ya Islamu itakuwa ni ya ajabu lakini itakuwa ni mfano ya moja. Na hii kwa ajili ya haya, tunataka dini ya Islamu, iwe sheria yetu hapa.

Nikiguzia hapa kidogo education, education kama vile tumbeki sana. Watu saa hii wengine kutoka asubuhi amezungumza mengi sana, Wanasema ati mtu asome, mtu asome, degree degree, hii degree, ni kusikia tunasikia hakuna degree hapa. Siricha division unaona hapa iko watu zaidi ya watu laki elfu hamsini au thelathini, ile kijana amezaliwa Isiolo district kutoka Siricha division, labda ni wawili au watatu, hakuna ingine. Hii ni vile tumbeki nyuma zaidi. Masomo yetu, kama vile watu wengi sana wamezungumza juu ya emergency hapa, tupatiwe free, miaka hii kumi na nne au kumi na tano, ingine hii sheria ikikuwa, au miaka ishirini, nimesema ishirini, ishirini tupatiwe miaka ishirini free kutoka nursery, mpaka university. Kwa masomo yangu ni haya.

Mahali ya security, okay mimi napinga polisi. Polisi ifutiliwe mbali. Kama ni security, watchmen wawekwe, mfano ukichukua Nairobi, Nairobi kila nyumba iko na watchman na hiyo watchman anajua ni nani mwizi hapo Nairobi kila mmoja. Mimi napenda hii mambo ya watchman wapatiwe power, wapatiwe nguvu wawe wakichunga, wizi na kila kitu.

Moja tu nitamaliza. Hii mambo ya administration. Watu wanasema administration namna hii namna hii, administration kweli, eh administration ukianzia president mpaka chini hapa, iko mambo mengi sana haswa kwa President. Nguvu mingi. Hata hizo zipunguzwe. Lakini hasa, wacha hii D.C. na D.O. hii watu nakula mshahara hapa, Kuna hii ingine naitwa chief na assistant cheif hapa, Hawa watu wako na jukumu kubwa zaidi zaidi zaidi. Kwangu mimi, kama hawa hawako, sisi hatungeishi hapa. Tukisema ukweli ya mambo, Machifu ndio macho hapa. Na ukienda hapa, sub-location kama Banda (?) utakuta walimu na Assistant chief pekee yake kwani iko ngapi? Idara yote iko na hakuna ile takaa huko. Hawa watu wawe, wapatiwe nguvu hata zaidi zaidi.

**Com. Lethome:** Malizia sasa mwalimu.

**Mr Abdi Haji:** Mwisho sasa. naguzia NGO kidogo. Kuna hii watu naitwa NGO hapa Kenya. Unaona kila miti ni NGO, NGO NGO. pesa mingi sana natoka nje, na hii pesa kazi yake sana utasikia mfano moja hapa Isiolo, iko karibu nane, saba hivi ambaye budget yake ukiangalia kwa mwaka ingine ni thirty to twenty million. Hii pesa ukiangalia, ukirudi kwa wananchi hata kazi hatupati ndani yake.

## **Com. Lethome: Pendekaza.**

**Mr Abdi Haji:** Mimi napendekeza serikali ichunguze sana mambo ya NGO ndani ndani zaidi. Hata kazi yao sana sana ni ya incitement badala ya maendeleo. Wachunguzwe zaidi.

**Com. Lethome:** Asante sana shukran.

**Mr Abdi Haji:** Asante sana. Na hiyo sheria, iwekwe kwa sheria.

**Com. Lethome:** Itawekwa inshallah.Ginani Ali.

**Jimnani Ali:** Asalaamu aleikhum walahi (?) wabarakate.

**Jimnani Ali.** Kwa majina naitwa Jimnani Ali Boru. Mimi pia ni kijana kutoka hapa Modagashe. Nafikiri maoni mengi sana yamesemekana na wazee, na wavijana na wanawake ambaye walikuwa mbele yangu, yangu itakuwa ni machache sana. Kwanza kabisa ningetaka kugusia utawala, yani governance. Kuhusu governance nafikiria nitapitia kidogo kile nimeadika kwa kizungu. The government should write clear Constitution that guarantees the citizen to supervise governance. Yani katika Katiba yetu ya Kenya, tungependa ama napendekeza serikali ama Katiba yetu mpya igusie kabisa ni vipi utawala itaendeshwa. Na hii utawala ni lazima pengine wananchi pia, wahusishwe. Hivi kwamba namaanisha, tukisema utawala, utawala isiwe ni serikali pekee yake, kutoka presidemt, mpaka kwa chief, assistant chief halafu iishie hapa. Lazima raia wa Kenya pia wajue ni vipi serikali hii yetu ya Kenya inawakilishwa. Na hii yote lazima tuwekewe katika Constitution.

Jambo lingine, jambo hilo tu la Constitution ya governance, a clear Constitution should be made to discipline those who are participating in corruption. Tukisema mambo ya governance, hapa Kenya kunakuwa na corruption, yani uvujaji wa pesa, uvujaji wa cheo, umekuwa ni kwa wingi sana. Lazima sheria mpya iongee juu ya uvujaji wa pesa, na pia tuseme cheo. Mfano unakuta mtu ni D.O. ama D.C. ama head of department katika district level ama provincial level, kunakuwanga na pesa ambazo ni budget allocation ya nchi hii. Pesa hii kwa kweli kabisa, hakuna mtu ana habari ikitoka kutoka donors mpaka tuseme budget allocation ya Kenya yote, hakuna mtu ako na habari. Ni heads of provincial administration may be heads of civil servants na President mwenyewe ndio wako na habari hiyo. Lazima raia wahuishwe na vipi pesa hii ambaye imetengewa hawa inatumika. Na hayo yote lazima tuwekewe katika Katiba yetu, yani kwa maoni yangu ili raia hawa ili raia hawa wajue pesa yao wanatumia aje.

Kuna haki moja ningetaka kuongea, na hii haki pengine watu wengi wamepitia ambayo ni basic right. Tunaambiwa katika Constitution ya Kenya, zamani kuna kitu inaitwa fundamental right. Constitution yetu ya zamani imetuandalia vizuri sana

wakasema kuna haki ya kutembea, haki ya nini, yani ile fundamental right yote, lakini je, haki hii ambayo imetengwa iko katika Katiba yetu ya Kenya, inafuatiliwa? Haifuatiliwi. Na hayo yote lazima katiba mpya, itengwe, yani tuseme tuwe na kitu kama Constitutional court. Kama kuna mtu ambaye anavunja haki yako, lazima kuwe na kortini ambaye, itafuatilia mambo haya. Ile mtu amevunja haki yako, lazima Constitutional court ifuatile. Hiyo pia inakuja katika judiciary. Judiciary pia watu wengi wameongea juu ya Kadhi's court. Moja tu ningegusia, court yetu ya Kadhi's court the other court pengine court nyingine tuna court ambayo inaitwa high court of appeal. Pengine kama jambo fulani ama judge fulani ame kuhukumu na hiyo hukuma hujakubali, hujaridhika naye, unaenda katika high court of appeal. Lakini sisi Waislamu, pengine kama hatujaridhika, na pengine trial hiyo ni wapi tunapeleka? tukienda katika High court of appeal, high court of appeal haiwezi husika na mambo ya dini. Lazima katika Constitution pia high court of appeal ya Kislamu pia tuwekewe. Hiyo ni maoni yangu.

Kurejelea parents' rights, nafikiri wazee wengi hapa, wamezaa watoto na wamewalea, na pengine watoto hawa ambao wamewalea walisoma vizuri wakapata kazi nzuri nzuri. Na tungependa, kuna vijana ama tuseme watoto ambao wanakuwa ni watoovu, ambaye pengine hawawezi wakaangalia familia yao, mzazi ni mkongwe kabisa, amemlia pesa yake yote, ng'ombe yake yote ameitumia kwa kumfunza huyu mtoto basi Katiba ya Kenya pia iangalie jambo hili kama kuna mtoto kama hiyo mzee unamkuta tunasema unahaki hapa Kenya lakini mtoto yake mwenyewe anamlemea hataki kumpatia chochote mzee anaumia hapo nyumbani. Lazima Katiba pia iliangalie jambo hilo wazee pia wasaidiwe hapo.

Pia hapa Kenya hii yetu kulikuwa na mambo mingi sana ya retirement, kuna mambo mingi sana ya retirement. Kuna wazee pengine mfano tuchukulie mzee anatoka hapa Modagashe, ama anatoka pale Ma-Commissioners pengine hawajaenda mahali inaitwa Gubatu. Ameserve katika serikali ya Kenya, miaka thelathini ama thelathini na tano pengine ni mwalimu, pengine ni mfanyi kazi ambaye anafanya kazi hapa ama Siricho ama Gubatu. Na huyu mzee, akimaliza ile service yakupatiana government, akienda retire, basi serikali hii yetu ya Kenya inamatatiza sana. Vipi inamatatiza? Retirement, pesa yake ambaye ni ya retirement hawezi akapewa. Akienda katika ofisi fulani,..

**Com. Lethome:** Naona badala ya kutoa mifano, ungependekeza. Kuna tatizo hili tutalitatua vipi katika sheria mpya tafadhalii.

**Jimnani Ali:** Tatizo kama hilo serikali pia sio serikali, Katiba yetu mpya lazima retired personnels pia waandikiwe pia katika Constitution haki yao pia iangaliwe.

Tukirejea mambo ya pasture rights pengine, sisi hapa kitu ambayo tunahusika naye sana ni ng'ombe na pengine ng'mbe yetu siku ya kiangazi ama jalali, kunakuwa na drought sana na hatuna mahali ya kupeleka ng'ombe yetu. Basi tungependa, serikali ituwekee Act fulani lazima ng'ombe wetu pia kwa sababu ni serikali imechukua hiyo jukumu, watuvekee pasture Act, ama rights, ng'ombe wetu pia siku ya jalali lazima serikali iwalishe. Na pastoral community lazima tuwekewe Act kama pengine mifugo yetu, kama ni mambo ya industries, hapa Modagashe pia, ama sehemu nyingine ya pastoral communities pia wanakaa, lazima serikali ifanye jitihada ama mpango ya kuinua yani hali ya watu as far as poverty is concerned. Act kama hiyo pia lazima

iwekwe katika Constitution.

**Com. Lethome:** Wind up please.

**Jimnani Ali:** La mwisho, si la mwisho, lakini nikimalizia pengine, kuna hii Ewaso Nyiro, kuna mto ambayo tunaita Ewaso Nyiro hapa. Pengine inapitia mahali mingi sana. Serikali lazima, pengine kwa maoni yangu, serikali ifanye juhudhi ama Katiba yetu mpya Commissioners wafanye juhudhi, kama maoni wapeleke, river yetu ya Ewaso Nyiro, pia ifanywe pia like Nile, Egypt Nile. Kuna, hapa Ewaso nyiro kuna catchment areas mingi sana unakuta Wakikuyu wanakata maji yao mahali fulani, Wameru mahali fulani, mpaka maji ambaye inatufukia sisi hapa, ambaye ni soul yetu, inakuwa ni kidogo sana. Katika Katiba yetu mpya, pia hii mambo ya Ewaso Nyiro, vile itakuwa permanent, serikali ijadiliane lazima tuwekewe act kama hiyo asanteni.

**Com. Lethome:** Asante. Mohammed Jarso, hayuko? Halafu Haoth Gonjove yuko? Haoth, utamfuata Mohammed.

**Mohammed Jarso:** Kwa jina ni Mohammed Jarso, Kutoka Siricho division.

**Mohammed Jarso:** Yangu ni kusema machache tu. Kwa sababu tumeachwa nyuma kabisa kwa ile sherehe ingine. Napendekeza sheria ya watu ya pande hii kwa vile tunahusika na livestock, tuangaliliwe kwa sababu sisi ni watu ya msituni, pamoja na mali yetu, ni watu ya msituni. Hakuna sheria yoyote ile imetengenezwa ama mbeleni, inahusisha watu ya ng'ombe ama watu ya nchi hii. Sheria ile imetuacha nyuma, napendekeza hii sheria ya sasa iangalilie sisi, aweke hata asheria ya livestock. Sheria ya livestock iwekwe kwa sababu sisi hakuna matumaini yoyote kushikana na watu wa down country. Wale watu iko na shamba, watoto yao wamesoma shule kubwa kubwa, shamba yao inatoka watoto yetu saa hii kuuliza majani chai ni mimea aina gani hawajui. Ukiwaliza sasa miti hii ni ngano inatoka kwa mimea gani, watoto wa pande hii hawajui. Kwa sababu tuko nyuma kabisa, mimea hiyo haitapatikana area hii. Mimi napendekeza, iwekwe Act ya watu wa ng'ombe, saa hii barabara mnaona, Bw. Commissioner ulitembelea hii barabara, hii ndio barabara inaunganisha sisi na wale Wakenya wameendelea. Watu wameongea hapa maneno ya university, mambo ya shule na kila kitu. Lakini ikiwa hali yetu, thirty nine years, hii Siricho, thirty Kilometres, unaenda six hours. Ama gari zile za relief tulipewa, iko saa hii ndani ya matope. Hatuoni kama maendeleo ile ingine tutapata lakini at least hii sheria mpya, iangalie sisi kwa barabara pia kwa livestock. Iwekwe act ya livestock. Sheria kama ile ya kahawa, ile ya sukari, kama hii kwa sheria mpya iwekwe ya livestock halafu ili sisi naye watu ya ng'ombe, tusiachwe nyuma kabisa. Tukisema tunalaumiana tumeachwa zamani nyuma, haina maana. Mambo hiyo imeenda, hatutakuta wale wengine, hiyo watu wameenda kabisa. Kwa hivyo Bw. Commissioner, naomba ama napendekeza sisi watu ya pande hii tuwekewe sheria ya livestock, livestock saa hii unaweza kuwa na ng'ombe yako, haikubaliwi kusafirishwa usiku. Inahesabiwa hiyo sasa ni kama bunduki. Nasemekana sheria ya Kenya haikubali ng'ombe kutembea usiku. Ng'ombe hii ukitoa hapa, uende ushukishe Isiolo, waizi watachukua. Wewe huna boma ya kuweka ile ng'ombe, Mwenye gari anataka kukuhesabia siku zingine extra, kwa hivyo nilikuwa naomba ama napendekeza, ng'ombe isafiri kama wale wanyama wengine usiku na mchana, ikiwa ni ng'ombe halali sio ya wizi.

Mambo ya retire, watu wameongea mambo ya retire. Kweli watu wakienda retire wanapata shida. Wewe umefanya kazi hapa, inasemekana haki yako iko Nairobi. Nairobi yenyewe wewe hujaona maisha yako, Sasa ukiwa retire, wewe ni mzee kabisa, ndio unaenda kutafuta haki yako Nairobi. Hukupata nafasi mbeleni ya kuishi Nairobi, hujui Nairobi ni wapi, huna pesa ya kuishi huko kupata ile haki. Napendekeza, kwa vile sasa serikali imeendelea iko na nguvu kabisa, iweke hata haki ya kila district iwekewe haki, wa-retire apate haki yao katika district level, ikiwa haitawezekana, kwa division kwa sababu serikali ya Kenya ina mpango ya kusema inalete maendeleo karibu kila mahali, imewekwa chief, D.O. kwa hivyo tunaomba hiyo watu ya retire ama napendekeza, wangepata haki yao hapa karibu karibu ndio wasiangamie huko Nairobi.

Mambo ingine watu wanasema, mambo ya local government, Bw. commissioner local government, kama tutasema form four, form four yetu, kama tunasema form four ni shida hatuwezi pata labda vijana, yote ya form four. Kuna wengine wamezaliwa na akili ya kuzaliwa, kabisa wanaweza kutetea wananchi ama Mungu amewapatia jukumu ya kuongoza. Sasa, bahati mbaya hakupata nafasi ya kwenda shule. Tukisema ni form four peke yake, basi wale naye haki yao itapotea. Kwa hivyo mimi nilikuwa napendekeza, bora tu mtu ajue kusoma na kuandika, haki yake isipotezwe, aongoze akipata nafasi ya kuongoza, kwa sababu kuna mpango ya kusema, sasa ikisemekana form four peke yake, wale hawajasoma watapoteza (?) napendekeza, watu wale wengine wanajua kusoma na kuandika waendelee tu kugombea wadhifa wa councillor. Yangu ni machache, nasema asante sana.

**Com. Lethome:** Haya asante. Haoth Gonjove.

**Haoth Gonjobe:** Asalamu aleikhum. Mimi nikianza nataka kuongea juu ya...

**Com. Lethome:** Majina tafadhali.

**Haoth Gonjobe:** Kwa majina naitwa Haoth Gonjove kutoka Siricho. Mimi nataka kuongea juu ya resource management. Nikisema resource management, nina maanisha ya kwamba all resources available in Kenya are in Nairobi today. Na kwa hayo, the only developed country ama developed towns in Kenya are only five or six. Kwa sababu ile resource kama industries, companies and cooperatives, inapatikana mahali ambapo Rais na mabunge wake wanakaa. Kwa mfano kama K.M.C. leo, ingekuwa ina-operate na inapatikana mahali kama Isiolo, I think Isiolo today is the same as Nairobi. But kwa maana vitu kama hivyo havipatikani, ndio maana leo tuko nyuma. All pastoralists ambao wanaishi na ng'ombe, wako nyuma. So mimi ninapendekeza ya kwamba the resource should be distributed in all towns not only Nairobi. Second, ama kuongea juu ya resource, ama nadhani kuwa today, yule mtu anakaa Nairobi anafamu Duse kuliko Siricho ama Garbatullah ama sehemu nyingine. Kwa sababu ako na interest ya kujua Duse lakini hana ile interest ya kujua ile pahali ingine. So ni lazima ya kwamba kila pahali, all resources should be distributed.

Nikiendelea, kukuja kwa livestock act, sisi wale ambao tunaishi na wanyama kama ng'ombe na mbuzi na kondoo, leo tunapatikana tuko nyuma lakini tukiona pahali hawa wanyama zinaishi, is over sixty percent or over seventy percent. Na lakini hiyo percentage haina maana. The other thirty or forty percent which is remaining, is more resourceful na ina maana zaidi kushinda ya sixty kwa sababu kama hakuna K.M.C. ya kwamba leo, canned beef inatolewa Botswana, na ile ya Kenya ambayo inapatikana haina maana. Hiyo pesa ya ku-import canned beef, ingeendeleza Isiolo na pahali ingine, kufikisha Nairobi. Basi napendekeza kwamba K.M.C. ifunguliwe, na iletwe karibu na wale wako na wanyama.

Next, nikienda kwa transport and communicatuion, ninaelewa ya kwamba leo huyu Commissioner ambaye yuko hapa, lazima ajue security ya pahali anaenda na ile transport. Ama the situation of the road. Na ameambiwa ya kwamba ile mahali iko na security, na njia sio mbaya ni Modagashe. na angeendelea mbele angeona zile mambo ziko huko. Kwa sababu tumechelewa asubuhi kujenga bridge, ili tuvuke na tukuje hapa. Na wale ambao wanatoka pahali kama Irisaboro, mnajua ya kwamba hawajafika leo hii pahali ambaye wana-contribute kwa hii division. Lakini wanabahati chief wao anakaa Siricho wanaishi Siricho leo amefika.

Haya third nikikuja kwa group rights. The Constitution should support youth groups, women groups and child rights. Kwa sababu youth groups wengi leo wameungana kwa kutokosa kazi. Na wakiungana pia hakuna usaidizi wanapata kutoka Constitution. So the government or the Constitution which is going on should support the youth groups and women groups. and the Constitution shoud also support the right of association and trade union.

Haya, nikiendelea nikuje kwa mambo ya Ewaso Nyiro. Ewaso Nyiro ni ile river ambaye iko kwa hii district na ambayo ni seasonal. Na the government should look ways of making permanent distribution of water to that river. Hata kama wakitoa pahali ingine ambaye kuna river ambaye ni permanent halafu hata hii seasonal river, ijaribu kuwa permanent na iwasaide sisi ambao tuko pande hii. Na nikiona mambo ya election process, ninaonelea kwamba the ballot box is more secret na ambaye ni mzuri kushinda mlolongo. I think that is the end of my (?) .

**Com. Lethome:** Ngoja kuna maswali. Kuhusu ballot box. Ungependelea ballot box iendelee kuwa vile ilivyo giza giza au ungependelea nini? Karibia hapa.

**Haoth Gonjobe:** Nikiongea kuhusu community yetu, unaona watu wanakaa kwa mlolongona na ambaye ile haki ambaye ungesimama nayo hapo, kuna bwana, kuna bibi na mtoto, na hiyo haki, kwa sababu unaogopa ile mtu yuko nyuma yako, huwezi kusimama kwa ile msitari unataka kwa sababu labda ukirudi nyumbani huko unaweza fukuzwa. So inamaanisha kwamba unasimama kwenye ile msitari ambaye bwana anataka.

**Com. Lethome:** Mlolongo imeisha siku hizi mama. Siku hizi tuko na secret ballot. Lakini nakuuliza ile ballot box yenywewe, unajua, ushaiona ballot box, vile iko? what colour is it? Is it transparent or not transparent?

**Haoth Gonjobe:** It is not transparent ? huwezi ona, secret.

**Com. Lethome:** Okay. Ile sanduku yenyewe, ungependelea iendelee kukaa hivo hivo ama iwe transparent? Kuna nchi zingine iko transparent. Ukiweka ndani unaona.

**Haoth Gonjobe:** Ikuwe transparent. Why, kwa nini ikuwe giza kwa sababu unatumbukiza karatasi huko ndani?

**Com. Lethome:** Aha. Sawa. Ngoja bado. Electoral commission of Kenya. Do you think it is independent as it is and if it is not in your opinion, what do you recommend?

**Haoth Gonjobe:** It is not independent now.

**Com. Lethome:** Why is it not independent?

**Haoth Gonjobe:** Si inategemea government.

**Com. Lethome:** Sasa unapendekeza kitu gani?

**Haoth Gonjobe:** To be independent on its own.

**Com. Lethome:** Haya ungependa ichaguliwe vipi na chairman wa commission hiyo achaguliwe vipi?

**Haoth Gonjobe:** Na raia.

**Com. Lethome:** Achaguliwe na raia. Haya ahsante sana. bona hukuzungumzia habari za hakiza kina mama?

**Haoth Gonjobe:** Si nimeongea.

**Com. Lethome:** Okay!nataka uzungumzie habari ya domestic violence.What do you recommend?

**Haoth Gonjobe:** It is bad. Domestic violence should not be there.

**Com. Lethome:** Suppose somebody is guilty of domestic violence, baba amepiga mama, ama wacha we put it the other way round. Mzee akikosa, mama amempiga. Mama achukuliwe hatua gani?

**Haoth Gonjobe:** They should go to councils of elders.

**Com. Lethome:** Hakuna kupelekwa kortini?

**Haoth Gonjobe:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Ni mambo ya nyumbani hiyo eh.

**Haoth Gonjobe:** Eeh.

**Com. Lethome:** Haya sawa.

**Haoth Gonjobe:** Iletwe karibu na wananchi.

**Com. Lethome:** Are you happy with the way the Kadhi is appointed?

**Haoth Gonjobe:** Now?

**Com. Lethome:** I am asking one person. Please, I am asking this lady here. Unafikiria vile anavyochaguliwa hivi sasa ni sawa?

**Haoth Gonjobe:** Si sawa.

**Com. Lethome:** Ungependa achaguliwe vipi?

**Haoth Gonjobe:** Kadhi achaguliwe na...

**Com. Lethome:** Let her talk please, she is being recorded there.

**Haoth Gonjobe:** The leaders of Muslim Islam should elect them.

**Com. Lethome:** So the Muslim leaders should be involved in the appointment of the Kadhis.

**Haoth Gonjove:** Yes.

**Com. Lethome:** Okay, today ukienda kwa Kadhi, kama hukuridhika na hukumu yake, unapeleka appeal kwa high court. Ungependekeza iendelee hivyo au ungependekeza kitu gani?

**Haoth Gonjobe:** The High Court ya Kadhi ya Islamu.

**Com. Lethome:** Kuwe na high court ya?

**Haoth Gonjobe:** Ya Waislamu.

**Com. Lethome:** Haya. Tafadhalini mtu akitoa maoni yake mwacheni atoe mwenyewe. Mmekosa kumwambia aseme nini. Do not put words into her mouth. Zahara Osman, yuko?

**Zahara Osman:** Ahsalaamu aleikhum. Mimi kwa jina naitwa Zahara Osman kutoka Siricho. Nataka kuongea juu ya participatory governance. Kwanza, nataka kuongea juu ya NGO's. Sisi hapa Kenya kuna NGO's wengi wako lakini hatuoni kazi yao. Kwa mfano (?) ya Isiolo wako wengi lakini wachache tu ndiyo wanakuja kwa location yetu kama Siricho division tuseme ni wachache tu wanafika, kusaidia wananchi lakini wengi wao wanaenda tu kukaa Isiolo. Sasa maoni yangu nataka, NGO's should be transparent and accountable in terms of activity. Maoni ingine, government to work with NGO's. Serikali washirikiane na NGO's. tatu, CBO's to be empowered. La nne, CBO's leaders to be elected by community. Nataka viongozi wa CBO's wachaguliwe na wananchi. Maoni yangu ni hayo machache tu. Asanteni. (*Clapping*)

**Com. Lethome:** Haya asante.Ibrahim Buke!

**Ibrahim Buke.** Kwa majina mimi naitwa Ibrahim Buke kutoka hii sehemu ya Siricho. Kwa maoni yangu, mimi nataka kuongea juu ya security, kitu ya kwanza ile mimi nataka kuongea juu ni security. Mimi napendekeza kwamba, the government has to provide the equal security to all citizens, especially sehemu ambayo hali ya usalama sio mzuri sana. Sehemu kama hii, sehemu kama hii yetu, wakati mwangi inakuwa sehemu mbaya kwa hali ya usalama. Kwa hivyo, badala ya kuweka askari, sehemu ambaye hakuna shida mingi sana, inafaa sehemu kama hii sasa, ikuwe na security officers wengi sana. Pia ningependelea kusema kwamba wakati mwangi, hata kama kuna askari, askari wakati ingine inakuwa wanakosana na wananchi hata pengine hawana hatia. Kwa hivyo napendekeza kwamba, tukue na ile ambayo tunaita nini, security committees, ambaye wanatambuliwa vizuri na serikali. Hawa watu wakue pengine wawe intermediary, wakue katikati ya wananchi na pia hii serikali, wakue katikati. Pengine kama ng'ombe inaibiwa, askari wakati mwininge wanakuja kushambulia, wananchi ambaye hawana hatia. Kwa hivyo, wakati kama hii sasa, kazi ya sasa hii security committee ndio inafanya hii kazi ambayo wanatambuliwa na serikali. Nikimaliza hiyo sasa, nitapitia tu ile ambayo imesemekana kama mfano hii land ownership.

Mambo ya Trustland, iwachiliwe kabisa ifutiliwe mbali. Na sehemu ama land iwe ya wananchi. Land iwe ya community ambayo

wanaishi hapo ndani. Hawa wawe wa-control hiyo sehemu mtu ingine asi-control hapo. Kitu ingine nitaongea juu ya local authority. Nikiongea juu ya local authority, kuna clerks na pia tuko na mayors. The mayors and the clerks to be elected by the wananchi. Sio mambo ya councillors wananchi wanafaa kuchagua hawa clerks na mayors. Na pia, napendekeza ya kwamba, huyu mayor na clerks, wanakaa hapo kwa ofisi kwa miaka miwili, kwa hivyo napendekeza hawa wakae mwaka tano kwa hiyo ofisi. Kwa sababu hiyo miaka mbili haitoshi vizuri. Wakae kwa ofisi miaka tano. Pia, ninataka hii nomination ya councillors isimamishwe. Badala yake, sehemu ya wards iongezwe badala ya hii nominated councillors wachaguliwe. Pengine hawa raia hawapendi, wacha wale watu raia watu wapenda waingie hapo. Mambo ingine ni sheria iwekwe, sheria ambaye unaweza kuuliza serikali, mambo ambaye imefanya watu. Mambo ya saa hii ama mambo ya zamani yote. Mambo ambayo imefanya zamani kunyanyasa watu wote. Sheria kama hiyo sasa iwekwe ili uweze kuuliza ama kupeleka kotini.

Ya mwisho, nitaongea juu ya haki ya hawa watu ambaye naitwa pastoralist community. Hii pastoralist community, ile kitu wanaishi nayo ni ng'ombe. Wanaishi na livestock. Hawana majani chai, hawana coffee, hawana vitu zingine na ile vitu wako nayo ni ng'ombe. Kwa hivyo, nataka sheria ambayo inasimamia hii livestock iwekwe. Tunasikia ya kwamba iko Coffee Act, tunasikia ya kwamba iko Tea Act, iko sugarcane act lakini hatujui kama hakuna mambo hii ya Livestock Act ambayo na hii maziwa ya ng'ombe, hakuna sheria inashugulika na nyama ya ng'ombe. Kwa hivyo sheria kama hii iwekwe ili ishughulikie hii nini hii community. Nafikiri nitamalizia hapo.

**Com. Lethome:** Tunashukuru sana, asante sana Ibrahim Buke. Najua kuna watu walikuwa wameenda kuswali nikapitia majina yao. Mimi najua sasa wamerudi. Wanaanza kuwa na wasiwasi wanaona kama nimewaonea. Sionei mtu ye yeyote mimi nawapenda nyote hapa. Nitarudia hayo majina wale walikuwa wameenda kuswali halafu sikuwaita. Mukhtar Abakula yuko hapa? Haya karibu. Nitawaita nyote hata kama ni saa sita ya usiku nyote tutakaa hapa, labda mnaogopa (?), iko (?) hapa?

**Response:** Hakuna.

**Com. Lethome:** Basi tutaendelea.

**Mukhtar Abakula :**Ahsante sana, mimi ni kwa jina, ninajulikana kama, Senior assistant chief, Modagashe South Mukhtar Abakula Halake. Langu la kwanza ni mambo ya Trustland. Mambo ya trustland. Trustland maana yake ni wale wamesahaulika. Nikifafanua kidogo na kiBorana, (in KiBorana) Mambo ya trustland, wale wamesahaulika, tumesahaulika katika Kenya. Tumekatwa kando na Wakenya wengine. Kenya wengine wameendelea, wameendelea na tumbaki nyuma. Tunataka hiyo mambo ya trustland, wachukuliwe kwetu. Watuwekee jina ya community land. Ardhi ambaye ako na watu. Ardhi ako na wenyewe. isikuwe wamesahaulika. Langu la pili, mambo ya soko. Nikisema soko, hatuna shamba hapa. Sio soko ya viazi, wala maharagwe, wala nyanya. Ni soko ya ng'ombe wetu tunafuga. Katika Kenya, pahali inafuga, ni wale wanatafuta ndio wanafuga mifugo. Wale wengine, hawana mambo ya mifugo. Na katika Kenya, mifugo yetu kwa leo hii hawana dhamana yoyote, katika

Kenya. Kama ingekuwa na dhamana, K.M.C. ingekuwa Isiolo, au Garissa, au Mandera au Wajir au Moyale au Siricho. Hainingkuwa Athi River ambaye ni Machakos ni wale hata hawajui mambo ya ng'ombe. ama mbuzi. Na kwa leo hii, hatuna dalili ya mifugo yetu. Tukipeleka soko, tunapeleka soko mpaka K.M.C ambaye ni Athi River. Na kutoka siku ile tunatoka

(?) mpaka Athi River tutachukua mwezi mzima. Naikifika kule, ile ng"ombe ilikuwa umeondoa kwa boma, ambaye amepata shida, ya kuumizwa na njaa, kuhara imekonda. Na hakuna bei yoyote. Unatupa, unarudi. Unarudi wapi, unarudi hapa Eastleigh unalala lodging, ingine hapa ya wenyewe, unakutana na msichana mrembo hapo,(Laughter) ile pesa ile yote, ulikuwa na shida, ulikuwa na shida ndio unaenda kuuza, inakuja kupotea potea hapa. leo hii, iko na ugonjwa mbaya. Iko na ugonjwa mbaya hatari, na soko inapelekwa AthiRiver K.M.C. Na soko, kwa nini isikuwe hapa Isiolo, ama Siricho? Tunaenda unadanganywa na wasichana ya wenyewe huko, tunapatia mali yote tunarudi bila. Hata hiyo ni soko ingine kama hata hajajua. Hiyo ni soko ingine, soko ya viazi iko, soko ya mambo yote iko, tunawacha pesa yetu yote huko. Kurudi ni mkono tupu. Tunataka soko ifunguliwe hapa Isiolo K.M.C. ikuwe Isiolo ama Marsabit. Tunataka ikue karibu na sisi.

Kidogo, mambo ile ya Trustland, leo hii hapa D.C. inasemekana iko na wazungu ingine hapo na Muhindi ingine. Hiyo muhindi amezaliwa ng'ambo, hakuna muhindi ya Kenya. hatujawahi kusikia. Ni muzungu wa ng'ambo ndio leo hii anasikika kuliko watu wa Trustland wale wamesahaulika ndio wako na dhamana zaidi kuliko watu ya trustlands.Ambaye ni sisi. Wazungu wahindi ndio leo ako na dhamana kushinda sisi. Ndio intambulika ndio inapatiwa (?). Hiyo tunataka inudi mikononi mwetu.

**Com. Lethome:** (?) ni nini hatujajua ni nini?

**Mukhtar Abakula :** (?) ni ardhi ingine hapa katika Isiolo katika hapa ni Kina division, ambaye imepatikana na (?) dhahabu, dhahabu ambayo inaitwa (?)ndio imepatikana, ndio tumenyang'anywa, tumenyanyaswa, tumeigwa, tumeigwa, ndio napatiwa muhindi. Mambo ya boundary, mambo yote imeongewa na watu wale walikuwa wameongea mbele yetu lakini, tutapitia pitia tu. Mambo ya boundaries ifanywe kama zamani wakoloni wamewека. Koloni wakati wamewека, kila siku wanachunga, na serikali ya wakati huo wanapitia boundaries Wajir anachunga zake, Garissa anachunga zake, Isiolo anachunga zake, wanalindwa namna hiyo. Serikali yetu ilinde mipaka yetu namna hiyo.

Mambo ya majimbo. Mambo ya majimbo, nikisema kweli, hii mambo sisi hatujafamu zaidi. Kwanza kitu ya kwanza, tungeelimisha watu, sio ati sisi watu mia moja ama watu ingine watu ishirini ndio wamejua ndio hiyo kesho itakuwa ndio inaendelea. Ingepatiwa muda, watu wajue ni nini.

**Com. Lethome:** Senior Chief, Maliza maliza.

**Mukhtar Abakula :** Nitamaliza kidogo.Nitamaliza.mambo ya majimbo inafaa kujulishwa watu zaidi kinaganaga. Sio wale tu wale wanakaribia hapo mbele ya power ndio wajue halafu, ndio hiyo ikuwe sheria na wengine bado hawajajua ni haki yao. Mambo ya NGO. NGO kweli tunaona inatusaidia hapa, hapa tumeipenda lakini kuna kitu sisi tumeshangaa. Zamani wanasema

serikali ndio inapakua pesa ya wananchi. Lakini kile tumeshangaa, NGO mtu akiajiriwa leo, baada ya miezi tatu ama miezi nne, hata sijui vile huyu mtu ako. Ako na gari yake, ako na mali yake, kama hajapokonya, amepata wapi hiyo pesa? Hata kama ameomba ng'ambo, imekuwa ya wananchi.

**Com. Lethome:** Ungependekeza nini Chief?

**Mukhtar Abakula :** Nimependekeza NGO, kwanza ikiingia Kenya, lazima imeaandikishana na serikali, authority ya kuingia hapa kukaa muda fulani katika Kenya. Na ikiandikishwa namna hiyo, watachagua, district fulani ndio wataenda kufanya kazi. Wakienda kuchagua hiyo district, kama Isiolo mfano, saa hii tukianza na hii yetu ya Action Aid, wafanyi kazi yote ni vijana ya Waborana. Sisi tumeshangaa ni nani ameajiri hiyo hapo. Sijui kama ni bunge, sijui kama ni councillor, sijui kama ni chief, tunaona tu mtu anaajiriwa inapita na inakuachia vumbi hapo, ati ye ye ni mtu wa NGO, tunataka, hiyo NGO iajiriwe na wananchi. Pili, asipoteze pesa ya wenyewe, wachunge vizuri. Mimi nafikiri yangu nitafikisha hapo. Ile nimesahau, itapitiwa na wenzangu.wale wamebaki. Asanteni.

**Com. Lethome:** Asante sana Senior Assistant Chief. Kuna Maulit A. Moi. Najaribu kupitia wale walikuwa msikitini saa zile. Abdi Aziz Hussein, sasa huyu tunapita kabisa. Huyu atatupata Garbatula akitaka. Mohammed Galgalo, Huyo mwambie atukute Garbatula pia. Hawa ni wale walikuwa msikitini.Kuna yule amekuja kuniambia saa zile alikuwa msikitini. Jina lako nani. Njoo. Ulikuwa umejandikisha hapa?

**Ibrahim Abdel Kader:** Asante Bwana commissioner, mimi naitwa Ibrahim Abdel Kader. Ni mtoto wa hapa Modagashe. Pendelezo yangu ni kwamba, kwanza nitazungumzia juu ya uchumi. Watu wa North Eastern ama watu wa pande hii Boran communities wanategemea the backbone of the economy wanategemea, livestock. Kwa hivyo, ningependelea serikali, ningependekeza ya kwamba serikali, iko na nguvu ni kwa vile nadhani haitaki, serikali iko na nguvu kutafutia market soko ya nje hata sio ya ndani. Na nasikia watu wanaongea juu ya soko, wangetafuta soko ya nje Kwa sababu unaona nchi zingine wanaauza mifugo yao nje for example nchi zingine wanaauza mifugo wanatafutiwa market kwa hivyo ningeomba serikali yetu kuu itutafutie. Commission iundwe ambaye itaangalia hali ya uchumi wa upande huu. Kamati iundwe, ambayo kwa sababu serikali iko na nguvu ya kufanya hivyo. Watu fulani waundwe, waende watafutie market, ng'ombe mbuzi, ili tuweze kuinuka. Hali yetu ya uchumi iweze kuinuka. Kwa sababu yenye hapa, wakati tunapeleka ng'ombe yetu Nairobi, kuna mambo mengi inaulizwa. Wacha nje, hapa just within Kenya kuna restriction mingi ambazo hizo restrictions kulingana na mimi, ni zile colonial systems, zile sheria ambazo wakoloni waliacha ndio bado inaendelea. Na kwa hivyo, ningependekeza kwamba hizo sheria, watu wakae chini waunde kamati amba watafikiria ile ya ku-change hizo colonial systems kwa vile huwezi kupeleka mbuzi yako Nairobi, kuna a lot of restrictions. Na hizo restrictions zimewekwa na colonial systems, ile ya zamani. Waafrika bado wanatumia zile sheria tu. Kwa hivyo tutafutiwe market, soko ya kuuza vitu yetu nje, hata nchi kama ya jirani Somalia, wanapeleka vitu zao nje, Saudi Arabia, Yemen, kila mahali, mbona isikuwe Kenya, ambaye ni stable country? Na kwa vile naona sasa serikali ya Kenya imeanza kujifungua, zamani tulikuwa tumefungiwa mlango, sasa naona serikali imeanza kujifungua, kufungua mlango kwa upande

wa Northerners, Northerners in general.

Kwa hivyo, yangu ya pili niwache mabo ya uchumi, niende kwa security. Kuna hii mambo ya operation, jeshi wanaletwa hapa, wanapiga watu vile wanataka, na hakuna mtu ambaye anaweza kuwafuata. Kwa hivyo, ningependa, ningependekeza ya kwamba, mtu yejote akiwa jeshi au polisi akupige, kuwe na kamati fulani iundwe, ambaye inaweza kwenda kushitaki. Kwa sababu ukienda kwa polisi unaenda tu kuwapelekea ile lawama kwao tu, na hiyo kitu haitafika mahali, watalalia. Kwa hivyo ningependekeza, kuwe na hata wazee amba, kuna ofisi iundwe, kamati ya watu, iundwe unapeleka lawama yako huko, halafu huyo askari anaweza kushikwa. Excessive use of force, by military should be abolished. Asanteni.

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Abdel Kader. Iskhak Abadala. Karibu. Resident of which country?

**Com. Lethome:** Karibu. Karibu bwana.

**Ishak Abadalla:** Habari zenu. Asalaam Aleikhum. Yangu mimi naitwa Abadalla, natoka Siricho. Mimi nikigusia kidogo, ya kwanza, nataka kugusia juu ya structure ya government. Hii serikali yetu, kuna hii serikali ambayo ni ya bunge, Executive, Legislative na judiciary. Kile iko mbaya zaidi ni bunge yetu ambaye tulichagua, hawana uwezo. Tulichagua, lakini kufika huko juu hawana uwezo hata kuandikisha bills au Katiba fulani ya kuitisha kwa sababu ile executives ambayo ile serikali inakalia, inakataa kuweka sahihi. Na the same executives ana-appoint, judiciary yani judges. Na hii judiciary ingekuwa independent body lakini ubaya imechaguliwa na nani?, Na Rais. Sasa wataimba wimbo ya nani?, Wimbo ya Rais. Kwa hivyo mimi natoa maoni yangu ya kusema kwamba, executives, yani judiciary, iwe independent body ambayo inafanya elected by who? By the parliament, hapana ni wabunge. si Rais peke yake akae chini halafu apitishe. By bunge, wabunge wapitishe waseme hii ndio judge yetu.

Nikiongea mambo ya local government, serikali yetu, serikali kuna central govrnment, kuna local government na central government. Hii serikali ya central government, hii serikali ya Nairobi imetu haribu. Kwa sababu wanafanya mpango, mpango wao yote iko Nairobi juu. Sisi wananchi wa hapa, tunetaka hii local government, communities should be empowered. Sasa, kuhusu mambo ya chairmen, kura ya chairman, ichaguliwe na wananchi, sio council, kwa sababu hii mtu anawakilisha sehemu kubwa division mzima, sio ambaye na chaguliwa by the councillors. Nikirudi upande ya, mambo ya educational, hii curriculum, hii mafundisho ambayo inafundishwa, syllabus ambayo inafundishwa sisi, ni mambo ya coffee, mambo ya kahawa, hakuna mambo ya ng'ombe inazungumzwa juu. Hakuna mambo ya ng'ombe mbuzi, zile ambazo tunaendesha. Tunataka hii curriculum ambaye inafundisha watoto wetu, iwe inahusika na mambo ya uchumi wetu hapa, mambo ya mifugo, mambo ya ugonjwa ya ng'ombe, mbuzi na kadhalika. Na pia, upande ya adult education, the curriculum should be well designed. Hii masomo ya gumbaru tunafundisha ya watu wazima pia ni curriculum ambaye inahusu mambo ya kahawa, mambo ya kulima, mambo ya kuku, ufugaji wa kuku, ufugaji ya kahawa, sio ufugaji ya ng'ombe.

Nikirudi upande ya mambo ya government, hii pia kuna hii serikali ambaye inaundwa kutoka P.C. provincial administration, hii ndio serikali ambayo imesumbua wananchi. Sasa kwa sababu wana-sideline upande gani? Wana-sideline upande ya government. They are not for the civil society. Hawapigani haki ya wananchi. Kila wakati wako upande gani? Upande ya central government. Wakitoa maoni mzuri                    (?) unaambiwa wee kaa chini kwa sababu kuna chief ambaye amefutwa kazi, kwa ajili ya kwenda kwa harambee ya ya mwana siasa, opposition party. Sasa.(laughter)

**Com. Lethome:** Pendekeza, pendekeza.

**Ishak Abadalla:**                    (?) Kwa sababu hii watu ni                    (?) ambayo imeundwa na colonial government. Hii ni kunyanyasa wananchi.Hii post ya chief na assistant chief, hii post ambayo imeundwa na serikali ya koloni ni kunyanyasa wananchi. hii ni (?) wakati ya koloni. Kwa hivyo hii watu nataka kuwa cut off kwa sababu ni ya colonial. Inafaa, serikali ya council of elders, council of elders iundwe, ili wananchi waendeshe kazi yao kwa njia mzuri. Na nikigusia mambo ya national dress, tunakidharau hiyo kifaa. Hakuna dini inakubali uende uchi kwa sababu hata kama kuna uhuru ya kutembea. au uhuru ya kuvaah (?) sisi tunapendelea national dress, mavazi mzuri.hapana kamisi ambayo tunavaa, mchana official, tutembelee, kwa mfano uki visit Nigeria, unaona mavazi ile wanavaa ni ile natinal dress mzuri.ya waislamu lakini Kenya, huwezi kubaliwa hata kuvaah kamisi utembee vile unataka.

**Com. Lethome:** Sasa tupatia nini pendekezo lako la vazi.

**Ishak Abadalla: Abagala:** Vazi nataka pendekezo la vazi, sasa mini-skirt hii itupiliwe mbali.

**Com. Lethome:** Na mtu akipatikana nayo afanywe nini?

**Ishak Abadalla:** Achukuliwe hatua.

Na nataka hiyo national dress, ile ya Islamu ikubaliwe. Mtu avae kofia, avae kamisi yake atembee huru vile anataka.

**Com. Lethome:** Na unajua kamisi kwa kiswahili ni nini?

**Ishak Abadalla:** Kanzu.

**Com. Lethome:** Sema kanzu. Ukitsemka kamisi kwa kiswahili utaleta mambo mengine.(laughter)

Kamisi ni nguo ya akina mama ya ndani.

**Ishak Abadalla: Abagala:** Kwa hayo machache yangu naiachia hapo.

**Com. Lethome:** Haya asante. Ali Kofi, Ali Kofi. Na kama kuna mama yeoyote ambaye anataka kuzungumza alete jina lake. Ali Kofi hayuko? Tumpate Osman Ibrahim, Osman Ibrahim! Hassan Shallo, Hassan G. Shallo kutoka Waso Trustlandproject.

**Hassan G. Shallo:** Ahsalaamu Aleikhum Wabarakate.

**Com. Lethome:** Aleikhum salaam.

**Hassan G. Shallo:** Ya kwanza nashukuru Bwana Commissioner Ibrahim, kwa kuchukua hii nafasi yake na kufanya juhudi ya kuweza kufika katika hii jangwa. Nina hakika ingawa Commissioners wote imesemekana watazunguka katika sehemu zote za Kenya, lakini sio wote wanaweza kujitokeza katika sehemu kama hii ambayo ina mambo zake nyingi. Lakini Ibrahim, kwa sababu ametoka katika watu ambao wamejitaja hapa kutoka leo asubuhi kama mfugaji na pia muislamu ambaye yuko katika ile hali ya kunyanyaswa anajua kwamba sisi ni watu yake na alifanya juhudi kutoka hapo pote akaja. Na tumeambiwa nikiwa Isiolo wakati fulani na Commissioners ya kwamba kila sehemu katika (?) constituencies watatembelewa na commissioner watatu. Lakini tunaona tu Ibrahim amejileta kwa hivyo tunashukuru. Sasa Bw. Ibrahim unaona mara kwa mara yale yamezungumziwa hapa yanafanana. Sisi tukiwa wafugaji, hatuzungumzi katika zile siasa kubwa kubwa, zile structures zingine za Kenya. Ingawa tunapendelea kuzungumza lakini ile hofu tuko nayo ama ile shida inatukumba inatuelekeza tu... kwa sababu hii ni fursa yetu leo na lazima tutazungumzia yetu, na wale watu ambao wako na nafasi ya kuweza kuzungumzia zile zingine itatutosha kutusaidia. Kwa hivyo, mara zingine kwa hizo madakika zako mara ingine unaona watu wanazungumza wakapita mpaka. Hii ni kwa sababu ya ile shida ambayo imekumba watu na watu leo wameweza kupata fursa ya kupumua kwa hivyo utatusamehe.

**Com. Lethome:** Sawa sawa.

**Hassan G. Shallo:** Ya kwanza, mimi ningetaka kuzungumza katika hali tatu ya kibinadamu ambaye hiyo sifa zinagawanyika kwa wanadamu. Ya kwanza ni hali ya politics. Uongozi ya uongozi, ya pili ni hali ya kuishi ya kijamii ambaye ni social na ya tatu ni hali ya uchumi. Hizo ndio maisha ya kibinadamu wanaishi katika hizi hali. Sasa, nikiguzia kidogo juu ya political, cha kwanza tumesema, mimi nasema yani nikitoa rai yangu, President iwe ile ya hali Tuwe na Prime minister ambaye yuko na nguvu kwa serikali na President iwe ni ile ya kawaida. Katika parliament, nasema ya kwamba kwa sababu tunataka mambo iwe transparent na katika Kenya watu hawawezi kuaminiana mtu yeoyote unampa jukumu, ile jukumu anajichukulia tu bila kujali wale watu ambaye wanampeleka. Kwa hivyo hakuna kuaminiana na hii kwa hivyo tunafanya kila mmoja achunge mwenzake kwa hivyo tunafikiria ya kwamba parliament iwe na Lower House, na Upper house kama ya zamani ili wana-parliament wakipitisha mambo, senate pia iangaliwe na kuthibitisha. Halafu ije regional kwa sababu wazee wengi sana wamesema wanataka serikali ya majimbo tuwe na regional assembly ambaye kwa hali za hiyo majimbo wanajua ya kwamba wataongea na kupeleka mashida zao mbele katika natioanl government. Sasa kwa sababu wajumbe wamechukua jukumu zote za nchi na kufanya mapendekezo vile wanavyotaka, lakini kama kutakuwa na hii kikao kingine kama ya regional assembly na senate basi ile hali yao, kama ilivyotokea hivi majuzi wanajipitishia shilingi milioni moja– salary kwa mwezi, wakati waalimu, madaktari na

wale watu ambaye wanatufanya huduma mzuri hawakuweza kupata kuongezewa hata shilingi elfu moja. Kwa hivyo, ili pia hawa wasinyanyase sisi kiuchumi lazima kutakuwa na fursa za regional assemblies mbili tatu ambaye za kuchunga mpango zao.

Halafu tunasema ya kwamba county council serikali ya mitaa ipewe nguvu. Na serikali ya mitaa ikipewa nguvu iwe ministry zote za serikali ikiwa ni eucation, agriculture, water na zote amazo unaweza kuzitaja ziwe chini ya county council na county council imange hizo mambo. Lakini ile technical assistance kwa sababu hao ndio professionals wataendelea kusaidia sisi. Lakini ile pesa wanazipata zote ziwe zitagawanywa na county council kulingana na lie miradi zimepangiwa. Nasema hivyo kwa sababu Kenya inapata shilingi bilioni mia tatu kwa mwaka lakini kwa sababu ya upungufu ya kiserikali na management ambazo ziko katika idara sisi tukiwa watu ya Isiolo hatukuwa tukipata maendeleo zote ingawa planning zinafanywa, hakuna dip moja zimetengenezwa katika hii sehemu na serikali ingawa hizo pesa zimegawanyiwa katika district zote. Kwa hivyo hizo zote tumesema ya kwamba ingawa kunasemekana kuna kitu inaitwa District Development Committee wananchi wenyewe hawakuwako ndani na wale iko ndani ni mawajumbe na sijui chairman wa council na D.C ndio ma-chairman. Haya kuna hii ingine DEB, wale wale tu ndio wanakuwa ndani, ndio

(?) district security board district na hayo yote inatufanya sisi tukae katika shida. Kwa hivyo, kitu cha kwanza hata wajumbe wasikue na madaraka zingine. Madaraka yake iwe ni mjumbe ikiwa ni district development committee iwe ni mtu mwingine. Ikiwa ni district mambo zozote ambayo district education board iwe ni mtu mwingine. Ikiwa mtu ni mjumbe asiongezewe madaraka ingine kwa sababu ya madaraka nyingi ambazo wanazibeba hawakuweza kutekeleza hata moja yao. Kwa hivyo, hata President baada ya yeye kuweza kuchaguliwa wakati anapata President ile kazi ingine anastaafu kama speaker, yani speaker hapa Kenya akipata ile kazi ya speaker anaacha ile kazi. Kwa hivyo, hizo madaraka lazima iwe na vile wazee wamesema, chairman wa county council awe akichaguliwa na wananchi.

Na kuna shida zingine ambazo zina                          (?) kwa sababu hii nchi inainuka hali ya mambo zinabadilika na tunafikiria mambo ya municipal council kwa sababu hii zimeanza kukataliwa katika sehemu zetu zingine na hii ndio vile mji inaweza kuendelea. Sasa mji huu Isiolo kwa muda mrefu umekaa ni mji ambao imekaa karibu miaka mia mbele ya ingine lakini mpaka sasa inakuwa county council kwa sababu viongozi wetu hawataki ipate hiyo mamlaka ya municipality kwa sababu hao wenyewe wenye kuchaguliwa ndio wanafaidika na hiyo mji. Kwa hivyo, mambo ya municipality lazima ipangwe na utaratibu ya kwamba kiasi fulani ya pesa ikipatikana kwa council inapata madaraka inaingia municipality halafu council zina                          (?) na sehemu kama hii                          (?) Modagashe pengine inaweza kupata kitu inaitwa area council halafu pesa zitagawanywa katika hizo mipango.

Serikali ya ndani. Serikali ya local government lazima igawe pesa zingine kwa county council kwa sababu ardhi sabini na tano kwa mia za Kenya zimetoka katika arid lands yani pastoralist communities ndio wamepeana hizo pesa zao na ardhi na pesa za kigeni nyingi zinapatikana kutoka ministry of tourism, lakini sisi wafugaji hatufaidiki na hizo pesa.

Kwa hivyo, pesa za ministry of tourism ambazo zimepatikana kutoka wanyama, na wanyama wametoka katika nchi za wafugaji lazima sisi tugawanyiwe. Tax ambazo zinatolewa katika sehemu zingine kwa mambo zingine ya national ikiwa

zinapatikana kama KPA Kenya Ports Authority Kenya Railways, Kenya nini,hizo vitu ambazo zinajumuisha wananchi yote ikiwa zinakuja regional, hizo pesa zigawanyiwe kwa ile faida ambazo zinapatikana zipatikane kwa ma-regions zote.

Halafu, tukuju katika uchumi sasa, sisi tukiwa uchumi ya kwanza ni, tuko na resources. Resources zetu ni maji, minerals, wildlife land na hata human being pia ni resource. Wanadamu pia ni resource ikiwa tunapata elimu , tunapata nini, na wanyama hawa yote ambao tuko na game reserve lazima hiyo resource zetu zingine iwe na faida na sisi na zile ardhi ambazo zimefanywa kando kwa mifugo ya wanyama lazima faida zake zipatikane kwa wale wafugaji. Hizo ni ya kufanya ya kwamba, ile mbuga ya wanyama yote irudi kwa mkono ya wafugaji, wananchi, communal conservations, sisi kwa sababu tume-trust ardhi yetu kwa county council, na County Council imetumia hiyo kiholela holela mpaka sisi tumeadhirika na mpaka sisi tukawa fukala na kunasa kutoka katika famine relief kwa miaka arobainne. Kwa hivyo njia ya sisi kutoka katika hali ya shida ni sisi tuwai hiyo resources zetu kama vile dhahabu mpaka hata petroli zimepatikana katika sehemu za Merti lakini kwa sababu sisi hatukuhusishwa kisha baada ya watu wale waliotengeneza walichimba hiyo kitu baada ya kuharibu mazingara zetu yote na miti walileta matrakta na kuharibu kisha tukaambiwa walijiondoa mara moja. Sasa tukabaki na hasara ya hiyo mazingara yote .Hiyo yote kwa sababu hii serikali ambayo tuko nayo hawahuishi wananchi katika hali zote za kiuchumi Kwa hivyo tukiwa katika leadership,sisi hapa tuko na parastatals karibu mia moja na katika hii sehemu sisi hakuna.

**Com. Lethome:** Tafadhali, tafadhali maliza.

**Hassan Shalo:** Haya hatuko katika parastatals, katika board of directors lakini nyingi ya hizo vitu si ati kwa sababu ya serikali peke yake, kwa sababu ya leadership ambaye hawakufanya lobbying kwa sababu mahali kama hii commissions sisi pia tuko na wasomi hata katika hii baraza tunakaa tuna karibu watu tano ambao ni graduates ambao wanaweza kukaa katika commissions kama hii ,ambao wangeweza kuingia katika K.E.C Electoral Comission. Hapo ndipo mahali pazuri ya kufikiria leadership kwa hivyo nitafikiria, halafu watu wengine (?) affirmative action hiyo, ni maneno ya ukweli kabisa kwasababu hali zetu sisi tumenyanyaswa kiuchumi na serikali ya ukoloni na serikali ya Kenya zaidi zaidi wakati waliweka sisi katika concentration camp na sisi tumewekwa ,tunasema ya kwamba ile Idemnity Act ambayo hivi majuzi imeletwa na yule mjumbe wa Wajir ambayo imepitishwa najua ya kwamba a ni popular sasa haijakuwa effective tunataka iwekwe katika Constitution ya kwamba yale dhulma ambaye imepita mbele na sasa akati iko shida huna nafasi yoyote ya kuzungumza , lakini hiyo uzembe ikipungua na wewe umepata kupumua lazima unatetea dhulma ambayo umefanyia.

Kwa hivyo katika hii affirmative action hizo tunesema ya kwamba sisi tulipwe ridhaa kwa ile dhulma ambayo tumefanyia. Pengine hatuwezi kulipwa mtu kwa mtu, bali tufanyiwe yale maendeleo ambayo tumekosa kwa barabara, kwa elimu, kwa maji na nini ile infrastructures yote ambayo tumekosa zote tutengenezewa tufanyiwe hivyo. Jambo lingine ni habari ya simu. Yani communicatinis power wazungu wanasema yaani mawasiliano ni nguvu. Serikali imeweka mawasiliano ya kuweka hii radio call mnajua ya kwamba hii radio call ambayo tuko nayo hapa inatusaidia sisi katika usalama na jambo lingine lakini haikubaliwi kwa wananchi kukuwa na radio call ya kibinasi. Hivyo, ikiwa tuko na radio call kila mahali, hii mambo ya kutokuwa na usalama

itapungua. Kwa hivyo, haki ya kila mmoja kuweza kumiliki yani radio call, na kila mambo yote ya mawasiliano. Halafu shida za naunga mkono wale wamesema kwamba yale bunduki ambaye ziko katika sehemu hizi zetu za North zihalalishwe kwasababu kama hatutaweza kuweka wale wadhamini usalama hautaweza kutekeleza hiyo usalama basi wananchi badala ya kuwa waizi na kutegemeana ingine afadhali ihalalishwe ijulikane mzee fulani, iko na bunduki, mtoto yake iko na bunduki, na hiyo jambo lolote la madhara ikitokea, utashikwa basi lazima ihalalishwe ifikiriwe hivyo kwa sababu Bwana Lethome wewe mwenyewe umetufafanulia ya kwamba sisi si lawyers kama wewe mmi najua wewe ni lawye na sisi ni watu ya kawaida hatujui jambo gani litawenza kuingia katika Constitution lakini kwa sababu umetuambia tuongee shida zetu, ndio tunajua tunazungumza hiyo shida zetu ili na nyinyi wasomi muweze kutupangia lakini sasa wakati yenyewe ilikuwa ni mfupi sana kwa sababu sisi tulikuwa tunataka tukutane sisi watu ya North kama pastoralists halafu tukutane na pastoralists ya south halafu ndio tuweze tutoe karatasi moja aweze kusaidia sisi lakini wakati yenyewe ni taabu.

Sasa katika upande ya Islamu, tunasema kitu naitwa wakfu commission ambaye inaangalia maslahi ya watoto yatima, watoto ya maskini kwa sababu na iundwe kwasababu hiyo ndio jambo alikuwa akifanywa wakati wa mtume (?) na iliweza kufanyika vizuri sana na kina Omar. Kwa hivyo, kitu kama (?) wakati hizo zinaitwa na sasa wakafu ni mahali ambapo waislamu watapeleka zaka zao na kila kitu yao. Na ile institution divine institution of muslims ambaye wasomi wetu wataweza kujadiliana waislamu Kadi hivi sasa zinatolewa na serikali bila kujali maslahi zetu. Kwa hivyo wale wasomi halafu ambaye inaongozwa na mufti lazima ikae iangalie maslahi zote ya waislamu ambaye ina ina (?) kwa sababu ikiwa itatuacha hivi sheria zingine mabaya mabaya inaweza kutokea mnajua ya kwamba katika Amerika hivi sasa wanasema haki ya binadamu mpaka sheria zingine chafu mbovu chafu kama kuwa na ushoga wanaume kuoana wanawake, wanaume kuo na wanaume, wanawake kuwaona wanawake inaweza kutokea ikiwa sheria hizi hatuwezi kuweka chini kwasababu tunasema kila kitu ni haki ya binadamu. Hivi jana gazeti ilikuwa mama moja alikuwa anataka bwana yake asaidie yeye auwawe kwa sababu yeye ile haki ya binadamu na huyo akizuiwa kuawa umeharibiwa haki yake ya mwanadamu. Kwa hivyo hii mambo ya kibinadamu hii ikiwa haiwezi kushikana na dini inaweza kutupoteza zaidi. Kwa hivyo sisi tunataka wale waulamaa wale wasomi wa kidini wa consult dini ya kiislamu na tunaunga mkono wale watu wamesema ya kwamba sisi tukae waislamu ingawa (?) minority, milioni kumi people hapana minority. Kwa hivyo, katika ile hali ya kugawa zile makeki za maendeleo na zingine, lazima sisi katika siasa , katika uchumi, katika kazi, katika jambo lolote tuko empowered kabisa ya kuweza kuendesha hata maserikali katika njia yoyote ile.

**Com. Lethome:** Sheikh Hassan tafadhali.

**Sheikh Hassan:** Kwa hivyo, nashukuru nakomea hapo Asanteni.

**Com. Lethome:** Asante. Ningependa tu kuwajulisha Sheikh Hassan analalamika kuhusu wakati. Hamukupata wakati wa kutosha kujitayarisha. Ni kweli lakini nataka kuwajulisha sisi kuondoka hapa si mwisho wa kutoa maoni. Kama kweli muna nia hiyo ya kutoa maoni, bado munanafasi, mnawenza kukutana, mwandike memorandum yenu, mupitishe kwa district coordinator

ambaye yuko hapa Isiolo na hapa mimi ninajua muna members wa 3 C's committee wako hapa. Itatufikia memorandum yenu. Kwa hivyo Sheikh Hassan bado muna nafasi ya kufikisha memorandum yenu. Na mtu mwininge yeoyote, ukilala usiku ukumbuke mambo ingine, andika, itafika mpaka kwetu. Kwa hivyo, sio mwisho wa kutoa maoni leo. Adan Turo, na akina mama, kama kuna mama yeoyote ambaye hajazungumza tunataka kufanya affirmative action akina mama wazungumze. Kina mama.

**Adan Turo:** Kwa jina mimi naitwa Adan Turo. Ahsalaam Aleikum. Kwa jina mimi naitwa Adan Turo. Ahsalaam aleikhum.

**Com. Lethome:** Aleikhum salaam.

**Adan Turo:** Nafikiri wenzangu ambao wamefanya presentation hapa mbele yangu wameongea mengi na kwa wakati yangu mimi nitajaribu ku-avoid ile area wame-cover sana halafu nijaribu kuongea ile area pengine nimeonelea haija pengine mtu pengine haja-cover vizuri. na moja wayo nitaanza na area kama electoral process halafu kidogo niingilie juu ya political parties halafu baada ya hapo niingilie issue ya succession and transfer of power na mwisho nimalizie cultural, ethnic and regional diversity and communal rights. na kila moja wayo nitaelezea zaidi wakati nikifika hapo na nikianza ya kwanza electoral process ni jinsi ya kupiga kura. Na kwa ukweli ukiangalia kenya yetu ile hali tuliko leo kwa wakati hii Constitution yetu iko na gap kubwa sana ya jinsi ya kupiga kura na ndio sababu unakuta watu wako kwa maoni tofauti wako kwa camp tofauti hakuna election inafanywa mara mtukufu rais anasema ni young turks, mara nini simply because hakuna jinsi ya transfer of power ama hakuna jinsi ya ya kamili ya kuwezesha mtu pengine kuingia kwa elections na ile kitu moja mimi nasuggest ni ya kwamba kuna area ambayo tunaita wards area ambayo inasimamiwa na ma-councillors kuna area ya constituency ambayo inasimamiwa na wajumbe na president ambaye huwa tunafanya election yao na unajua ya kwamba for each one of this people to become a viable winners in the election lazima wawe wamepata ah fity one percent kwa maana mimi naona mtu akipata nusu nusu ya kenya ama nusu ya hii ikisupport mtu mmoja mimi naona hiyo mtu nikama watu wote wanampenda si ati mtu tu akishinda majority tu ati mtu amekupita na kura moja ati unasema hiyo mtu ni councillor yangu ule mwininge ako na nine hundred wewe uko na nine hundred and one halafu through out five years muna camp mbili kwa sababu tofauti ya kura moja tu kwa hivyo hiyo inaleta imbalance in leadership na nimeonelea sio mzuri na wanasiasa wetu mara kwa mara wakiingia katika elections na waanguke kura utakuta mtu yule ako kwa Ford People just before the final elections ameingia Ford Kenya kwa hivyo vile mimi naona hii Constitution iangalie hiyo maneno vizuri and we should constitutionally restrict a change of party baada ya mtu kuanguka mtu awe tu amekaa kwa party yake si ati kwa vile tu ameanguka ndio anataka mamlaka aende kwa party ingine.

Na kuna hii rule nafikiri tumesumbuliwa nayo sana hii ambayo tunaita twenty five percent ruling five province naona hiyo sheria sio mzuri ati mtu anakuwa President simply because amepata twenty five percent in five province ile seventy-five ingine iko wapi? Kwa hivyo mimi naonelea hiyo nayo siyo siyo mzuri na upande ya political political parties kabla kuingilia kuna maneno ya nominations watu walikuwa wameongea hapa Nomination ya Councillors, nomination ya wajumbe, ni jambo moja mzuri sana na mimi singetaka kupendelekeza itolewe kwenye katiba. Lakini kulingana na vile tuko kwa wakati huu hai-serve purpose yoyote kwa maana nomination ukiangalia kwa wakati huu inafanywa na mjumbe ama inafanywa na chama yeoyote ambayo iko

kwa serikali kwa wakati hiyo ama chama ama viongozi wa chama yako kwa huyo hiyo ni kuonyesha kwamba ukipatiwa kitieyote kwa nomination we ni kama unakuwa spy tu huwezi represent community ama ni ya kama unakuwa spy ya community. Kwa hivyo maoni yangu ni ya kwamba badala ya kupoteza representation kama hiyo na kuitupa mbali we need to give it to some special groups of people in the community kwa mfano tunaweza patia hiyo nomination specifically kwa wanawake amba ni kikundi moja ya jamii tunajua hawatajitokeza sana pengine kuingia katika election.

Halafu ya pili tuna minority groups kwa mfano ukiangalia Kenya kwa jumla na pengine uone ile nomination ya wajumbe ambayo inaweza fanywa kwa Kenya mzima ni kumi na mbili. Si ati hiyo kumi na mbili yote iende kwa ile kabilia kubwa kubwa. Mimi naonelea at least special preference lazima ipatiwe kwa ile watu amba inatoka kwa makabila kidogo kidogo ile jamii ya chini kabisa kwa idadi. Na ya tatu pengine tuangalie hali kama ya youth hiyo representation tu-attach kwa special group kama hiyo. Na kuna jambo moja katika representation yetu ya leadership imetuletea shida kubwa sana. Kwa wakati huu tunasikia mambo mengi ati KANU na NDP ina merge National Alliance sijui for Change hiyo ni ya opposition pia wanaendelea ku-merge hii system ya ku-merge yote ni system ya kutafuta Alliance na nini na nini na nini. Na naona tukiingia katika elections hata hapo utakuta, utakuta mwanasiasa mmoja ambaye anataka mjumbe ana merge na mwanasiasa mwingine ambaye anataka councillor na katika harakati kama hiyo ahh mara mingi tunapata mtu ile pengine ambaye tunakuta siyo mtu ambaye anahifadhi pengine hiyo mamalaka na simply because of hiyo merger ambayo sisi tumefanya kivyetu. Kwa hivyo kwa maoni yangu mimi naona civic, parliamentary and presidential elections zifanywe siku tofauti and they should be constitutional recognised ifanywe katika Constitution yetu ijulikane ya kwanba civil elections in kenya will take place this month of the year, Parliamentaly, presidential, differently sio lazima ziwe zinafanywa pamoja na hii process yote lazima iwe inakuwa inaangaliwa juu na hii tume ambayo tunaita tume ya uchaguzi an independent electoral commission sio kama hii yetu ya kuregea regea saa hii, Kwa wakati huu. It should be independent; lazima iwe inaweza kuchukua jukumu kivyake. Naingia topic ya pili hali ya chama ya siasa. Ukiangalia chama ya siasa ya leo ya Kenya katika Kenya hakuna chama ambaye iko na mwongozo dhabitii hakuna chama ambaye iko na lengo mzuri katika Kenya leo kwa sababu Constitution yetu yenye hajitengeneza bara bara mzuri kwa political parties katika Kenya na mimi naona vile watu wanatengeneza chama hii leo ingine hiyo ingine chama yote inakuwa ni chama ya kikabila imegawanya Kenya mzima naona kila kabilia iko na chama labda sisi watu wadogo wadogo tu bado hatujatengeneza chama. Na unless may be we, we work on it seriously tutakuja kuwa na chama around 42-43 kulingana na kabilii ya Kenya.

**Com. Lethome:** Ndugu yangu saa hizi tuko na registered parties 46?

**Adan Turo:** 46, then its all above its above that, then that means that some may already be having 2,3 when some even don't have one. So mimi naona ni mzuri the Constitution should regulate the formation, management and conduct of political parties and the number of political parties should be restricted to two me that is my suggestion. Tuwe na chama mbili of which now at the end of the day wawe wanaform coalition government ndio tuweze kuendelea sio mambo ya kipingana kutengana kila wakati na kila political party katika Kenya iwe financed na serikali kwa hivyo yangu ni hayo juu ya political parties.

Nitaingilia juu ya successsion and transfer of power. Our current Constitution, is very silent on the succession issue. Nafikiri wale wameongea mbele yangu wamesema kwamba president ako na mamlaka kubwa sana katika hii Constitution. Na kwa ukweli hakuna mtu yejote ambaye anaweza patiana mamlaka kubwa namna hiyo kwa mwigine kwa njia rahisi namna hiyo. This is why utakuta the President is not ready to retire he is not ready to forfeit his seat sio yeje peke yake hata mimi mwenyewe ama wewe ukiwekwa hapo kesho utakuwa tu namna hiyo. Kwa hivyo mimi naonelea the President should be elected directly by the people. Na wale Presidents ambao wanaingia election waache hiyo maneno suggestion ya two political polites ambayo ni me-suggest saa hii. If we are to go in to elections the way we are at the moment utakuta ni ma Rais pengine nane, nne, tano, saba pengine wataingia election naonelea ya kwamba ule winning President pengine anajaza ile 51% na number 2 yake, pengine waingie kwa run off tuingie kwa elections na tukiwa kwa hali kama hiyo which of all will be monitored again by the electoral commission na suggestion yangu pia ni ya kwamba. utakuta President yejote ama mtu yejote ambaye ako kwa mamlaka kwa sababu ya hofu ya kujiogopa baadaye hataki kuacha hiyo mamlaka. Mtu lazima awe responsible kwa ile dhabi ambayo amefanya wakati alikuwa mamlakani na hakuna immunity yejote ambayo tutapatia President ama any other ah maybe office ah during maybe their tenure or during their tenure in terms of security welfare hakuna nini kama hiyo tutapatiana.

Ya nne nikimalizia ni juu ya cultural, ethnicity and regional diversity and communal rights. Hii ni hali ya mila, kikabila na jinsia ya pengine enviroment ile tunakaa kama vile Kenya unaona vile watu wanakaa leo, kwa ukweli nafikiri tukijaribu ku-trace origin ya Kenya Kenya iko na tribes mingi sana na nafikiri kila mmoja tulikutana hapa by accident sisi Waborana tumeonekana, Isiolo, Marsabit, Moyale, it was not by our planning the kikuyus are in central province it wasn't by their planning the way it looks like like tumekutana ki-accident tu ndio tukasema wacha tukuje tukae pamoja and then we make a nation of which up to today we have not yet made a nation na hii kabila tunasema yote iko na culture tofauti iko na mila tofautina wakati tulisema tumepata uhuru tukasema hii ndio constitution yetuya kenya kila mtu alitupa mila yake kila mtu alitupa culture yake. Tukasema ile kitu itatuongoza tukuwe mandugu ni hii Constitution ya kenya ambayo nafikiria hata haijatupeleka nchi moja so that means we are almost a lost African society hakuna wafrica wamekuwa kama wafrica wa kenya so mimi naona hii Constitution lazima i-recognize na i-promote indigenous languages of the kenyan society utakuta vijana waborana wengine wanaishi Nairobi watoto wao hawajui hata Kiborana. Na ni mtoto ya fulani simply because ati kiingereza ukisoma unapata kazi nzuri kiswahili ukisoma unapata kazi nzuri we have forgotten about our language na mimi naona hiyo lazima tuweke kwa Katiba tuseme ya kwamba katika Kenya kuna kabila fulani kabila hata kuna mzee aliongeza moja leo nilikuwa najua kama ni 42 pamoja na hiyo ya mzee 43 hiyo yote iongezwe isemekane ya kwamba kabila fulani wanaishi katika Kenya na hiyo language yao constitution iwapatia nguvu halafu tu recognise. Then we must also recognise varying cultures ya hizi community tofauti tofauti tofauti and then strengthen our customary law because tumetupa customary law yetu maneno kidogo ikitokea ni kortini polisi anakukula pesa kesi haiishi watu wako kwa taabu. So I think the Constitution should also strengthen. We have very good things to learn from our own Constitution, our own tradition rather than going to this written whatever. So this Constitution should strengthen our cultural law.

Now, to sum it up, kuna jambo kidogo nafikiri kila mtu aligusia ni-summarize mutanisamehe kama nimechukua muda mrefu juu ya basic rights. Wale wameongea mbele yangu wote walikuwa wanasma tunataka affirmative action towards better health care, education, food, security and all this lazima sio maneno tu ya serikali kuweka kwa policy paper. Ati tutapiga ugonjwa, tutapiga njaa, ujinga na kadhalika sio maneno ya kuweka kwa policy paper peke yake na kukaa, that is not enough commitment. Tunataka serikali iweke kwa Constitution. Na uliangalia maneno kama security, ambayo serikali imeji-commit the same government which has already committed itself kuangalia security ya community leo wanasma community waangalia security yao mwenyewe. Halafu tunaambiwa civil society provincial administration na wananchi waungane watengeneze security committee which is not even constitutionally recognised. Wazee wanafanya kazi wanatembea wanafanya nini but they have no Constitutional backing and my suggestion is that this kind of initiatives like the peace ah the community peace initiatives should be constitutionally strengthened okay come to such forums like the DDC yenyewe although it is a government organ ambayo inaangalia maendeleo ya wapi na wapi na wapi is not even a constitutional organ.Ni kitu D.C leo anatoa, ingine inakuja anatoa, kwa hivyo all this including school, health, management board and all these Institutions should be constitutionally recognised so that they can have the legal backing to be able to say A B C D . So may be with that nafikiri mutanisamehe. Thank you very much.

**Com. Lethome:** Asante, swali moja tu ndugu yangu. Umesema political parties ziwe mbili?

**Adan Turo:** Yes.

**Com Lethome:** I just want you to suggest kuna hii interim period sasa kwa sababu we are moving from one situation to another

**Adan Turo:** Yes.

**Com. Lethome:** Tuna political paties nimekwambia arobaini na sita.

**Adan Turo:** Yes.

**Com. Lethome:** Unataka tuzilete mpaka ziwe mbili. Criteria gani tunatumia sasa?

**Adan Turo:** I think I said it very clearly. Now nilikua nimesema nime-suggest Constitution. I mean political parties mbili. That is my view If we are to go into the elections the way we are now I think I have also given you the way forward.

**Com. Lethome:** But still we will end up, you want us to end up with two political parties. So how do we end up with two political parties?

**Adan Turo:** Meaning that you have to complete your Constitution before election.

**Com. Lethome:** Forget about the elections now. Eventually you want us to end up with two political parties.

**Adan Turo:** Yah.

**Com. Lethome:** We have forty six. What will be the criteria of reducing them from forty six to two?

**Adan Turo:** May be we work on a merger based on what we all said. What kind of a person is leading this political party. Why this political party formed. What is the purpose of this party, and may be this kind of agreements and we can reach a concensus.

**Com. Lethome:** Haya, thank you. Sora Abagila alishaenda? Wacha nimpe mama nafasi aende akapikie watoto. Chucha Duba.

**Chucha Duda:** Ahsalaam aleikhum.

**Com. Lethome:** Aleikhum salam mama.

**Chucha Duda:** ( in Borana dialect, through translator)

**Chucha Duda:**

**Translator:** Mama anasema atazungumza machache tu, kutoka asubuhi, wengi wamezungumza pia ataongezea kidogo tu.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Anasema niyi wote ni watoto wetu ambao tuliwazaa.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Anasema ye ye amezaliwa huku na ameolewa hapa hapa na tangu amezaliwa anaishi huku.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Sasa anasikia kama ardhi hawana ardhi na alikuwa anajua kwamba ardhi hii anaishi ndani ni yake.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Wakati wa koloni sisi tulikuwa tunazaliwa kule huku na tunaishi huku.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Kila mtu alikuwa na sehemu yake yani wilaya yake ya kuishi.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Lakini leo mipaka sijui imeondolewa kila mtu anaenda vile anavyotaka.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Kutoka ukoloni, kutoka uhuru mpaka wakati tumewekwa kizuizini ya concentration campmpakawakati huu sisi tumbaki maskini na hatuna msaada yoyote.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Wanawake wamefanya juhudhi baada wamekosa maji ya kuunda vikundi vyta wanawake ya aina mingi.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Ma-groups haya yamesaidiwa na serikali kwa kupewa msaada kidogo kidogo ambayo sasa wamenunua mifugo kidogo kidogo wako naye.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Wamechukua jukumu ya kuchunga hii mali mara kwa mara wanapata hata wanaenda mbali mpaka hadi Isiolo kutafuta nyasi, nyasi yao imekuliwa na jirani ambao wametembea vile wanavyataka.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Mali hii ambayo tunahangaika nayo, hatupati soko ya kuuza.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Mama anapendekeza K.M.C iletwe karibu hapa Modagashe na soko ya ng'ombe ipatikane ili sisi tupate faida ya kazi ile tunafanya .

**Chucha Duda:**

**Translator:** Ya pili anasema wamesomesha watoto na watoto wao wamekaa bila kazi wanakaa varandani.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Hata wale wanataka kwenda kwa kikosi ingine kama

(?)ama nini hawapati nafasi kwa sababu

wazazi wao hawana mali.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Hata wale wamehitimu form 4 na wamepita hawapati kazi mzuri.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Anapendekeza serikali ape hawa vijana kazi mzuri na amemalizia hapa.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Wapate msaada ya kupatia vijana wao kazi mzuri.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Na pia groups wapatiwe support ya kutosha kwa sababu wanawake wanafanya kazi mzuri sana nyumbani.

**Chucha Duda:**

**Translator:** Asante sana amemalizia hapa.

**Com. Lethome:** Asante sana mama. Hassan Galgalo, Hassan Galgalo.

**Hassan Galgalo:** Ahsalaam aleikhum.

**Hassan Galgalo:** Basi Asante sana Bwana Commissioner. Vile ulisikia asubuhi labda mimi peke yangu nimetoka kwa sehemu moja ambayo inaitwa Olesamburu. Mimi kwa majina naitwa Hassan Galgalo. Chief Olesamburu location. Kwa hivyo nitajaribu kusema kitu chochote peke yangu tu kwa hivyo hata kama nitaongea nyingi hiyo dakika utaniongezea. Mimi na-represent location mzima.

Basi kitu ya kwanza ambayo nitaongea kidogo juu ya border mambo ya border. Nimesikia watu wanaongea mambo ya majimbo mimi mwenyewe vile nimependekeza hapo nitatoa mapendekezo tu. Nimeonelea sisi tupatiwe Province mzima kama jamii ya kiborana na hii Province iwe ni Isiolo, Moyale na Marsabit. Na vile mimi naona hii Province haiwezi shindwa na Province kama ile North Eastern hii Province ni kubwa kabisa. Kwa hivyo ingefaa zaidi kwa sababu ile watu sisi tunapakana nao ni watu ambao sisi hatuwezi ku-match pamoja na hawa. Ni watu ambao ni wengi kushinda sisi, wameelimika kushinda sisi, kwa hivyo vitu kidogo ikipatikana resource yote inaenda kwa hawa tu. Kwa hivyo sisi hiyo ndio njia moja imetufanya tubaki nyuma. Kwa hivyo tumependekeza tuywe na province moja peke yetu kama ya jamii ya Kiborana. Hapo mbeleni kidogo, kuna wakati moja kulikuwa uandikishaji wa kazi. Mambo ya kazi sisi tumebak nyuma sana. Tungependelea, wakati ya kuandikisha watu kama tuseme kazi kama military, police, prison inafanyika Isiolo ambaye inafanyika kwa District headquarter. Lakini

District Headquater yetu imekuwa ni pahali ambaye panaishi watu wengi sana kwa hivyo sisi tunapata kiwango kidogo sana. Kwa hivyo tungependelea kwa vile hapo mbeleni 1979 na 1978 recruitment inafanyika Garbatula sub-District. Tumependeza iwekwe kwa sheria kwa vile sisi ni watu wachache ambaye tumbaki nyuma, iwe ni njia moja ya kuinua sisi recruitment yetu ifanyike Garbatula Sub-district. Ifanyike Garbatura Sub-District ama kwa Sirichwa Division.

Hapo hapo ningeongea mambo ya tena border tu. Mambo ya border vile unajua zamani kidogo hapo mbeleni kila mtu alikuwa na boundary yake, mpaka yake. Vile sisi tangu tulipozaliwa tuliona kama sasa hapa boundary yetu ilikuwa ni hii (?) zamani ambayo inagawanya Eastern na N.Eastern. Sasa ile vitu tumeona tangu uhuru 39 years, unakuta hii mpaka inahama nahama na bila kuhama. Inahama kulingana na vile labda watu wameelewa ama sijui resource ile mtu ako naye. Kila Minister wa land akiingia anasongesha piece fulani. Zamani border yetu ilikuwa ya Eastern Province ni hii (?) kubwa unaona. Sasa imekuwa ni katikati ya Town hii. Sasa imesonga imekuwa ni Sricho. Kwa hivyo sasa tungependelea mambo ya border kutembea, ku-move sasa margin inakosa barabara inatembea tembea hiyo maneno iwekwe kwa sheria ya kwamba border ibaki kama zamani ya 1960s. Iwe border yetu ni Laga, na iwe imewekwa kwa sheria apala kitu ya kusema fulani atakuja (?) fulani na mtu akiitwa hapana (?) wewe. Iwe ni kitu ambayo iko kwa sheria kabisa ambayo inajulikana. Kila jamii iwe na boundary yake ile ya zamani. Na ikiwa namna hiyo hata mambo ya usalama itakuwa mzuri kila kitu itakuwa mzuri hakuna shida.

Naongea juu ya barabara. Barabara ukitembea kuanzia hapa unakuta lami ama muram imefika kwa kila Division ama hata Location imefika. sisi mimi nafikiri nyinyi mumekuja jana, halafu ukifika hata Isiolo badala ya kwenda kwa kazi yako unaenda kwa hospitali kwanza kwenda kutibiwa, kwasababu umevimba matakao, labda mkono umefanyika namna hiyo, hii yote ni hali ambayo barabara ilivyo.

Kwa hivyo tungependa, tupatiwe barabara mzuri kama wakenya wengine. Barabara ile inafaa. Ndio tuwe na ma-bus, tuwe na matatu hiyo vitu yote sisi labda tunaweza kujaribu hata kama labda ni masikini iko mtu moja anaweza kuleta bus, anaweza kuleta matatu lakini tumeshindwa kwa sababu barabara yetu ni mbaya. Ukilete gari hapa hata gharama ya barabara yenewe, inamaliza kwa siku moja, na hakuna mtu angependa kumaliza pesa yake kwa siku moja. Barabara mzuri. Unakuta kama sehemu yetu kama location yangu mwezi mbili watu hii hawana chakula, unatoka na mguu pekee yake. Unaenda thirty kilometres ndio uende ukamate hata ile iko pahali hii barabara mbaya hata hii mbaya hakuna huko, huko ni mashimo tu. Imeingia maji laga napita, unakuta watu wanakaa kwa Island. Kwa hivyo hiyo sasa hapo ndio tunapenda nyinyi tunge angaliwa zaidi.

Tunaenda moja kwa moja kwa maji, hapo kwa barabara nimemalizia hapo. Maji Wakenya wote mimi nafikiri kwa wakati huu, kuna wakati imetangazwa kwamba kufikia mwaka ya elfu mbili kila Mkenya atakuwa na maji safi. Sisi mpaka saa hii, ile maji tunakunyua ni ile inateremka ambaye inasafisha sijui kila kitu ndani mimi nafikiri, kama sehemu yangu sasa ile ya Lesamburu, sisi tunatumia maji ya pahali ingine naitwa swamp Tafa. Hii yote watu wanajua. Kila mwezi sisi ni typhoid, typhoid typhoid kwa

sababu maji ni ile inapitishwa kila kitu ndani, maji chafu hakuna maji safi. Kwa hivyo tungependa kuwe na maji safi. Badala ya yani kila mtu apatiwe maji safi kama ile right ya kawaida ya binadamu. Hapo hapo hii maji, sisi ni watu amba wanakaa kwa Ewaso Nyiro, Ewaso Nyiro hii, tangu tulizaliwa Ewaso Nyiro unakuta kwa wakati huu na wakati ile ingine, Ewaso Nyiro iko na story tofauti. Mimi nafikiri ardhi bado badilika mvua ya Mwenyezi Mungu inaendelea kunyesha tu. Lakini ile kitu imefanyika, iko watu wanajaribu ku-tamper na Ewaso Nyiro river. Kwa hivyo kitu ile tungependa, tungependa hii sheria iwekwe kwa sheria ya kwamba, Ewaso Nyiro yani sheria ya mto iwekwe ya kwamba, hakuna mtu atafunga maji ya mto ambaye inatembea. Kwa sababu Ewaso nyiro unakuta Ewaso Nyiro inatoka upande ya upande iko na miti, upande ya Aberdares. Na huko iko mvua kabisa, mvua ya Mungu iko tu kama kawaida, hakuna kitu imefanyika. Lakini unakuta hiyo maji ni watu tatu ama mbili ambaye ni wanaume kabisa ndiyo wanaendelea kufaidika naye. Wale wako pande hii wamesahaulika. Haingeweza kuwa Ewaso Nyiro ni seasonal river, Ewaso nyiro hapana seasonal river, labda kwa mwaka ni mara moja tu. Lakini sasa unakuta kwa mwaka moja miezi sita hakuna maji. Hiyo nikusema iko watu wanaendelea kutumia, dams najengwa huko, mwezi moja mzima nakwenda kwa hiyo dam, mwezi ingine naenda kwa dam ya mtu mwengine, mwezi ingine naenda kwa dam kwa mtu mwengine. Kwa hivyo tampering iwekwe kwa sheria Ewaso Nyiro kwa vile iko watu wengine wanaendelea kupata faida ya Ewaso Nyiro. Iwekwe kwa sheria kabisa Ewaso Nyiro mtu asikamate kunyunyiza maji hiyo kitu kwa shamba yake. Ewaso Nyiro iendelee kutembea. Mtu aki tamper naye iwekwe kwa sheria kwamba iwe ni hatia kufanya namna hiyo.

Tunaingia upande ya health. Tungependa pia sisi ni vile ni vile hapo ni vitu ile watu wameongea tu. Unakuta upande ya health pia sisi tuko na shida zaidi. Kama barabara hakuna, maji hakuna sasa lazima ujue ya kwamba hata upande ya health namna hiyo tu. Tunataka tujengewe pahali ambaye tunaweza kupata dawa, kama ni dawa munapimwa, kama Wakenya wengine wote. Sisi ile kitu imetumaliza resource yote, mtu akipata ile malaria kidogo unaona anatembea mpaka Isiolo. Unakuta resource yako yote inaishia huko. Kitu kidogo tu ambayo ungetibiwa hakuna pahali ya kutibiwa. Hapo tuangaliwe pia tunataka iwe ni lazima kwamba kila mtu anapata dispensary kwa pahali anaishi.

Tuaingia pia mambo ya masomo. Mimi nafikiri watu wengi wameongea juu ya masomo. Masomo yetu iko tofauti na Wakenya wengine. Sisi pia tuko na walimu, tuko na kila kitu lakini masomo yetu hapana iko sawa sawa. Kwa sababu ya shida. Hii shida ni ya nini? Tuko na shule. Environment yenyewe hapana mzuri kama ile ya down country. Kama tuko na shule, shule pia haina ile facilities ambaye inahitajika. Tunataka facility ya shule zetu kama mashule ingine. Ama tuangaliwe hata zaidi, kwa sababu ya kubaki nyuma hapo mbeleni. Pia masomo iwekwe ya kwamba, sisi masomo yetu iwe ni bure kuanzia standard one mpaka university. Sisi naye tumependekeza hiyo namna hiyo.

Hapo tena nitaingilia mambo ya haki ya wasichana. Haki ya wasichana hii, ni kiingilia kidogo sijui kama itakuwa mzuri nikiongea kwa Kiswahili lakini nitajaribu zaidi. Vile mjuavyo, iko wasichana tuseme ya aina nyingi kwa Kenya. Iko wasichana ya kila kabilo, iko wasichana. Lakini kimila Kiborana bila kuongea hata mambo ya dini, iko sheria ambayo inachunga wasichana. Msichana, hapana kitu ambaye inachezewa namna hiyo tu. Msichana kwa Kiborana, anahesabiwa kama mwanaume tu. Lakini of late sasa, sisi tumeanza kuchukua sheria ingine ambaye sijui ni ya Western ama ni ya Down country sijui ni wapi, unakuta mtu

nakuja tu nakamata msichana yako naweka mimba. Ukienda kwa kuweka sasa iko sheria yetu ambayo ni ya kiwazee, ukienda kuongea hapo useme sasa hiyo maneno itasuluuhishwa, unakuta mtu ameruka. Ukienda kwa sasa ati judge ama mahakama, imesemekana si wewe ndio umependa ni nguvu hapana sio nguvu, kama hapana nguvu, unakuta mtu amebaki namna hiyo. Sisi tunataka hii iwekwe nguvu mtu ambaye ataguza msichana yetu, tukamate na sheria yetu. Iwekwe kwa sheria kwamba kukamata msichana ya Borana ni hatia special. Na ni kama rape na ni hatia na ihukumiwe na hukumu ile ya hapo. Bila kuwa na hukumu ingine kando. Ama bila kusema hata Down country hakuna kitu mtu nafanyiwa mtu fulani namna hiyo, sisi hapana taka kujua. Iwe hiyo sheria ihifadhiwe, ndiyo mtu aogope.

Watu wameongea hapo juu ya wazazi, wameongea juu ya wazee, wazee waangaliwe, akina mama, wazee, lakini mimi naongea kijana mmoja tu nimesikia ameongea. Wazazi, haki ya wazazi. Wazazi, mimi nafikiri ni wale wamezaa, mimi na wewe na mtu mwengine wote. Basi, unakuta kama ni mimi ama ni mtu mwengine, wazazi mzee amesomesha mimi, nimeenda University, msichana namna hiyo, unakuta kama ni watoto yote wameenda mzee amebaki na mama peke yake kwa nyumba. Sasa unakuta watu wamekuwa wakora sana, saa ingine hawezi kusaidia mzee, na hata shilingi mia moja, wanaomba kila siku, unaomba, naitwa kwa chifu, naitwa kwa nani, ndio apatiwe mia mbili. Nataka iwe lazima, ni kama lazima iwekwe kwa sheria, ya kwamba, mtoto lazima asaidie wazazi. Mimi nafikiri hata kama kwa kimila ingine imeshindwa, iwekwe kwa kimila ya Kiborana ya kwamba mtoto wako ukisomesha kijana lazima asaidie baba yake na mama yake. Hata msichana namna hiyo.

**Com. Lethome:** Basi maliza.

**Hassan Galgalo:** Nimemaliza hata niko karibu tu. Basi ya mwisho kabisa nitaongea juu ya sisi wafugaji. Vile mjuavyo, sisi ni wafugaji sisi ambaye iko na shamba, vile tungependelea, tunataka sheria hii, ihushe sisi wafugaji. Ya kwamba tujengewe factory ya nyama ambayo itatengeneza nyama ya mikebe, nyama ya kila aina, fridge itengenezwe, halafu tuwe kama Wakenya wengine sisi naye tupate faida kwa ile vitu ambaye tunafuga kama ni mifugo. Pia tungependa zaidi, tuwekewe factory ya maziwa, K.C.C. kwa sababu kama wakati huu tunasema iko maziwa, maziwa yetu unakuta watu natembea wanapeleka kwa K.C.C. K.C.C hapa hakuna. Kwa hivyo tungependelea serikali yani Katiba hapana serikali, Katiba hii iundwe, sisi tuwekewe factory ya maziwa, K.C.C, ili wakati mmoja, kama tutakuwa na maziwa, factory yetu iendelee kufanya kazi, maziwa yetu badala ya ku-waste, watu wajisaidie nayo. Pia tungependa, tutengenezewa factory kama hiyo ya maziwa, factory ambayo itatengeneza maziwa ya powder. Maziwa ya powder ingesaidia sisi zaidi kama wakati huu kama tungepata machine ya hii ya maziwa ya powder, tungelete tu unakuta kila mtu analeta maziwa yake inawekwa kwa powder, wakati ule unakuta hakuna kitu ya kutumia tunatumia tu maziwa unaenda, hata kama fridge hakuna, iko njia labda ama watu wafundishwe. Tunataka iwekwe kwa Katiba hizi yote tuwe supplied with.

Halafu, nitaongea kidogo juu ya administration ambaye hata mimi mwenyewe ni mmoja wao. Nikiongea hapo, nimesikia asubuhi watu wanasema P.C. hakuna maana, D.C. hakuna maana, nimeona hii watu wako na maana zaidi. Mimi mwenyewe nilikuwa ni mmoja wao lakini kujisifi hapana mzuri, na beside hiyo, sisi iko wazee tunafanya nao kazi. Tunataka iwekwe kwa Katiba, hao

wazee ambao wanafanya kazi na ma-chief wawe wanapata malipo. Hao wazee ndio backbone ya location ama division, hawa watu wanafanya kazi zaidi. Kwa hivyo tungependa hao wazee, wawekwe kwa Katiba, walipwe. Basi kwa hayo machache, asanteni sana.

**Com. Lethome:** Haya Ali Dhuba. Ali Dhuba, hayuko? Abdi H. Mahadi halafu Hussein Borr yuko? Wewe ndio mtu wa mwisho Hussein Borr.

**Abdi Mahad:** Salaam aleikhum (?) Wabarakatu.

**Com. Lethome:** Aleikhum Salamu.

**Abdi Mahad:** Kwa majina mimi najulikana kama Abdi H Mahad na mapendekezo yangu ni ya kwamba, Constitution of Kenya, to protect the right of the individual, according to the bill of human rights in the U.N. Charter. Na the law Impossers, waangalie ya kwamba, kama mtu atanyanyasa haki ya binadamu, ama auwe binadamu, awe ni polisi, ama awe ni bandit, ichukuliwe sawa na sheria ichukuliwe hatua hapo hapo, kwa sababu wengine wanashika lawyers na nini na wameua binadamu ama wameyanyasa haki ya binadamu kwa njia moja ama ingine. Kwa hivyo, sheria iangalie sana yule ameumizwa.

Ya pili ni kuhusu mambo ya uchumi,economy. Economy njia moja ya mapato ya Wakenya leo ni mshahara na serikali itilie maanani sana na ingie kwa sheria kwamba wafanyi kazi wa serikali ama wengine mshahara ya hawa iwe reviewed na commissions ambaye itakuwa inaangalia mshahara ya wafanyi kazi wa serikali iwe appointed by the parliament, but not the executive. Ile ingine kuhusu hali ya uchumi pia ni ile nitaongea juu yake ni price, bei ya vitu, especially basic needs, kama food, clothing and shelter. Bei yake iwe chini ili Wakenya wapate chakula, mahali ya kuishi na mavazi kwanza.

Na kitu ingine nataka kuongea juu yake ni Kenya Bureau of Standards. Hiyo sheria yake sheria ihakikishe ya kwamba wanatimiza kazi yao kwa vile leo hii Kenya tunapata low quality goods ambaye inatumiza kabisa hiyo vitu ukinunua kitu haidumu. Na mambo ingine ningetaka kuongea juu yake ni liberal markets. Kwa hivyo it should also be limited kwa hivyo wanaleta vitu zingine na our local goods inakosa market ama inakuwa ni bei ya juu vile ambaye ni vitu kutoka nje inakuwa bei chini na inahariu local goods yote inakosa maana yote hata Wakenya hawaendelei kiuchumi.

Ile ingine nataka kuongea juu yake ni banking system ya Islam to be establlished in places where much inhabited by the Muslims especially the Coast and the Northern Frontier district. So that to avoid (?) which has been condemned by the Quran and also condemned by philosophers like Aristotle. And mostly we are being disturbed by banditry na sioni kama serikali inatilia maanani watupatie anti stock theft unit wawe wanakaa mahali popote ambaye inhabited by the pastoralist so that mara moja ng'ombe ikichukuliwa wanafutilia. Na nafikiri badala ya regular police hawa, wahimize sana tuwe na anti stock theft unit kila mahali katika northern frontier district.

Employment in Kenya should be according to the qualification but not through corruption and godfathers and people who are not competent and who are not qualified for certain jobs wanawekwa mahali wanaharibu mambo yote katika Kenya. Okay, also, laws to be formed to root out corruption from all public sectors because it has become threat to every Kenyan and Kenyans have thought that it came to stay and corruption will never be rooted out.

Electoral commission of Kenya, ambaye ndio referee, ya viongozi wale tunapata na viongozi ndio wanaenda kuwa serikali, ihakikishwe ya kwamba, iwe imetuwa independent body na commissioner yake iwe appointed by other bodies not the executive. Na those other bodies, kama mimi na propose the other groups kama council of churches, Supkem, NGO, Council of NGO's na hawa ambaye pia wanahudumia raia wawe wanakaa chini according to the professional qualification waangalie nani atakuwa commissioner ya electoral commission na hawa wengine.

Lastly Bwana. commissioner, niko na swali moja nataka kuuliza. Kama Kenya tulikuwa na sheria hata zamani, na nyingi ya hizo sheria hata kama ilikuwa, haikuwa inatekelezwa. Tuko na guarantee gani kama Wakenya kwa sababu Wakenya wengi vile walikuwa wanaongea leo ni kukosa imani na zile sheria hata zile zilikuwa hazitekelezwi. Na hii inaundwa leo kama vile tunaonanga budget ya Kenya inakuwa ama mambo yote ya Kenya kama salary ya teachers wakati ilikuwa imewekwa sign itakuwa ni paper work ama tuko na guarantee gani ya kwamba itai-implement-iwa?

**Com. Lethome:** Shukrani kwa maoni yako na asante kwa swali lako. Unataka jawabu sasa hivi?

**Abdi Mahdi:** Naam.

**Com. Lethome:** Unajua ndugu zangu lazima niwaambie kitu moja. Kuna kitu kinaitwa Constitution au sheria na kitu kinaitwa costitutionalism usheria. Katiba na Ukatiba. Haya ni mambo mawili tofauti.. Unaweza kuwa na sheria nzuri sana lakini ikiwa ile sheria itabaki kwenye karatasi, haitakusaidia na chochote. Kwa mfano Kenya tunawizi ama hakuna wizi? Kuna sheria ambayo inakubali mtu aibe Kenya? Sheria yetu inasema mtu asiib. Lakini kwa Sababu haikufuatwa hiyo, watu wanaiba. Corruption, hakuna sheria ambayo imepitisha watu wawe corrupt, lakini kwa sabbabu tunavunja sheria, ndio sababu tuna corruption. Sasa hii, sio swali ambalo linaweza kujibiwa na mtu yeoyote, ni attitude yetu kama Wakenya ibadilike sasa, tunabadilisha Katiba na lazima sisi mwelekeo wetu juu ya sheria ibadilike. Unajua siku hizi vile ilvyo, ukiajiriwa mahali, unaona yule ambaye yuko juu yako ni mwizi. He is corrupt. Na wewe unasema hata mimi naiba. Kama fulani anaiba, na mimi si nitaiba. Sasa ni culture. It has become a culture in ourselves kuwa hatufuati sheria kwa sababu unaona wengine wanaharibu na wewe unasema wacha na mimi ni haribu. So, hata sisi tunaambia watu, ni vile tu pengine hamukupata nafasi ya kusikiza programme zetu kwenye redio, sijui kama K.B.C. inafika hapa ama haifiki, tulikuwa tunawaambia watu kwenye redio tunaweza kutumia pesa nyingi sana na wakati mwingi sana watu watoe maoni mauri sana tutengeneze katiba. The best in the world. Tunaweza kupata ile katiba nzuri kuliko zote ulimwenguni. Lakini ikiwa haifuatwi, kuna faida yoyote? Na sasa, hakuna mtu ambaye anaweza kulazimisha sheria ifuatwe,

ni sisi kama Wakenya, attiitude yetu ianze kubadilika na ndio tunafurahia wale ambao wanatoa maoni, na kusema civic education, kuhusu elimu za katiba au elimu ya haki za kiraia, isiwe inafundishwa mara moja pekee yake. Iwe ni kitu ambaye inaendelea. Skulini watoto wanafundishwa habari ya Katiba, kina mama kwenye group zao wanafundiswa, wazee wakiwa kwenye group zao wanafundiswa, mpaka tubadilishe attitude yetu. Mimi nina amini kuwa, hata hii Katiba ambaye tunabadilisha sasa hatukufuata yote. Mambo mengi hatukufuata. Tungefuata, hatungekuwa mahali tuko. Mimi nimeenda katika nchi za arabuni, nasema hivi ukienda katika nchi zingine, mtu anaogopa kutupa karatasi njiani. Kwa mfano yuko kwenye gari yake, amekula chakula pengine ana hawezi kutupa kararasi nje kwa sababu sheria inasema, keep your town clean. sisi kwetu, njiani huko unakula ndizi unarusha hata unapiga mtu wingine naye macho. Si ndio takataka imejaa? Garbage imejaa kila mahali. Unaambiwa, usichafue mazingara, usichafue mto, Nairobi tuko na mto. Hiyo mto hata unaweza taka hata kuoga ndani yake? Inanuka harufu yake. Nitawapa mfano, River Nile. River Nile si inatoka hapa Lake Victoria? Nenda Cairo in Egypt. Cairo ina populaion ya fifteen million people, hiyo ni town moja. river Nile imepitia katikati yake. in the middle of the city unaweza kuchota ile maji ukunywe. Ni safi kabisa. In the middle of the city kuna mahoteli, kila kitu, kando kando ya hii mto. Lakini wameihifadhi, wanajua kwamba hiyo ndio uhai yao, River Nile. Sisi hapa kwetu, tunachafua mito yetu tunachafua. Ni kwa sababu ya nini? Attitude yetu. Kwa hivyo tunapozungumzia habari ya Katiba, lazima pia tuzungumzie habari za attitude zetu. Zitabadilika ama hazitabadilika. Otherwise it will be Waarabu wanasema rangi wino kwenye karatasi. It will just be ink on paper. Useless for all of us and we have no business sitting here, we are wasting time for nothing. Kwa hivyo tunapozungumzia habari ya kubadilisha Katiba, pia tufikirie habari ya kubadilisha attitude zetu tuweze kufuata hiyo sheria. Asanteni. Haya tumpate Chief Hussein Borr.

**Chief Hussein Borr:** Wasalamu waleikhum (?) Wabarakanatu.

**Com. Lethome:** Waleikum Salamu.

**Chief Hussein Borr:** Mwenyekiti Bwana Commissioner nafikiri yangu nafikiri ni kichangia hii maneno ya Katiba nitaongea maneno ya kadhi. Kadhi's court napendekeza iwe independent huru, na Kadhi, asichaguliwe na kura. Kadhi achaguliwe na watu maalum Waulamaa. Sisi Waislamu, siku yetu ya kitaifa ya Islamu, ni siku mbili. Kuna Id Ul Fitr na Id Lalah. Katiba hapo mbeleni tulikuwa tumekubaliwa Id moja tu kama sheria ya kitaifa. Napendekeza Id yote mbili iwe siku ya kitaifa. Wakati ninaongea maneno ya court, nafikiri asilimia sixty percent ya watu ya Kenya ni watu maskini. Si watu wa kujimudu. Wakati mtu anashtakiwa mtu maskini aende kortini Isiolo, ambayo transport kwenda zaidi ya elfu moja, gharama zaidi ya elfu kadhaa, unasilchia maneno ya mentioning, maneno ya kuahirisha, unaona ile mtu hajiwezi heri abadilishe kujitetea anaona tu akubali mashtaka afungwe akae jela. Mimi

naona kuna wazee wanafanya kazi muhimu katika jamii, katika location katika sub-location.

(?) katika Kenya, ipatie mamlaka katika hii wazee, wazee mafuko maalum watafutiwe, sababu hii wazee wana-deal na maneno ya bibi na bwana, maneno ya watoto kwa watoto, mpaka hata wanyama kwa wanyama hata punda wote mambo mengi wanashughulika. Nafikiri kama ingekubaliwa kesho watu waende court, wanashikilia zaidi shahidi wazee nyumbani. So

wazee kama hawa lazima watambuliwe na mafuko maalum ipatiwe court ya kawaida iendelee tu na court one.

Hapa katika northern Kenya, either siku yote ni siku ya kiangazi. Unaona either ukame ama hata ile mvua kidogo nakuja inaonekana baada ya mwaka mbili yote, kuna ukame na mwaka moja mvua. Mimi naona, Katiba hii, sababu saa hii ukipita hapa kidogo unaingia Ladera constituecy, kuna daraja, (?) maji mingi kabisa inapotea hivi. Kwa nini hii Katiba haikubalishi watu wa Northern Kenya hii maji ishikwe, ile muda ya mwaka mbili ambaye tunakaa ukame maji hii iwekwe kwa mashamba sio ati kila wakati mfugaji, hii land yetu tunapata huru na sisi tunakula kila kitu si nyama peke yake na maziwa. Nafikiri hii maji ikishikwa, hiyo kangazi ya miaka miwili hatuwezi kuwa na shida. Kwa hivyo hii mambo ya ukame kila wakati disaster, disaster itapotea. Kwa hivyo, hii Katiba hii itenye hazina maalum ya kuangalia maneno ya disaster ikiwa ni mvua ama ukame, wacha tupate shamba ya kutosha, na hata sisi tukae safe na hata tukisema majimbo (?) yote tutaomba. Nafikiri tutaomba zaidi ya miaka hamsini serikali itutembelee. Kwa hivyo badala ya hayo wacha kwanza hata sisi tuwe tayari, hii maji iwekwe maanani.

Trade Union. Katika Kenya yetu, inastahili kuwa na vyama ya kuangalia masilahi ya wafanyi kazi. Lakini mimi naona kidogo si hivyo. Kenya Civil Servants Union, nafikiri karibu miaka kadhaa ilikuwa hajakubaliwa, imekubaliwa juzi juzi tu. Hata hivyo ukiangalia huko ndani wanasema tumekubali kutoka from job group A to H. J to Z tuko wapi jameni? Bona tumetengawa? Si tungekua pamoja Ndio ingekua mzuri? Si kutengana ni udhaifu kushukikana ni nguvu. Tunataka haki sawa katika trade union.

Katika sehemu yetu wakati wa ukame, umesikia watu wanasema oo! Wale ambaao wanapatikana on the ground ni ma-chief na walimu. Nafikiri hata hawa ukiangalia kazi yao mzuri, si sawa, kuna kasoro. Ukisikia mitihani ya national, Isiolo, mkia, Marsabit mkia, Moyale mkia, hii yote kulikuwa kuko shida. Kama hospitali ya (?) unaenda mpaka Isiolo, birth certificate mpaka Isiolo, chochote unatafuta kwa maisha ya binadamu mpaka Isiolo, kweli kazi yao on the ground itakuwa mzuri namna gani? Nafikiri hao watu wanaishi katika hardship wafanyi kazi, waangaliwe vizuri kabisa. Hiyo thirty percent hiyo hata watu wanasema ikifika elfu moja mia mbili ati isifike hiyo, hiyo si sawa. Hata hiyo kitu iende mpaka sixty percent na isiwe na mpaka hiyo watu ambaao wanaishi katika sehemu hii waangalie kabisa hata kazi hawana mzuri.

Wakati tunaingia maneno ya diwani, tunesema masomo ya diwani iwe masomo ya O'level na wengine wanasema iwe ya kawaida tu hata kama hawajui kusoma ni sawa. Lakini mimi najua si sawa. Sisi tunaongea maneno ya illiteracy kila wakati kile ambayo inapeleka sisi nyuma ni hii literacy. Tunajaribu kuondoa maneno ya illiteracy mpaka kila mtu anajua kwa nini hiyo mwanakenya haki yake kama mwanakenya. Nafikiri nikisema hivyo (?) minimum qualification kwa polisi, kwa walimu inaenda juu hata C+ hata naenda kwa D. Tunataka kiongozi kama councillor, ambaye pengine anaogopa askari, anaogopa mfanyi kazi wake sasa hana elimu, hiyo si sawa. Mimi naona maneno masomo ya O'level ni mzuri. Tunataka maneno ya literacy iendelee watu wajaribu kupigana mpaka wakati ile wanona matokeo yake ni sawa.

Moving Permit. Kidogo hapa, sheria hapo awali ilikuwa inakubali usafirishaji wa mifugo ya biashara kutoka district fulani mpaka

district zingine. Lakini wananchi wa kawaida kila wakati wanalamika. Wanasesma hii mali inapita katika sehemu yetu, ina madhara mingi, ina hali ya ujambazi, ina ugonjwa, na mambo mengi (?) , lakini sheria hapo awali ilikuwa inakubali kama legal document mtu ako naye, na permit, no objection, license, mtu anakubaliwa kusafirisha yake mahali mpaka ambayo iko.

(?) kama hii tatizo watu wanasesma iko, ngombe ya sehemu fulani haijapata chanjo, na ikiingia sehemu hii inaweza hatarisha mali ya sehemu hii kwa hivyo hiyo pia, hiyo sheria ibadiliswe na badala ya kusafirisha kwa miguu, isafiriswe kwa barabara.

Maneno ya (?) act. Hii maneno ya act hiyo ilikuwa amezuia watu ya Northerners hiyo mifugo yao isiende isifike pahali ya soko, na ili ipatie hoa wazungu soko yao ipate nafasi. Maneno ya Quarantine, kila wakati baada ya miezi tatu inasemekana ng' ombe ni mgonjwa ng'ombe foot and mouth na (?) pengine hata wa kawaida, ambayo ni njia tu sababu Act ya zamani (?) na watu ya pande hii, pia Act hii iondolelewe act ambayo inahakikisha watu wote wako na uhuru wa kupeleka mali yao soko, pia iangaliwe.

Ofisi ya utawala, provincial administration. Mimi naona administration ni sawa. Ni njia ya kipekee inashikanisha wananchi na serikali pamoja. Ofisi ya chief, ninafikiri bila (?) ya serikali katika location ambao pengine watu wakiona serikali

(?) pengine ni huyo chief. Ni ofisi ambayo first hand information, chochote ambacho kinatokea katika sehemu inapaswa inafika kwake. Mimi naomba, hii ofisi ipatiwe nguvu, hazina maalum ambaye chochote ambao pengine wananchi wanahitaji kwa dharura haraka, maneno ya kusema tumia dini, ama una unapewa na wananchi isiwe, nguvu rasmi ipewe hiyo ofisi idumu.

Maneno ya resource distribution. Leo Kenya ukiangalia, ofisi kuu yote, parastatal yote iko Nairobi. Kwani sisi hatutaki hiyo ofisi iwe karibu na sisi? Sababu huduma ya ofisi hiyo ni nyingi sana. Kwa hiyo, napendekeza, distribution ya hiyo resource ya maofisi mingi, hiyo itambazwe katika Kenya yote. Kwanza ofisi ya maji kwanza iletwe karibu na sisi tupate hiyo maji ambayo imepotea mingi.

Maneno ya Katiba, hapo mbeleni mumesikia, Katiba wananchi wafunzwe, sioni sababu wananchi, ambao iko na haki yao, baada ya miaka thelathini na kadhaa, ati watu nafunzwa haki yao ya sheria. Hiyo maneno isiwe tena. Nafikiri kuanzia sasa, mafunzo ya sheria, wacha iwe mpaka mtoto nyumbani. Katika classes, katika madarasa hata mabaraza ya ma-chief yote. Maneno ya Katiba ni haki ya kwanza mtu akijua haki yake pengine anaweza kujitetea. Lakini kama hajui, itakuwa vigumu sana. Kwa hivyo hiyo Katiba iwe daima kwa mambo zote. Nafikiri kwa hayo machache nasema asanteni thank you very much.

**Com. Lethome:** Shukrani, hivi sasa natamani kufunga kikao, lakini kwanza swali moja, kuna.. Mzee umekuja, karibu mzee. Tulikuita lakini ulikuwa umetoka kidogo, karibu. Na kama kuna mama ye yote anataka kuzungumza kabla sijafunga kikao mama natoa nafasi na yule Sheikh yuko karibu na Joseph kama anataka kuzungumza nitampa nafasi naona amekuja sasa hivi. Mzee mulize Joseph kama anataka kuzungumza.

**Mzee Sora:** Ahsalaam aleikhum

(?) waibarakatu.

**Com. Lethome:** Anza kwa jina mzee.

**Mzee Sora:** Mimi naitwa Sora

(?), mzee wa hapa na kule Siricho, yote mimi iko naye. (in Borana dialect, through traslator)

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee Sora amesema yeye ni mzee wa hii Division, kile angetaka kuzumza mengi imezungumzwa na watu lakini atagusia kidogo kidogo.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Wa kwanza ni mambo ya maji.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Tangu Kenya ipate uhuru Sirichwa division haijawahi kupata maji ya bore hole.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Ile maji tunategemea ni ya Ewaso Nyiro.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Hiyo maji ya Ewaso Nyiro ni district saba inategemea.

**Mzee Sora:**

**Translator:** na wanyama na kila kitu. Ile system ingine yote iko hapa duniani, watu saba peke wanatumia hiyo maji.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee amependekeza iwekwe katika Katiba hiyo maji hawa watu wote wakose na watu saba wafaidike, iwekwe katika Katiba hii maji iwe ni ya kila maisha.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Ya pili sisi ni wafugaji.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Sisi kama wafugaji Northern Kenya, wale wanaishi yote Eastern na North Eastern hatuna haki hiyo ya wanyama.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Wacha kitu ingine hata hii dust, I mean ardhi ambaye mama, babu yetu yote imezaliwa hapa tunaambiwa sio yenu ni Trustland.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mimi kwa ufupi nimemaanisha Trustland ni kusema nyinyi wale wafugaji wale wanaishi kwa Trustland mumepatia mkuki, bunduki mpigane juu.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee amependekeza hii ardhi iwe kikamilifu ni ya wale wanaishi ndani, sio Trustland irudishwe jina kama community land.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Ukiangalia mfano wa Wakenya wengine, wale watu wa kahawa, ya majani chai, wale wanaweka viazi kila moja iko na factory yake.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Na hiyo hiyo factory yote vile wewe unajua nawekwa katika ile mahali hiyo vitu inapatikana kwa chai kwa chai, kwa majani kwa kahawa kwa kahawa.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Haki, kama sisi tungepata haki kama wengine hiyo K.M.C ambaye imewekwa hapo Athi River, na hii ya Mombasa, badala ya huko ingeletwa hapa katika hapa pahali inapatikana hiyo nyama yani kwani ni Siricho, Garbatula, Marti au Wajir District.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Anasema sasa ukisafirisha wanyama mpaka Athi River au Mombasa, transport peke yake tunagawanyana na ile bei ya ng'ombe kama ni elfu kumi, elfu tano ni ya transport na elfu tano anapata.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Siyo haki na anapendekeza hiyo machine ya K.M.C iwe hapa mahali nyama inapatikana.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Vile hii wanyama yetu na nyama yetu ipate soko.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Tena mfano ingine ni maziwa ya ngamia, mbuzi ya ng'ombe na hata hiyo vile vile haina soko na hakuna faida yoyote.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee anapendekeza hata hiyo iwekwe hapa karibu maziwa hii yetu tuihifadhi. Hii maziwa ikiwa fresh sisi nasikia mwingine anatolewa mafuta hiyo mafuta pia inakua faida, maziwa pia inatumika, vile vile hata sisi tuwekewe hapa karibu na hizi tarafa hizi ziko na wanyama tupate hiyo K.C.C.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Ya nne anasema, hata ingawa kidogo wakati ya ukoloni sisi tumepitana na serikali, baada hii ya mambo mengi sisi tumejamini ya kwamba tumepata uhuru na tuko kama wengine.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Sisi watu ya Isiolo district ambao tunajiamini tu s/isi ni wakenya moja lakini hatuna hiyo haki.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Kuchukua hii jukumu ya kuongoza serikali, u/kiwa serikali wewe unapaswa kuchukua haki yote. Yani barabara unatengeneza, maji inapatikana mahali, kila kitu yani watu wapate huduma yao kwa mahali wanahitajika.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Ya maj/i, hata wewe mwenyewe ni shahidi, kama vile unajua hapa maji hakuna, ile iko nayo si mzuri umebeba maji yako, moja example uko nayo, ya pili barabara nayo umeona wewe mwenyewe umeshuhudia ukatembea nawe ukaona vile barabara inakaa.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee anasema mambo ya maji kama utakubaliana na mimi, kama kweli ni maji ile mimi nakunyua hapa na iko kwa jerrycan nitakuletea sasa hivi wewe mwenyewe Commissioner tafadhali kunyua.

**Mzee Sora:**

**Com. Muigai:** Nimekubaliana na wewe.

**Mzee Sora:**

**Com. Lethome:** Lete, nitakunyua, nitasema tu Bismillahi nitakunyua

**Mzee Sora:**

**Translator:** Anasema wewe unaamini dini labda hii jina ya Mwenyezi Mungu kusema Bismillahi umeamini na unaweza kunyua lakini mwenzako Commissioner mwingine hata kama labda anatoroka maji, ametoroka hayuko hawezi amini hapa ni kama mahali ya wanyama wanaishi achukua hivyo.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Sisi tuko na shida hii, uhuru uhuru tunaita, hakuna ile kitu tumepeata ndani yake.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Uhuru ya kwanza ni usalama, kama usalama hakuna, hakuna mambo, kazi yoyote hakuna maendeleo yoyote.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Tulikosa namna, hakuna ulinzi, hakuna security tuliomba serikali tunapewa bunduki sasa kwa raia, raia wanatembea kwa bunduki wanachunga sisi.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Ile ya serikali inashinda kutosha, sisi natoa ng'ombe nanunua bunduki tunajichunga sasa na bunduki yetu.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Hakuna ile kabilia inaishi hapa Kenya na hawana bunduki ile yao ya kujichunga.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee amependekeza hii ya security kama vile sasa tumeiba na tuko na bunduki, na tunaweka ile kuficha bunduki na amependekeza serikali ahalalisho hiyo bunduki sisi tujichunge nayo, badala ya kujificha naye ndani ya porini tujitokeze naye nje iwe kwa Katiba katika Kenya kila mtu awe ana ulinzi yake anakuwa na bunduki yake ya kujichunga iwe halali. Hiyo ni kianzio.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee anasema ye ye ni mzee wa viti na chief alikuwa hapa, a very senior chief ambaye leo huyo chief mahali aliwakilisha, leo inawakilishwa na ma-chief wanne na ye ye alikuwa anawakilisha hiyo location yote nne pamoja kama division nzima anawakilisha.

**Com. Lethome:** Haya okey dakika mbili ingine chief , endelea.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Nitaguzia kwa serikali kidogo.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Wale watu wamezungumza mbele yetu, wasema wanataka jimbo.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Hata pia mimi niwaunga mkono.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mzee anasema, kama vile tunafanana si Tana River, Marsabit, Moyale na Isiolo district ziwe kama region moja.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Kama vile wengine wanasema, council, local government ipatiwe nguvu kabisa.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Na katika Kenya, yule mtu anataka kuwa President asiwe mjumbe, awe ni President tu na anachaguliwa na wananchi.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Anasema local government ikishikanishwa pamoja na administration, chief na assistant chief, sasa hii itakuwa ni ile serikali ya ndani kabisa na itakuwa inalekea vizuri.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Hata mila yetu tuko nayo.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Hata katika mila yetu iko. Wakati wa ukoloni, wale wazee wanafanya na chief, chief wako na power ya kuwaandika na kuwalipa kitu kidogo lakini leo hii wanaweza kuwaandika lakini hawana kitu ya kulipa.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Na up keep ya wazee lazima iangaliwe.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Iko kimila yetu ya asili ya Waborana ya kabisa kabisa ya Borana. Hii judiciary ilipoanza, kotini ilianza, yote ikapotea.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Hii korti inamaliza umaskini kabisa na hata tajiri anapunguzia mali.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Maskini atahudhuria mara mbili hiyo kortini case asikie mara ya tatu yeye mwenyewe atakubali ataondoa mkono kwa sababu hana la kufanya naye atasema mimi nimekubali na anafungwa.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Kimila yetu, hata kama ni kesi aina gani itakuwa siku moja siku ya pili inakwisha.

Kwa ufupi katika kimila yetu hakuna gharama yoyote kwa kesi inasikika. Watu wanaweza kuja kwa kesi waangalie kati ya fulani na fulani na makosa yake inaangaliwa bila gharama yeyote ni wazee wanakuja wanakalia wanaangalia na hiyo kesi inamalizika vizuri bila gharama yeyote. Kama ingine sasa unaona sheria ya Kenya mtu mpaka anashika wakili, anafanya nini, sijui anafanya court of appeal, sijui nini, watu wanafungana hakuna.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Constitution ikubali ada ya Borana ile sheria ya Borana, Katiba ya Borana pia iwe ni kama Katiba ingine, iwekwe katika Katiba.

**Com. Lethome:** Haya asante sana mzee, sasa maliza tafadhali.

**Mzee Sora:**

**Translator:** Mimi najua hata wewe mwenyewe programme vile imeanza na watu wengine wako hata hatujafikia na wiki nzima tulikuwa tukishughulika tu na mambo hii ya Katiba, Katiba, Katiba wiki hii yote tangu juzi hawa watu wa Trustland na (?) walikuja kutujulisha.

Mzee Sora:

**Translator:** Kwa vile tulikuwa na hamu zaidi ya hii Katiba usiku na mchana tulikuwa tukikalia hii mambo sheria tu tunazungumza.

Mzee Sora:

**Translator:** Ndiyo tulikuwa na hamu zaidi kwa sababu tangu hii mwaka thelathini na tisa hakuna siku tuliambiwa hii sheria yenu namna hii namna hii lakini leo vile tulikuwa na hamu zaidi ndio tulijishughulisha zaidi.

Mzee Sora:

**Translator:** Amri ya Mwenyezi Mungu Alihamdila tumekutana sisi hapa na mumeandika ile mambo tumezungumza yote maoni yetu yote tumechukua sasa amri ya Mwenyezi Mungu wewe ndiwe uko nayo.

Mzee Sora:

**Translator:** Anasema sisi watu ya Isiolo district tumebahatika sana, sijui kama Garbatula na kila eneo ni wewe tu utaendelea kwa vile wewe ni mwislamu ndugu zetu. Tumepata maoni nzuri na umetusikia vizuri na shukuru zaidi.

Mzee Sora:

**Translator:** Tena serikali inachagua wewe kama muislamu tena kwa wale watu Islamu tena wafugaji na wewe nafikiria unajua mambo ya mifugo anasema, tumebahatika sana, nashukuru zaidi.

## Mzee Sora:

**Translator:** Tutakuombea Mungu hii kazi tunakupatia iwe ni ya kitendo sio paper work na sisi tunakuombea Mungu vile tumeandika imeingia na Ibrahim (?) tunakuombea utafanya namna hiyo.

**Com. Lethome:** Asante sana.

**Mzee Sora:** Basi sina mengi ya kusema salaam aleikhum (?) Abarakate!

**Com. Lethome:** Waleikumsalam. Kwa hayo machache tunamshukuru. Sema jina lako.

**Mr. Shar Ahmed:** Salaam aleikhum (?) Wabarakatu. Hapa kweli leo sisi tumeshukuru sana kwa Wataalah

**Com. Lethome** : Anza kwa jina lako tafadhalii.

**Mr. Shar Ahmed:** Naitwa Shar Kur Ahmed.

**Com. Lethome:** Shar Kur Ahmed?

**Mr. Shar Ahmed:** Shar Kur. Kweli fursa hii ya leo tunashukuru sana Allah (?) , sisi hatujawahi pata fursa hii. Fursa hii leo, mwaka thelathini na tisa sisi bado pata maisha yetu. Leo sisi mfugaji kama si mfugaji Kenya iko watoto arobaine na mbili, khabila arobaine na mbili tuseme watoto arobaine na mbili sisi iko nayo. Watoto arobaine na mbili hao, thelathini na saba kama nalia nakimbia kwake nasema nani napiga wewe nakimbia kwake na watoto tano hawangaliwi hata kama wanapigwa na nani. Hata kama wanapigwa na nani, manyatta imevamiwa na shifta, majambazi , haangaliwi. Tunakimbia kwa polisi, polisi tunamwambia hebu tuangalie sisi tumenyanyaswa na shifta, majambazi, hebu tukimbie kwetu, polisi nacheka ha! ha! ha! Ala! Siu ujiokoe, nyinyi mwenyewe shika bunduki yenu, si ujiokoe, naaangalia sisi na macho. Kweli kweli hiyo ni haki? Hapana. Serikali nasema, sisi ndiyo tulisaidia nyinyi usiku na mchana, usiku na mchana sisi iko (?) yenu tunasaidia nyinyi wanaambia sisi, na haangalii sisi. Kweli sisi tunahitaji serikali ya Kenya haoni sisi. Tunahitaji serikali ya Kenya aone sisi. Aangalie sisi kama watoto thelathini na saba hao wakati analia nakimbia kwake watoto tano haangaliwi kwake. Turkana , Samburu Rendille, Borana, Somali haangaliwi. Yani hapana angalia sisi. Mali yetu sisi wafugaji, hawezi kupelekwa soko, angalia soko, majani napelekwa soko, Kenya Rais mwenyewe anakwenda kutafuta wapi, nakwenda mpaka Afghanistan nakwenda kutafuta bei ya majani, ya nini mali yetu hawezi kuangalia soko, hawezi kutafutia soko. Sisi hapana watoto ya Kenya? Iko sisi kweli shamba ingine? Si mali yetu ni hii tu.? Iko mali ingine sisi kweli? Si mali yetu ni hii? Yani hapana tafutia sisi soko. Sisi iko ng'ombe, iko mbuzi, iko ngamia! ya nini hapana tafutia sisi soko kweli. Tunahitaji hapo serikali iangalie sisi.

Barabara yetu angalia vile inakaal! Siku ingine bado pitika hii barabara. Nasemekana nyinyi hii ni mali yenu. Mali yenu siku ya njaa naichukuliwa fee. Fee hii napelekwa wapi? Fee ya serikali nachukuanga hii napeleka wapi. Mbuzi nachukuliwa mbuzi moja shilingi thelathini, ng'ombe nachukua mia na thelathini, ngamia namna hiyo, punda namna hiyo napeleka wapi hii pesa ya fee? Napeleka wapi? Miaka thelathini na tisa yote napeleka wapi pesa hii. Serikali ya Kenya nakwenda kujenga ardhi yao haangalii ardhi yetu. Barabara yetu tunahitaji msaada. Iko wapi serikali ya Kenya yani hapana ona sisi? Rais Daniel Arap Moi kila mwaka anakwenda kutafuta pesa wapi? Naenda kuto nchi za nje. (?) yeye na kwenda kuchukuanga, nachukua na jina yetu. Napeleka hii pesa wapi? Hawezi kujenga ardhi yetu. Iko wapi pesa hii? eh! kweli iko wapi pesa hii? tunahitaji (?) . Tunahaki ya kuongea haki yetu! tunahitaji. Unajua inasemekana kwa wale wansema ( in local language) kila mbwa iko siku yake, leo siku yetu imeingia, na sisi iko haki ya kuongea kweli. (clapping) Au kama sisi bado pata uhuru wa kuongea tuelezwe!

**Com. Lethome:** Iko.

**Mr. Shar Ahmed:** Kama sisi iko huru ya kuongea haki yetu sisi tunahitaji

**Com. Lethome:** Iko, iko uhuru ya kuongea.

**Mr. Shar Ahmed:** Eh! haki yetu tunahitaji. Sisi watoto tano tunanyanyaswa, tena hasa mtu naitwa Somali. Iko kadi ingine nawekwa hapa shingo naitwa screen card kama (?). Screen card naitwa, nawekewe shingo nasemakana hiyo shingo ni ya Somali pekee yake. Hebu angalia watoto ngapi? Watoto arobaine na mbili kitu gani hiyo peke yake natoa kando eh! Hawa watoto, watoto tano hii, serikali ya Kenya haoni kabisa. Haoni, haangalii kabisa hawa watoto. Tunahitaji haki yetu, tunahitaji haki yetu, atupatie. Kama sisi iko haki kweli, tupatiwe, haki yetu. Mimi nimetokea hapa ahsanteni sana. (*clapping*)

**Com. Lethome:** Tunashukuru sana Bwana Bishar Bukuru. Na nafikiri sasa tunafikia mwisho wa kikao chetu cha leo, lakini kabla hatujafunga, kuna swalii ambalo watu wengi wanauliza. Hebu kidogo tusikizaneni, kidogo nitawapa nafasi baada ya hapo mtazungumza mpaka asubuhi, Inshallah! Kwanza tunashukuru kabisa kwa vile mmejitokeza na maoni yenu ambayo tumeyachukua lakini mimi najua kuna wasiwasi ambao watu wako naye kwa sababu ya matatizo ile ambao wamepitia hasa watu wa Northern Kenya. Nimezunguka North Eastern, Alhamdulilahi tangu nilipoanza hii kazi, North Eastern na pande hizi za Moyale, Marsabit na Sololo, nimezunguka sana. Najua watu wa huku wanashaka, wana wasi wasi kitu yoyote ambayo inatokana na serikali, wanaweza kuwa na shaka ama sivyo. Hata kuna mzee mmoja pande za Buna karibu na Bute huko alitwambia wewe unataka kutuambia kuwa

(?) ameamua kutokula panya tena? Amenyoa masharubu na amekata kucha. Haiwezekani nyanyor awache kula panya. Lakini tunataka kuwaambia hivi,

(?) ni panya eh!

**Crowd** : Nyarnyur ni paka.

**Com. Lethome:** Nyarnyur ni paka. Sasa ningependa kuwashakishia hivi, kuna mtu hapa ameuliza, Commission nyingi zimefanya kazi, lakini hatujaona matokeo yake. Ni kweli kabisa. Lakini nataka kuwashakishia kwa niaba ya commission hii ya marekebisho ya Katiba, hii ni Commission ambayo ni tofauti na Commission zingine zote. Hizo zingine huwa zinaundwa na Presidential decree, Rais mwenyewe anaamua kutengeneza Commission. Hii imeundwa through an Act of Parliament sheria ambayo imepitishwa katika bunge na hiyo sheria imepitishwa baada ya negotiations watu wamejadiliana, wakajadiliana, ndio wakakubaliana hiyo sheria iundwe. Na hiyo sheria imetulazimisha sisi kuja mpaka hapa. Kwa tumeacha hiyo manyumba kubwa kubwa Nairobi, mahali iko maji safi, wacha ile mzee ananiambia maji ya hapa, tungekaa huko, tutengenezee huko na tuandike, si mawakili wako huko wamejazana? Lakini sheria imesema lazima mwende huko chini mkachukue maoni ya watu. Sasa swalii ni hili, kuna hakikisho gani kuwa baada hii maoni yenu kuchukuliwa haitapotelea hapa njiani? Pengine itafika hapa kula mawe ikule mawe pia ipotellee hapo. Sasa tunawaambia sheria imetulazimisha baada ya kuchukua maoni, hebu angalia vile tunachukua, kuna mtu anaandika pale kwa mkono mimi ninaandika, mimi saa zingine inanipita, yule pale na mashine, hata ukikohoa inashika. Na akifika huko ofisini lazima aende huko, ana compare ile list iko pale ile ameandika, na huyu hapa ile

ameandika, na mimi ile nimeandika na ile yake. Isipotee maneno hata moja ndani yake. kisha baada ya hapo, itaandikwa kwenye report na hiyo report itarudishwa kwenu kwa muda wa miezi mbili. Munaona vitabu kama hii nyekundu ambayo tumegawanya. Itarudi kwenu itazunguka miezi mbili, labda uwe umelala ndiyo itakupita. Hiyo ni ya kukupatia nafasi wewe kama mwanachi uangalie ile maoni ulitoa imefika ama haikufika, ama imebadilishwa huko. Bila shaka tutabadilisha tuandike kwa lugha ya kisheria, hatuwezi kuandika vile unavyosema, tutaandika kwa lugha ya sheria lakini mtaangalia muone maoni yenu yamefika ama hayajafika. Kwa hivyo hiyo ni -step- ya kwanza kuhakikisha maoni yako yamefika.

Step ya pili, kuna Conference ambayo tumeiita National Constitutional Conference kongamano ya kitaifa kuhusu Katiba yani ni mkutano, kongamano ni lugha ya coast lakini Swahili ya bara tunasema mkutano. Katika huo mkutano tunataka wawakilishi kutoka katika kila district. Kila district itatoa watu watatu. Waende kwenye hiyo conference kwenda kujadiliana ile maoni ambayo itapita ipelekwe bunge kabla hatujapata Katiba mpya. Kwa hivyo mtakuwa na watu wenu watatu kutoka Isiolo district na mmoja atakuwa ni mama. Mama mmoja na wanaume wawili watatoka katika kila district waende kuwaakilisha. Kuna ula Maudin, wazee wa dini pia wana nafasi yao. Kama ni Wakristo, Waislamu na dini zingine zote watakwendwa huko. Wajumbe wote mia mbili ishirini na mbili wote watakuwa huko kwa hivyo mjumbe wenu pia atakuwa katika hiyo conference. Conference itaendelea kwa muda wa miezi mbili sio conference, sio mkutano ya siku moja au mwezi mmoja, miezi mbili, siku sitini. Kupitia hiyo report moja moja, moja moja, ile mambo watu watakubaliana itapita.. ile ambayo watu hawatakubaliana, tutaingiza katika kura ya maoni tunaita referendum. Kwa hivyo kuna nafasi karibu tatu ya kuweza kupitia hii maoni yako kuhakikisha kuwa imefika huko. Na ndiyo tunasema hivi, ikifika wakati wa kuchagua district representatives, mchague watu ambao, msichague mtu kwa sababu ni tajiri, pengine au pengine (?) ni mnene ama nini, chagueni mtu ambaye ana akili ya kuweza kuwaakilisha huko, katika hiyo conference. Kwa sababu ikipita kwenye conference itapita itaingia bunge. Ikikataliwa hapo, haitapita hapo. Kwa hivyo ni muhimu sana mjue hivyo na makae tayari kungoja report yenu irudi. Hii ndiyo province ya tatu sasa Eastern, tukitoka hapa tunaenda Nairobi province, tukitoka hapo tunaenda North Eastern, halafu Nyanza halafu Western, tukisha maliza report inarudi kwenu tena. Lazima vijana wenu wale ambao wamesoma na viongozi wenu waweze kusoma hiyo yote na kuangalia ni maoni yenu gani ambayo imepita. Sijui kama tumefahamiana hapo? Kwa hivyo, mpaka hii Katiba mpya itoke, msilale lazima muwe macho. Kama vile mzee ananiambia hii ni amana, na mimi nawaambia pia ni amana hata nyinyi. Kwenu pia ni amana kwa sababu umengojea wewe miaka thelathini na tisa. Huyu mtoto atangojea miaka ngapi na hii sheria? Tukitengeneza mbaya, tunamdhulumu huyo mtoto, miaka mia mbili ingine. Hiyo ni amana pia mbele ya Mwenyezi Mungu utaulizwa tena wewe mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, hii nafasi, hata kama nyinyi mumeumia miaka hii yote thelathini na tisa, msiwache hawa watoto waumie miaka hamsini ingine lazima tuwatengeneze sheria nzuri ambayo itakayo saidia kwa hivyo misiseme tumemaliza, watu wa Modagashe tumemaliza sasa tukalale, hapana, hakuna kulala mpaka tupate sheria mpya. Na sheria mpya ikipatikana, lazima tuhakikishe imefuatwa, ama sivyo? Kwa hivyo ndugu zangu tunawashukuru sana kwa kutulia na kutusikiza na kesho inshallah tutaondoka kwenda Garbatullah bado tuko Isiolo district mpaka tarehe ishirini na moja ndio tutamaliza Isiolo district halafu tutaingia sehemu nyininge ya Eastern. Kuna watuwengine wako pande ya North Hor, saa hizi na Marsabit na Moyale wako huko, kwa hivyo bado tuko hapa na maoni mnawenza kuleta hata Nairobi, mnawenza kuleta Isiolo kwa ofisi ya district Cordinator, itafika huko na tunaweza kuyapokea. Kwa hivyo tunashukuru sana Mwenyezi Mungu

awabariki tunaomba Sheikh mmoja atufungie kwa dua inshallah! Sheikh Abdi Ali, hebu tufungie kwa dua halafu tumalize . kama kuna matangazo yoyote kutoka kwa district coordinator atawaambia.

**Sheikh Abdi Ali:** Dua (In Islam).

The meeting ended at 6.00pm. That was the end of the hearings in Modagashe.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&